Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA ISHIRINI

**Kikao cha Tano – Tarehe 13 Juni, 2005**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

*D U A*

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 41

**Ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Wilaya**

**MHE. JUMA S. KIDUNDA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilitenga fedha za kusaidia ujenzi wa ofisi na nyumba za kuishi zilizotangazwa pamoja na za Wakuu wa Wilaya ya Kilindi mnamo mwaka 2002.

(a) Je, ni kwa kiwango gani cha ujenzi kimekamilika hadi sasa katika kila Wilaya iliyopewa fedha hizo?

(b) Je, ni asilimia ngapi ya fedha iliyotumika hadi sasa ikilinganishwa na asilimia ya kazi iliyokwishakamilika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kidunda Juma Mbunge wa Kilindi lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003 Serikali ilitangaza kuanzisha Wilaya mpya kwa kuzigawa baadhi ya Wilaya mara mbili, Wilaya mpya zilizoanzishwa ni, Kilolo, Kishapu, Mvomero, Namtumbo, Kilindi, Ilemela na Nyamagana iliyorithi iliyokuwa Wilaya ya Mwanza. Kwa kuwa Wilaya hizo ni mpya

Serikali ililazimika kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi na nyumba za Wakuu wa Wilaya hizo kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wilaya ya kilolo kwa kipindi cha mwaka 2002/2003 fedha zilizokuwa zimetolewa ni Tshs. 200,000,000 kati ya Shilingi m 2,002,678,571.40 zilizokadiriwa kugharamia ujenzi wa Ofisi. Fedha zilizokwishatumika hadi sasa ni Tshs. 113,500,000 sawa na asilimia 56 ya fedha zilizokadiriwa. Ujenzi umefikia hatua ya kupaua, kuweka *frame* za milango na madirisha. Ujenzi wa nyumba mpya ya Mkuu bado haujatengewa fedha.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kishapu, kipindi cha 2003/2004/2005, jumla ya fedha zilitolewa ni shilingi 100,000,000 kati ya shilingi milioni 100,000,000 zilizokadiriwa kugharamia ujenzi wa Ofisi. Fedha zilizokwishatumika hadi sasa ni Tshs. 79,657,650.90 sawa na asilimia 79.6 ya fedha zilizokadiriwa.

Ujenzi wa Ofisi umekamilika kwa asilimia 100 na shilingi milioni 20,342,349.20 zilizobaki zimeanza kujenga nyumba ya Katibu Tawala wa Wilaya. Ujenzi wa Nyumba ya Mkuu wa Wilaya umeanza na utakamilika mwaka ujao wa fedha 2005/2006. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mvomero kwa kipindi cha mwaka 2003/2004/2005 jumla ya fedha zilizotolewa ni *T.Shs. 100,000,000* kati ya Shilingi milioni 300,000,000 zilizokadiriwa kugharamia ujenzi wa Ofisi awamu ya kwanza. Fedha zilizokwishatumika hadi sasa ni shilingi 68,635,560 sawa na asilimia 42 ya fedha zilizokadiriwa. Ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa Wilaya hadi hivi sasa haujaanza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wilaya ya Uyui, kwa kipindi cha mwaka 2003/2004 na 2004/2005 jumla ya fedha zilizotolewa ni Tshs. 240,000,000 kati ya shilingi 356,000,000 zilizokadiriwa kugharamia ujenzi wa Ofisi. Fedha zilizokwishatumika hadi sasa ni jumla ya Shilingi 138,400,500 sawa na asilimia 38.9 ya fedha zilizokadiriwa na asilimia 68 ya fedha zilizokwisha kutolewa. Kazi zinaendelea ni upauaji na kuweka milango na madirisha. Kuhusu Nyumba ya Mkuu wa Wilaya TShs. 56,000,000 zimetolewa katika mwaka wa Fedha 2004/2005 na kazi ya ujenzi imeanza tarehe 27/4/2005.

Mheshimiwa Spika, Wilaya na Namtumbo kwa kipindi cha mwaka 2003/2004/2005 jumla ya fedha zilizotolewa ni shs. 100,000,000/= kati ya Tshs. 201,006,467.75 zilizokadiriwa kugharamia ujenzi wa Ofisi.. Fedha zilikwishatumika hadi sasa ni Shilingi 74,408,960.30 sawa na asilimia 37 ya fedha zilizokadiriwa. Jengo sasa limekwishapauliwa. Nyumba ya Mkuu wa Wilaya, imekamilika na iko katika kipindi cha marekebisho *(defect liability period)* katika kipindi cha 2003/2004/2005 fedha zilizotolewa ni Shilingi milioni 100,000,000 na zilizotumika ni 83,741,243.80.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilindi katika kipindi cha mwaka 2003/2004/2005 jumla ya fedha zilizotolewa ni Shilingi 160,000,000 kati ya 160,000,000 zilizokadiriwa kugharamia ujenzi wa Ofisi. Fedha zilizokwishatumika hadi sasa ni shilingi 109,456,087

sawa na asilimia 70 ya fedha zilizokadiriwa. Mkandarasi anatarajia kumalizia kazi za ujenzi tarehe 1/8 na kukikabidhi sehemu ya malipo yaliyobaki.

Kuhusu ujenzi wa Nyumba ya Mkuu wa Wilaya Mkandarasi, anatarajia kumalizia kazi za ujenzi tarehe 18/7/2005 amekwishalipwa kiasi cha shilingi milioni 13,000,000 ambacho ni sawa na asilimia 27. Wilaya ya Ilemela kwa kipindi cha 2003/2005 jumla ya fedha zilizotolewa ni Shilingi 90,000,000 kati ya Shilingi 300,000,000 zilizokadiriwa kujenga Ofisi. Fedha zilizotumika ni Shilingi 45,000,000 kwa ajili ya kujenga msingi na 45,000,000 zilizobakia zitajenga boma na kuezeka. Hata hivyo zitahitajika milioni 62,000,000 za ziada ili kukamilisha ujenzi.

Mheshimiwa Spika, jitihada zote hizi za ujenzi wa Ofisi na nyumba za Wakuu wa Wilaya, ni kielelezo dhahiri kwamba Serikali imedhamiria kwa dhati kuboresha mazingira ya kazi si kwa Wilaya mpya tu bali na kwa Wilaya zote nchini. (*Makofi*)

**MHE. JUMA S. KIDUNDA**: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali lenye vipengele viwili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa mazingira ya Makao Makuu ya Wilaya, hizi mpya ni mazingira ya Vijiji na kwa kuwa baada sasa Vijiji hivyo kuwa ni Makao Makuu ya Wilaya, watendaji wengi wa Serikali Kuu pamoja na Serikali za Mitaa wanahitajika kwenda kukaa katika Vijiji hivyo. Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia fedha zake zinazotokana na mpango wa kuuza nyumba za Serikali na kujenga mpya ili kusudi kujenga nyumba mpya za kutosha katika Makao Makuu ya Wilaya hizi ili kusudi Wafanyakazi hao wapate mahali pa kuishi? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa kwa mujibu wa sensa ya 2002 Wilaya ya Kilindi, ndiyo pekee katika Wilaya zote nchini ambao wakazi wake wote hukaa katika mazingira ya kijiji na kwa kuwa Vijiji ambavyo vina watu wengi kwa vile Kibilashi, Kwejiboma, Muswaki, Negelo na Kilindi, je, Serikali haioni vema kutumia fedha zinazotokana na uuzaji wa nyumba za Serikali kuelekeza baadhi ya fedha hizo katika Vijiji hivi ili kusudi wananchi wa Kilindi nao waweze kuishi katika mazingira ya miji kama wananchi wenzao Tanzania? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Kidunda kama ifuatavyo:-

(a) Nyumba za Wakuu wa Wilaya haziuzwi na zinaongezewa kujenga nyumba hizo popote ambapo makao Makuu ya Wilaya mpya zinajengwa na hizo nazo zitajengwa na hazitauzwa. (*Makofi*)

(b) Fedha ambazo zinapatikana kutokana na kuuza hizi ambazo tunauza zinaendelea kujenga nyumba kwenye Mikoa na Wilaya. Hivi sasa kutokana na fedha hizo tunajenga nyumba mpya 20 kwenye Mikoa na nyumba mbili kwa kila Wilaya kwa ajili ya viongozi ambao wanahamahama. (*Makofi*)

Na. 42

**Ushirikishwaji wa Wanawake**

**MHE. RUTH B. MSAFIRI** aliuliza:-

Kwa kuwa idadi ya wanawake kwa ujumla wao inazidi asilimia 50 na ndivyo ilivyo katika Vijiji vyetu vingi ambavyo huunda kata na kwa kuwa wanawake ndio wengi wanaokabiliwa na tatizo la kukosa habari, hali inayopelekea ushirikishwaji mdogo katika masuala ya maendeleo na kwa kuwa bado mila na desturi za makabila mengi na imani za baadhi ya dini zinabadilika pole pole sana.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kudumu wa kushirikisha nguvu kazi za wanawake ipasavyo katika maendeleo ya nchi, hasa katika vyombo vya kupanga mipango na mikakati ya maamuzi?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza idadi ya asilimia ya wanawake katika Serikali za Vijiji na mabaraza ya Madiwani walau kufikia asilimia 40 ifikapo mwaka 2005?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Msafiri Mbunge wa Muleba Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba idadi ya wananchi hapa nchini inazidi asilimia 50 kwa mujibu wa sensa 2002 idadi ya wanawake ni 17,613,742 ya Watanzania wote ambayo ni sawa na asilimia 51.08. Serikali pia inatambua kwamba kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo alizozitaja Mheshimiwa Mbunge, kundi hili la jamii bado halishirikishwi kikamilifu katika vyombo vya kupanga mipango na kuamua masuala ya maendeleo yanayogusa maisha yao ya kila siku. Kutokana na mapungufu haya Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuondoa kasoro hizo na naomba nitaje chache.

(i) Ni kutoa upendeleo kwa wananchi katika Elimu, ili waweze kujiendeleza kwa kasi zadi kwa kuwa Elimu, stadi na taaluma

katika nyanja mbalimbali ni nyenzo muhimu inayomuwezesha mwanamke kushiriki kikamilifu katika mchakato wa maendeleo.

(ii) Ni kutoa msukumo zaidi katika suala la jinsia na hili limetekelezwa kwa kuanzishwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ambayo ndiyo inasimamia suala zima la namna ya kuwianisha jinsia zote mbili.

(iii) Kuweka katika dira maendeleo ya taifa ya mwaka 2025 usawa wa jinsia na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi na kisiasa *(gender equality and the empowerment of women in all economic and political relations and cultures)* jambo hili pia limepewa kipaumbele katika sera ya kuondoa umaskini na mkakati wa taifa wa kusimamia utekelezaji wa sera hiyo.

(iv) Ni kuweka idadi maalum ya wanawake katika vyombo mbalimbali ambavyo vinafanya maamuzi na hili naomba niseme tu kwamba katika ibara ya 66 (b) inataja kuwepo kwa Wabunge wa Viti Maalum kuanzia 20 na baada ya marekebisho yaliyofanyika idadi hiyo, sasa itakuwa imeongezeka kwa kiasi ambacho Bunge lilipitisha. Lakini vile vile katika sheria zetu za Serikali za Mitaa nako vile vile viko vipengele vilivyowekwa kutaka Madiwani wa Viti Maalum idadi yao isipungue theluthi moja na katika Mamlaka ya miji midogo isipungue robo. Hali kadhalika kipo kifungu cha 56 katika sheria namba 7 ya mwaka 1982 ambacho kimeweka bayana kabisa kwamba wajumbe wa Serikali ya Kijiji, ambao kwa kawaida wako kati ya 15 mpaka 25 wanaochaguliwa na mkutano wa Serikali ya Kijiji robo ya wajumbe lazima iwe ni ya akina mama.

(b) Mheshimiwa Spika, umuhimu wa kuwa na idadi ya kutosha ya wanawake katika vyombo vya maamuzi katika Serikali za Mitaa, ni suala lililokwisha kupewa kipaumbele siku nyingi kama nilivyoeleza hapo juu. Hivyo rai ya Mheshimiwa Mbunge ni nzuri kwani inaongeza ushiriki zaidi wa wananchi katika vyombo vya maamuzi. Hata hivyo kwa kuwa masuala haya yanatawaliwa na sheria ambazo ili kukidhi ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, vifungu husika havina budi kurekebishwa kwanza ili rai yake iweze kutekelezwa. Litafanyika punde mambo haya yatakapokuwa yametekelezwa.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kunipa taarifa na kuliarifu taifa juu ya taratibu mbalimbali zinazotumika katika kuhakikisha kwamba wanawake wanapata nafasi, napenda kuuliza swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa jamii ya Watanzania yaani wanawake na wanaume bado wamegubikwa na kutokupenda kuwapa nafasi wanawake hasa katika nafasi za kuchaguliwa katika kata na katika Majimbo na hata Urais vile vile. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atanisaidia vipi kwamba sasa itolewe Elimu ya mara kwa mara kwa wanawake, kwa wanaume ili waweze kuelewa kuthamini na kuhakikisha kwamba wanawake walio katika maeneo yao wanapojitokeza basi wawape nafasi za kuweza kushiriki na kupewa nafasi za kuwa katika nafasi hizo walizoziomba? (*Makofi*)

Kwa kuwa nafasi za wanawake katika Serikali za Mitaa yaani Serikali za vijiji pamoja na Baraza la Madiwani siyo sheria bali ni utaratibu uliowekwa na taratibu za kuendesha TAMISEMI. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kukubaliana nami kwamba kwa kuwa uchaguzi wa Madiwani, sasa uko karibu je, anaweza kukubaliana nami kwamba waende wakakae wabadilishe ili walau nafasi za wanawake waweze kufikia asilimia 40 badala ya moja ya tatu au robo ambayo ameisema? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Ruth Msafiri kama ifuatavyo:-

Kuhusiana na hili swali la kwanza najua si rahisi sana kulijibu lakini nitajaribu. Ni dhahiri kabisa kwamba jambo hili ni la pande zote mbili, akina mama wenyewe kwa upande mmoja ambao muda wote Serikali inatoa hamasa kubwa kabisa mjitokeze kwa wingi katika nafasi za Madiwani, Serikali za Vijiji, ili muweze kupata nafasi ya kuchaguliwa. Kwa upande mwingine ni kweli ni masuala vile vile ya *atitude* zetu huko Vijijini ambazo bado zinahitaji kuelimishwa zaidi juu ya jambo hili.

Kwa hiyo, mimi nadhani tukubali kwamba Elimu ni muhimu na ndiyo maana inaendelea kutolewa muda wote, lakini lazima tukubali kabisa kwamba bado vipimo wanavyovitumia wananchi katika kuamua ni vipimo ambavyo vinakwenda hasa hasa kwa kuzingatia uwezo, uzoefu na mambo mengine ikiwemo Elimu.

Kwa hiyo, mimi nafikiri jambo la kufanya hapa zaidi ni kukazana kwanza kwenye suala la Elimu ili akina mama waweze kupata nafasi ya Elimu kubwa zaidi na hivyo kuongezea uwezo. (*Makofi*)

Lakini la pili, kuhusiana na suala hili la Serikali za Mitaa naomba nirudie Ruth Msafiri, kwamba hili nililolitaja hapa wala si suala la Kanuni au taratibu ni sheria namba 7 na namba 8 ndizo zimewekwa matakwa hayo ya Viti vya Madiwani ambavyo ni wa akina mama visipungue theluthi moja kwa kwenye Mamlaka za Miji isipungue robo na katika Halmashauri zetu za Serikali za Vijiji nako wameweka kiwango hicho hicho cha kutokupungua robo. Sasa ndiyo maana nikasema hapa kazi ya kwanza, kwanza ni kurekebisha sheria halafu ndipo mengine haya yafuate. Ingekuwa ni Kanuni tu tungeweza hata leo tukatangaza. (*Makofi*)

Na. 43

**Sera ya Kitaifa ya Tiba ya Asili na Tiba Mbadala**

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI (k.n.y. MHE. EDWARD N. NDEKA**) aliuliza:-

Kwa kuwa moja ya malengo ya mwongozo wa kisera wa tiba ya asili na tiba mabadala ya mwaka 2001 ni kuweka msingi wa kutambua tiba ya asili na tiba mbadala na kwa kuwa ufanisi wa tiba unaimarishwa na huduma bora za uuguzi na ukunga katika mazingira ya uzazi;

(a) Je, ni kwa kiwango gani mwongozo huo katika mwaka 2002 umeweka msingi wa kutambua wakunga wa jadi hususan katika zahanati na kliniki za Vijiji ambako wakunga wa kisasa ni wachache au hawapo kabisa?

(b) Je, ni zahanati na kliniki ngapi zina wauguzi na wakunga wa kisasa na ni wangapi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma na zile zisizokuwa nao zinahudumiwa vipi?

(c) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba, upo umuhimu wa kufanya sensa itakayowezesha kuwatambua wakunga wa jadi wazoefu hususan katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma ambayo kwa sababu ya kijiografia, ukosefu wa barabara na uchache wa vituo vya afya wanawake wengi wanalazimika kujifungulia majumbani jambo ambalo linahatarisha maisha yao hasa uzazi unapoandamana na matatizo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edward Nziriye Ndeka, Mbunge wa Kigoma Kusini, kama ifuatavyo:-

(a) Mwongozo wa kisera wa huduma za tiba asilia na ukunga wa jadi umetambua rasmi kuwepo kwa huduma hizi nchini. Aidha mwongozo huo una lengo la kuunganisha nguvu za mifumo miwili ya tiba asilia na ukunga wa jadi kwa upande mmoja na tiba za kisasa kwa upande mwingine. Haja hii imejitokeza baada ya Serikali kuona kuwa kati ya mifumo hii miwili hakuna mfumo unaojitosheleza. Hata hivyo Serikali haina mpango wa kuwapeleka wakunga wa jadi katika zahanati za tiba ya kisasa kuziba pengo la upungufu wa wakunga wa kisasa pale ambapo hawapo. Badala yake pengo hilo litazibwa kwa kuajiri Wafanyakazi wapya na mafunzo yatatolewa kwa wakunga wa jadi ili kuboresha stadi zao za kazi na wataendelea kutoa huduma zao katika misingi yake ya asili.

(b) Mheshimiwa Spika, takwimu tulizonazo za mwaka 2003/2004 zinaonyesha idadi ya kliniki za afya ya mama na mtoto za Kigoma Vijijini ni 69 na zina idadi ya wauguzi/wakunga 18 ambao wote hao hutoa huduma za kisasa. Aidha kuna zahanati ambazo hazina wauguzi/wakunga ila zinahudumiwa na *MCHA* (Wauguzi/Wakunga Vijijini) ambao pia wanaujuzi wa kazi hiyo.

(c) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba upo umuhimu wa kufanya sensa ya *TBAs* (Wakunga wa Jadi) ili waweze kupatiwa mafunzo na hivyo kuweza kutoa huduma za ukunga kwa ufanisi zaidi hususan kwa maneno yasiyoweza kufikika kwa urahisi. Jambo hili limeanza kufanyika kwa awamu katika maeneo mbalimbali. (*Makofi*)

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri. Namshukuru kwa kutambua kwamba mafunzo ni muhimu sana kwa wakunga wa jadi.

Kwa kuwa mafunzo mengi yanayotolewa kwa wakunga hawa ni ya muda mfupi sana na hayakidhi haja za wale ambao wangependa kupata huduma za wakunga hawa na kwa kuwa upo mfano hai katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma, ambapo kuna wakunga wa jadi kama vile Bi. Tatu Salum, Mariam Rajab na Margaret Ruben, wanaotoa huduma nzuri sana katika Halmashauri hiyo na kwa kuwa mafunzo yaliyowahi kutolewa kwa watu hawa yalikuwa ya siku moja tu, je, Waziri haoni kwamba siku hiyo, moja ilikuwa haitoshi na unahitajika muda mrefu zaidi wa kuwapa mafunzo mazuri zaidi ili waweze kutoa huduma nzuri zaidi? (*Makofi/Kicheko*)

Kwa kuwa vitendea kazi muhimu kwa wakunga wa jadi hawa ni pamoja na mipira ya kuvaa mikononi, chemli, mafuta ya taa, miavuli, fomu za kutunzia kumbukumbu za vizazi. Je, chini ya sera ya uuguzi wa ukunga ya 2002, Serikali inatoa maelekezo gani kuhusu upatikanaji wa vitendea hivyo vilivyotajwa ili wakunga hawa waweze kutoa huduma nzuri zaidi katika Vijiji vyao? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Mporogomyi kama ifuatavyo:-

Mafunzo kwa ajili ya wakunga asilia yanatolewa kwa vipindi tofauti. Ninakubaliana naye kwamba iko haja ya kuwapa mafunzo kwa muda mrefu lakini kama nilivyosema katika jibu langu la msingi jambo hilo limeanza na sasa hivi Wizara ya Afya ina mpango wa kutoa mafunzo hayo kwa kipindi kirefu kidogo kuliko hiyo siku aliyoitaja. Aidha nataka nichukue fursa hii niwashukuru kwa dhati washirika wetu katika sekta ya afya ambao wamekuwa wakifanya kazi kama hiyo wakiwemo *UNICELF* na Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu vitendea kazi nataka nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge, kwamba mafunzo haya yanaendana na kutolewa kwa vitendea kazi

alivyovizungumza. Hivyo kila sehemu ambayo sasa hivi Wizara ya Afya inatoa mafunzo kwa wakunga wa jadi wakunga hao vile vile hupatiwa vitendea kazi kwa ajili ya kuboresha huduma wanazozitoa.

**MHE. BERNADINE R. NDABOINE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa zahanati nyingi za mkoa wa Kigoma kama siyo zote hazina vitanda maalum vya kujifungulia na hivyo kusababisha matatizo ya migongo kwa akina mama ambao huwa wanajifungua. Je, Serikali itakuwa tayari kuzipatia zahanati za Mkoa wa Kigoma vitanda hivyo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ndaboine kama ifuatavyo:-

Nataka nikubaliane na Mheshimiwa Ndaboine, kwamba maeneo mengi hayana vitanda vya kujifungulia. Lakini nataka nilieleze Bunge lako Tukufu kwamba utaratibu wa kuagiza vitanda unatokana na matakwa ya Wilaya husika. Mafungu yanatolewa kwa Wilaya zote kwa ajili ya huduma za mama na mtoto. Kwa hiyo, ni vipaumbele vyao ngazi ya Wilaya ndivyo vinavyopelekea aidha kuagiza vitanda hivi au la. Kwa hiyo, napenda nitoe wito kwa Wakurugenzi wa Halmashauri mbalimbali, ambao zahanati na vituo vya afya hazina vitanda hivi, basi wahakikishe wanatoa kipaumbele ili ziweze kupatikana. (*Makofi*)

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wakunga hawa wanasaidia sana akina mama kule Vijijini, sasa Serikali haioni sasa kuna umuhimu wa kuwajali kuwapa angalau fungu dogo la motisha ili iweze kuwasaidia akina mama hao? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, suala la motisha kwa wakunga wa jadi halina budi kutolewa katika ngazi ya jamii. Wakunga hawa hawako katika kada ya ajira. Kwa hiyo, hakuna Bajeti kwa ajili yao. Isipokuwa ni vema katika kila jamii watu wakahamasishwa kwa kazi nzuri wanayofanya wakunga hawa wakaweza wakawachangia ili angalau na wao wapate motisha ya kuendeleza kazi zao.

Na. 44

**Uongozi Katika Hospitali ya Muhimbili.**

**MHE. ALI SHEHA MUSSA (k.n.y. MHE. ALI AMEIR MOHAMED)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliajiri mtaalam kutoka nje kuongoza uendeshaji wa Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili kwa gharama kubwa kila mwezi:

(a) Je, Serikali inaweza kuelezea ni kiasi gani cha fedha za walipa kodi wa Tanzania zilitumika kugharamia mtaalam huyo kwa muda wote alioajiriwa?

(b) Je, Serikali inaweza kueleza kwa muhtasari tu mafanikio ambayo yalipatikana kutokana na utumishi wa mtalaam huyo?

(c) Je, Mtaalamu huyo bado anaendelea au ameondoka?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed Mbunge wa Donge, napenda kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo;

Serikali iliajiri mtaalam toka Uingerezaa Dr. David Tregoning kwa Mkataba wa miaka miwili toka tarehe 1 Novemba, 2003 kuindesha Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Jukumu kubwa alilopewa Mtaalam huyu ni kuiendesha Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kwa ufanisi. Bodi ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili ilitangaza nafasi hii ndani na nje ya nchi kama taratibu zinavyotaka. Aliyefanikiwa kupata kazi hii alikidhi viwango vyote vilivyotakiwa, vikiwemo Shahada ya Uendeshaji wa Hospitali (*Hospital Management*) na uzoefu wa kuendesha hospitali kubwa ya kiwango cha Muhimbili.

Baada ya maelezo hayo sasa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, Mbunge wa Donge, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

(a) Mheshimiwa Spika, Dr. David Tregoning aliajiriwa kwa mshahara wa shilingi 9,000,000/= kwa mwezi. Serikali ya Tanzania huchangia shillingi 1,000,000/= na Shirika la *Abbot Laboratories* kupitia *AXIOS* hutoa kiasi cha shilingi 8,000,000/=. Hivyo kwa kipindi cha miezi 19 mpaka kufikia Mei mwaka huu Serikali ilikuwa imemlipa Mtaalamu huyu kiasi cha shilingi 19,000,000/=.

(b) Mheshimiwa Spika, mafanikio ni mengi, naomba niyataje baadhi tu kama ifuatavyo:

- Wakurugenzi na Wakuu wa sehemu wa Hospitali hupewa malengo ya kutimiza katika madaraka yao. Hali hii imeleta ufanisi katika utendaji wa kazi hospitalini hapo.

- Kumekuwa na udhibiti mzuri zaidi wa matumizi ya fedha, hivyo kufanya huduma zifanyike bila kukwama.

- Ubora wa huduma umeongezeka kwa kiwango kikubwa.

(c) Mheshimiwa Spika, Mtaalam huyo bado anaendelea na Mkataba wake wa miaka miwili hapo Muhimbili. Hata hivyo Mkataba huu unaisha tarehe *31th October, 2005* na unaweza kuongezwa kwa makubaliano kati ya pande zote mbili yaani Serikali kwa kupitia Bodi ya Hospitali na Dr. David Tiogoning mwenyewe.

**MHE. MZEE NGWALI ZUBEIR:** Mheshimiwa Spika, je, katika utangazaji wa *tender* hakupatikana Mtanzania ambaye anaweza kuifanya kazi hii isipokuwa alipatikana mgeni? (*Makofi*)

Pili, kulikuwa na ubadhirifu mkubwa katika hospitali ya Muhimbili na ndiyo maana wakabadilisha uongozi katika uongozi katika hospitali hiyo. Je, wamechukuliwa hatua gani wale ambao wamefanya ubadhirifu fedha za Serikali? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba nafasi ya Mkurugenzi Mkuu wa Muhimbili ilitangazwa ndani na nje ya nchi. Ni kawaida baada ya kutangaza wanaoomba kuitwa kwenye usajili kwanza kuwa *shortlist* na kuitwa kwenye usaili mambo haya yalifanyika na hatimaye aliyeshinda alikuwa Dr. David Tregoning kwa maana ya vigezo vilivyotakiwa ndiyo alikuwa navyo, bila shaka hakukuwa na Mtanzania mwenye vigezo vinavyotakiwa kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, nataka niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba hii taaluma ya *Hospital Management* kwa bahati mbaya si Watanzania wengi waliokuwa nayo. Hivyo Serikali imeweka azma ya kuanza kufundisha ili hospitali zetu ziweze kuendeshwa na Watanzania wenyewe.

Kuhusu suala la ubadharifu pale Muhimbili, kilichokuwa kinatokea Muhimbili ni *Mismanagement* kwa maana ya kwamba huduma na uendeshaji hauikuwa sahihi na fedha hazikuwa zana zinazopatikana zinavyotakiwa. Toka Tumeanza mabadiliko katika uongozi mambo haya yanaonekana kwenda vizuri na bila shaka nikijibu swali la Mheshimiwa Mbunge ni kwamba hakukuwa na ubadhirifu wa dhahiri isipokuwa kilichokuwepo ni uendeshaji ambao ulikuwa hauridhishi. (*Makofi*)

Na. 45

**Fedha za *STABEX* kwa Ujenzi wa Barabara**

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE (k.n.y. MHE. DR. WILBROD P. SLAA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali kupitia mfuko wa *STABEX* ilipanga kutumia shilingi bilioni kumi (10 bilioni) zilizoletwa na Jumuiya ya Ulaya *(EU)* kwa ajili ya ukarabati wa barabara kwenye maeneo yanayolima Kahawa:-

(a) Je, utekelezaji wa mpango huo umefikia hatua gani na kwamba Wilaya ya Karatu ikiwa miongoni mwa Wilaya zinazolima kahawa kwa wingi imetengewa fedha kiasi gani kwa ajili ya ukarabati wa barabara katika maeneo yanayolima zao hilo hasa kata za Oldeani, Daa, Mbulumbulu na Buger?

(b) Kama utekelezaji umeanza au unategemea kuanza hivi karibuni, je, ni barabara zipi hasa zimeingizwa katika mpango huo na ni mkandarasi gani atakayeifanya kazi hiyo?

(c) Kama utekelezaji wa mradi huo haujaanza, je, ni kitu gani kimekwamisha kuanza kwa utekelezaji huo na sasa unategemea kuanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Wilbrod Peter Slaa, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Jumuiya ya Ulaya kwa kupitia utaratibu wa *STABEX* imetenga jumla ya *Euro* milioni 10 kwa ajili ya ukarabati wa barabara katika maeneo yanayozalisha kahawa kwa wingi nchini. Ili kutekeleza mradi huo, tarehe 17 Aprili, 2004, Jumuiya ya Ulaya iliingia mkataba na Mhandisi Mshauri ya kampuni ya *Roughton International* kwa ajili ya kufanya uchambuzi wa barabara zinazostahili kufanyiwa ukarabati katika maeneo yanayozalisha kahawa kwa wingi nchini. Mtaalam huyo aliwasilisha taarifa yake mwezi Septemba, 2004.

Baada ya kupitia mapendekezo yake, ilionekana kwamba taarifa iliandaliwa bila kuzingatia makubaliano na maelekezo ya mkataba na hivyo ilikuwa na mapungufu mengi. Baadhi ya mapungufu hayo ni pamoja na kutozingatia maeneo yote yanayozalisha kahawa nchini kama mikoa ya Tanga, Kagera, Mara na Kigoma ambayo haikujumuishwa na hivyo barabara za mikoa hiyo hazikuzingatia katika mapendekezo. Upungufu mwingine ulihusu kutohusishwa kwa uongozi wa maeneo yanayozalisha kahawa katika kupendekeza barabara za kufanyiwa ukarabati. Kutokana na mapungufu hayo, Mhandisi Mshauri kwa kushirikiana na *TANROADS* wamefanya tathmini hiyo upya wakishirikisha uongozi wa mikoa inayozalisha kahawa kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya awali sasa napenda kujibu swali la Dr. Wilbrod Peter Slaa, Mbunge wa Karatu, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango wa ukarabati wa barabara chini ya utaratibu wa *STABEX* ulianza mara tu baada ya kusainiwa kwa Makubaliano ya utekelezaji *(Implementation Protocol)* kati ya *TANROADS* na Hazina hapo tarehe 22 Aprili, 2005.

Katika mapendekezo yaliyowasilishwa na uongozi wa Mkoa wa Arusha, hakuna barabara za Wilaya ya Karatu zilizoainishwa kwa ajili ya kufanyiwa ukarabati. Hii inatokana na barabara za Wilaya ya Karatu kutokidhi vigezo au sifa za barabara zinazotakiwa kufanyia ukarabati chini ya utaratibu wa *STABEX.* Sifa hizo ni pamoja na kuwa barabara za

kimkoa *(Regional Roads)* na kuwa na mzunguko wa kuunganisha barabara za kimkoa.

(b) Mheshimiwa Spika, barabara zitakazohusishwa katika ukarabati katika maeneo yanayozalisha kahawa kwa wingi nchini kimkoa ni kama ifuatavyo:-

Mkoa wa Arusha, barabara za *Usa East* hadi Ngarenanyuki, *Masai Camp* (Kijenge) hadi *Usa West* na Monduli hadi Monduli Juu.

Mkoa wa Kilimanjaro, barabara za Kware hadi Lemira; Weruweru hadi Lyamungo, Kawawa hadi Nduoni, Kibosho Junction hadi Mto Sere; Mwanga hadi Kikweni; Mwembe hadi Msindo; Mshiri hadi Kokirie na Holili hadi Tarakea.

Mkoa wa Ruvuma, barabara ya Kigonsera hadi Kilindi na Kilindi hadi Lundu Mbaha.

Mkoa wa Mbeya, barabara za Luanda hadi Nyimbili; Kyimo hadi Sange na Sange hadi Katengale/Kalambo.

Mkoa wa Kigoma, barabara ya Kasulu hadi Manyovu

Mkoa wa Tanga, barabara za Soni hadi Bumbuli na Bumbuli hadi Dindira.

Mkoa wa Mara, barabara ya *Muriba Junction* hadi Kegonga.

Mkoa wa Kagera, barabara za Kagenyi hadi Kyerwa; Kakanja hadi Kikukuru; Kikukuru hadi Kitwe; Kihanga hadi Rwambaizi; Rugu hadi Ruhita; Nyakagoyagoye hadi Rwabwere; Kigarama hadi Mbabira; Mabira hadi Kyerwa, Bugorora hadi Kabingo; Kaibanja hadi Kazinga, Ishunju hadi Rwoya hadi Kibengwe; Kitobo hadi Nyabajwa, Ruhanga hadi Nyakahama, Kanyambogo hadi Rubya na Rubya hadi Ibuga.

(c) Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi wa ukarabati wa barabara hizo ulianza rasmi tarehe 22 Aprili, 2005. Kwa sasa kazi za usanifu, uandaaji wa michoro, nyaraka za zabuni zinaendelea kuandaliwa na Ofisi za Wakala wa Barabara za Mikoa husika. Kazi za ukarabati zitaanza ifikapo mwezi wa Desemba, 2005 baada ya taratibu za kuwapata makandarasi kukamilika. Kazi zote za ujenzi zinasimamiwa na *TANROADS* kwa kushirikiana na Wahandisi Washauri wazalendo *(Local Consulting Engineers).*

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika kwa kuniruhusu kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu kutoka kwa Naibu Waziri

kuhusiana na fedha hizi za *STABEX* nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza ningeomba kujua kwamba kwa sababu suala hili la fedha za *STABEX* limekuwa linaendeshwa katika njia ambayo haielewekieleweki ikiwa na majibu mengi kwa suala hilo hilo moja.

Je, ningeomba kujua ni vikao gani na vinahusisha watu gani ambao wamekuwa wanapanga barabara ambazo zinapaswa kufanyika ukarabati au matengenezo kwa kutumia fedha za *STABEX.* Naomba kujua Wajumbe wanaohusika katika vikao hivyo na watu wa kawaida wamehusishwa kwa kiasi gani na hasa ikizingatiwa kwamba katika orodha aliyoizungumza Wilaya ya Bukoba Mjini haipo pamoja na kutambua kwamba Mkoa wa Kagera unazalisha kahawa zaidi ya nusu ya kawa inayolimwa Tanzania na imetengewa milioni 900 tu? Naomba nipate maelezo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, pesa za *STABEX* ni pesa zilizotolewa na *European Union* wameamua kusimamia pesa hizi wenyewe na wameweka masharti haya wenyewe kwamba tutamchagua mtaalam *Consultant Engineer* yeye atuambie ni barabara zipi zinastahili kutengenezwa kwa kutumia pesa zetu, akateuliwa. Sisi kwetu tumeona ameshindwa. Mikoa mingine hakufanya. Tukakaa nao *European Union* na kushauriana na wakakubali kwamba sasa mtaalam huyu aungane na *TANROADS* kwenda kufuatilia na walikafuatilia wakatoa taarifa na moja ya sharti ni kwamba ni vizuri Halmashauri za Wilaya washirikishwe ili katika utekelezaji wa barabara hizi na uamzi wa barabara hizi usije ukawa wa kigeni mno. Kwa upande wa Mkoa wa Kagera barabara zilizopendekezwa na kuingizwa katika mpango huu ni zile za Wilaya zinazoungana na barabara za Mkoa. Hii ni kutokana na ukweli kwamba barabara zote za mkoa huo ziko katika hali nzuri ambao *European Union* waliweka sharti kwamba zile barabara za Mkoa. Lakini katika Kagera barabara zote za Mkoa ziko katika hali nzuri. Kwa hiyo, tukawashauri wakubali kutengeneza barabara za Wilaya zinazoungana na barabara za Mkoa. Kwa hiyo, hizi ndiyo barabara zilizokubaliwa na *Europen Union*. Wizara ya Ujenzi haina mamlaka zaidi ya hapo.

**SPIKA:** Kwa kuzingatia muda naona tuendelee na swali la Mheshimiwa Kabuzi.

Na. 46

***Kabuzi Road***

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati *Geita Gold Mine Limited* walipokuwa wakijenga mgodi wa Geita walipindisha barabara ya wananchi watokao Butundwe na Biharamulo na kusababisha ongezeko la umbali wa zaidi ya km. 22 kutoka km 5 za awali kwenda Geita na kwa kuwa, uongozi wa mgodi huo uliahidi kufungua barabara toka Nyamalembo/*Copkot* kupitia Magena hadi Samina na barabara ya Mpomvu ambayo inapita nje ya Mgodi:-

(a) Je, Kampuni hiyo inangoja nini kuitengeneza barabara hiyo ambayo wao waliita *Kabuzi Road* kwani wananchi wa Butundwe na Busanda wanaendelea kuteseka?

(b) Je, kuna haja gani ya kuwa na *Road Board* wakati barabara zinapindishwa na haiulizwi wala kuhusishwa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, Mbunge wa Busanda, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wakati shughuli za mgodi wa Geita zinaanzishwa, uongozi wa Mgodi ulitoa maombi ya kurekebisha sehemu ya barabara za Mkoa na za Wilaya zilizokuwa zinapita ndani ya eneo la mgodi ili zipite nje ya eneo hilo.

Kwa kutambua umuhimu wa mgodi wa Geita kwa Taifa, Wizara yangu kwa kushirikiana na uongozi wa Wilaya ya Geita ulikubali ombi hili na kuruhusu barabara ya Geita – Katoro, Geita – Nzera na Geita – *Port Nungwe* zifanyiwe marekebisho yaliyoombwa na uongozi wa mgodi kwa gharama ya mgodi wenyewe. Kazi hii ilifanyika na imekwisha kamilika tangu mwaka 2002.

Aidha, Wizara haina taarifa juu ya ahadi iliyofanywa na uongozi wa Mgodi wa Geita inayohusu ufunguzi wa barabara toka Nyamalembo/*Copkot* kupitia Magena hadi Saina na barabara ya Mpomvu na wala Wizara haina taarifa rasmi ya barabara inayoitwa *Kabuzi Raod. (Kicheko)*

(b) Mheshimiwa Spika, moja ya kazi kubwa ya Bodi ya Barabara ni kumshauri Waziri wa Ujenzi kuhusu masuala yanayohusiana na barabara za Mkoa na za Kitaifa. Kwa kuwa kazi ya ujenzi wa mgodi wa Geita lilikubalika kitaifa na kwa kuwa uongozi wa Wilaya ulihusishwa katika kupendekeza maeneo ambayo barabara zilizorekebishwa yatapita, hii ilitosha kuruhusu marekebisho haya ya hararaka yafanyike bila kusubiri kikao cha Bodi ya Barabara.

Aidha, umuhimu wa Bodi ya Barabara katika kazi yake ya kufuatilia miradi ya barabara na kumshauri Waziri wa Ujenzi pale inapobiudi, upo pale pale na Serikali inathamini na kuheshimu ushauri wa Bodi za Barabara na matokeo yake yanaonekana.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kuniruhusu niulize swali la nyongeza. Naamini Wizara imeshaelezwa matatizo wanayoyapata wananchi wa Busanda na Butundwe wanaokwenda Geita wanayoyapata kutokana na ongezeko la kilomita 22 badala ya kilomita 5 na suala hili tumeshalileta Bungeni mara kwa mara. Na kumekuwa na majadiliano ambayo wananchi na sisi Wabunge tumekutana na watu wa mgodi. Maombi ya Wabunge kufungua hiyo barabara na inaonekana yanapingwa na Wizara. Je, ina maana Wizara haina huruma na wananchi hawa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, tatizo hilo la wananchi kupita kilomita 22 badala ya kilomita 5 tunalifahamu, na limekuja na limezungumzwa sana na tumelirudisha sisi kama Wizara lianze kwenye Bodi ya Barabara rasmi kabisa ili kusiwe na matatizo ya maamuzi baadaye kwamba Bodi ya Barabara iamue sasa na tumewaomba waamue hiyo barabara kama wanaitaka kuifungua na waseme sasa ni njia ipi nyingine mbadala itatumika na mgodi, hawajatuletea jibu, wakituletea jibu tutawaelekeza mamlaka ya Mgodi watengeneze hiyo barabara nyingine ili wapate wao nafasi ya kutumia barabara iliyopo. Wizara ya Ujenzi inathamini sana wananchi na Mheshimiwa Mbunge analijua hili, na wananchi wenyewe wanalijua na ndiyo maana tunatengeneza barabara kwa bidii sana. *(Makofi)*

Na. 47

**Meli ya Abiria iliyozidisha Uzito ikitoka Dar es Salaam – Mtwara**

**MHE. MARGARETH J. BWANA** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni vyombo vya habari vimetangaza kuwepo kwa meli ya abiria iliyozidisha uzito ikiwa inatoka Dar es Salaam kwenda Mtwara kinyume na inavyotakiwa na kwa kuwa mamlaka husika ilitangaza kuzuiliwa safari yake lakini ikakaidi amri hiyo na kuamua kuendelea na safari:-

(a) Kama meli hiyo ilizidisha uzito, je, ilizidisha kwa kiasi gani?

(b) Kama Serikali iliizuia meli hiyo isiondoke hadi ipunguze uzito uliozidi, lakini meli hiyo ikaendelea na safari yake, je, ilipunguza uzito huo kama ilivyoamriwa?

(c) Je, Serikali imechukua hatua gani kwa waliohusika na kupuuza maagizo ya Serikali?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Margareth J. Bwana, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mnamo tarehe 15/12/2004 meli ya Shirika la Meli la Zanzibar ilikuwa ifanye safari yake kutoka Dar es Salaam kwenda Mtwara. Katika kujitayarisha kuondoka ilibainika kuwa na abiria wengi kuliko vifaa vya uokoaji. Idadi ya waliopanda meli ilikuwa 724 ikilinganishwa na idadi ya 535 ambayo ndiyo inakubalika kuwa wangeweza kupata vifaa vya kuokolea endapo vingehitajika kwa dharura. Hivyo basi, Msajili wa Meli aliizuia meli hiyo kwa sababu za kiusalama. Nahodha wa meli hiyo aliamua kuendelea na safari yake hapo tarehe 16/12/2004 bila kupata kibali cha Mamlaka ya Bandari. Hii ilipelekea Msajili wa Meli kumchukulia hatua Nahodha za kisheria kwa mujibu wa Sheria ya *Merchant Shipping Act, 2003.*

Mheshimiwa Spika, ni mategemeo yetu kwamba chombo tulichokiunda cha *SUMATRA* kitadhibiti taasisi husika kwa kufuatilia kwa makini na kuona kuwa wenye dhamana ya kazi zao wanatekeleza wajibu wao kwa uadilifu. Napenda nitoe wito kwa wamiliki wa vyombo vyote vya usafiri kujitahidi sana kufuata taratibu za uendeshaji zilizowekwa kisheria. Kupitia swali hili Mheshimiwa Margareth Bwana anatukumbusha wahusika wote umuhimu wa usalama katika usafiri wa majini na usafiri kwa ujumla. Kauli mbiu katika usafiri na uchukuzi kwa ujumla daima iwe usalama kwanza. Tumshukuru kwa hili na ufuatiliaji wake wa usafiri katika Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kutokana na matatizo yaliyotajwa katika swali la msingi. Je, Serikali sasa hivi inatoa matumaini gani kwa wananchi wa Mikoa ya Kusini kuhusu usafiri kati ya Dar es Salaam na Mtwara? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwa sasa kuna meli tatu ambazo hufanya safari zake kuanzia Dar es Salaam kwenda Mtwara na meli hizo ni *MV Safari* ambayo hufanya safari moja kwa wiki. Kuna *MV Mapinduzi* na *MV Maendeleo.* Hizi mbili, *MV Mapinduzi* na *MV Maendeleo* hazina ratiba maalum. Nakiri kwamba ni upungufu mkubwa kwa upande wa uchukuzi katika suala la usafiri wa meli kutoka Dar es Salaam kwenda Mtwara. Lakini kama unavyofahamu na Waheshimiwa Wabunge wanavyohamu suala la uchukuzi ni suala ambalo kwa kweli tunatafuta wawekezaji na wenye kampuni binafsi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba tushirikiane na Serikali, Waheshimiwa Wabunge, wafanya biashara wa maeneo ya Kusini, maeneo ya Mtwara na Lindi ili tuweze tukapata wawekezaji ambao watawekeza katika kununua meli za kwenda Mtwara na Lindi.

Na. 48

**Huduma ya Simu Songwa**

**MHE. PAUL N. MAKOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Maganzo uliopo Kata ya Songwa uliwekewa simu *(land line)* lakini baadaye huduma hiyo ya simu iliondolewa:-

(a) Je, ni sababu zipi zilizofanya huduma hiyo iondolewe?

(b) Je, Serikali haioni kuwa sasa ni muda muafaka kuweka simu katika mji huo ambao sasa unazidi kukua?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Paul Ng'wala Makolo, Mbunge wa Kishapu, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Huduma ya simu mjini Maganzo iliondolewa kutokana na wizi wa mara kwa mara wa nyaya za njia hiyo, wizi ambao husababisha gharama kubwa za matengenezo na ukarabati. Kwa sababu hiyo kampuni ya Simu Tanzania *TTCL* ililazimika kuiondoa njia hiyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukosekana kwa huduma za *TTCL* kwa sasa kampuni za simu za mkononi kama vile *Vodacom* zinatoa huduma katika mji wa Maganzo. Vile vile kampuni ya simu ya *Mobitel* imejenga mtambo wake wa simu maeneo ya Kishapu na mtambo huo unahudumia pia mji wa Maganzo. Aidha, Kampuni ya Simu ya *Celtel* nayo imekwishafikisha mawasiliano kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, tatizo la wizi wa nyaya za simu ni kubwa na ni la sehemu nyingi nchini. Wizi wa aina hiyo hakika ni kuhujumu uchumi na huduma za kijamii. Unarudisha nyuma maendeleo. Tushirikiane kukabiliana na tatizo hili. Tunamshukuru Mheshimiwa Makolo kwa ushirikiano mkubwa aliotupa katika kufuatilia tatizo la mawasiliano Kishapu na nchini kote kwa ujumla.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa Wilayani Ngara, kampuni za *Celtel* na *Vodacom* wameshindwa kufikisha huduma zao katika Kata za Mrusagamba, Muganza, Rugarama na Rukiro ambako ni mpakani mwa nchi ya Burundi ambako vita inazidi kushamiri. Na kwa kuwa ujambazi, wizi na hata mauaji umekuwa ni wimbo wa kila siku. Je, Serikali inasemaje kuhusu kuwalinda wananchi wa sehemu hiyo na mali zao ambao sasa wamekuwa kama wakimbizi katika nchi yao?

**SPIKA:** Ni swali jipya, lakini kama Waziri una majibu, hana. Lilete kwa njia ya kawaida. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 49

**Huduma ya Maji – Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani**

**MHE. AISHA P. MAGINA** aliuliza:-

Je, tangu Kampuni ya *City Water Limited* ianze kazi ya kutoa huduma ya maji katika Mkoa wa Pwani na Jijini Dar es Salaam imepata mafanikio gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Magina, kama ifuatavyo: Kampuni binafsi ya *City Water Services Limited* iliingia mkataba wa miaka 10 na *DAWASA* wa ukodishaji wa miundombinu na kuanza kuendesha shughuli za utoaji huduma ya majisafi na majitaka katika Jiji la Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Pwani mnamo mwezi Februari 2003, wakati huo mikataba ya ununuzi wa vifaa na ukarabati wa dharura wa mitambo ilisainiwa. Aidha, Kampuni hiyo ilikasimiwa kusimamia kazi ya ulazaji wa kilomita 1,000 za mabomba ya usambazaji maji kwa wateja. Lengo la mikataba hiyo ilikuwa ni kuiwezesha kampuni hiyo kuinua kiwango cha utoaji huduma ya maji wakati wa maandalizi na utekelezaji wa mradi wa uboreshaji wa miundombinu ya majisafi na majitaka Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, tangu kipindi hicho jumla ya dira za maji 100,486 zimenunuliwa na dira hizo zipatazo 10,003 zimefungwa kwa wateja mbalimbali. Aidha, jumla ya pampu 9 za kusukuma maji pampu 6 za Ruvu Juu na pampu 3 za Ruvu Chini zimekabarabatiwa. Kwa sasa pampu nyingine 3 pampu moja ya Ruvu Chini na pampu mbili za Ruvu Juu zipo Afrika Kusini zikifanyiwa ukarabati.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukamilika kwa kazi hizo, mapungufu kadhaa ya kiutendaji yalijitokeza kwa upande wa *City Water Services Limited*. Mapungufu hayo ni pamoja na kushindwa kuwekeza kiasi cha dola milioni 8.5 kilichopo kwenye mkataba, kushindwa kulipa pango kwa *DAWASA* kiasi cha dola milioni 3.6, kushindwa kutoa huduma ya kuridhisha kwa wateja pamoja na kushindwa kukusanya maduhuli ya kutosha ili kuboresha mradi.

Kutokana na mapungufu hayo, Serikali ililazimika kusitisha mkataba na *City Water Services Limited* tarehe 20/5/2005. Jukumu la utoaji wa huduma ya maji jijini Dar es Salaam na maeneo ya Mkoa wa Pwani sasa yamekabidhiwa kampuni ya *Dar es Salaam Water Supply and Sewerage Corporation (DAWASCO).* Kampuni hii mpya ilianzishwa tarehe 1/5/2005 chini ya Sheria ya *Public Corporation Act, No. 1* ya mwaka 1992. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba viongozi wa *City Water Services* waliondoka nchini tarehe 31/05/2005 na uongozi wa *DAWASCO* ulianza kazi rasmi tarehe 1 Juni, 2005.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, Benki ya Afrika *(ADB)* na Benki ya Uwekezaji ya Nchi za Ulaya *(EIB)* inatekeleza mradi mkubwa wa ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya majisafi na majitaka ambao pia unalenga kuboresha huduma ya majisafi na majitaka. Mradi huu unatekelezwa na *DAWASA* kwa niaba ya Serikali kuanzia tarehe 1 Agosti, 2003.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Nashukuru Mheshimiwa Spika kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nilikuwa nataka kuuliza kwamba kwa kuwa hawa *City Water* walivunja mkataba na kwa kuwa tuna *experience* kwamba *IPTL* walipovunja mkataba walitushtaki na sasa tunawalipa zaidi ya 3.5 billioni kwa kutushitaki. Ni kwa

nini tumewafukuza tu bila kuwashitaki ili na wao watulipe sisi kwa kuvunja huu mkataba?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, sisi Serikali tulichojali sana ni masharti ya mkataba na masharti ya mkataba yanasema ukivunja kipengele hiki ina maana mkataba unaustisha. Kwa hiyo, vipengele vyote nilivyovisema kutokuweka fedha kwenye huu mradi iliharibu *liquidity ration* kiasi kwamba kampuni isingeendelea. Kwa hiyo, tulichofuata ni yale masharti na *strictilly* tumefuata kibiashara siyo kwa masharti mengine ya kuanza kushitakiana kwa sababu masharti ya mkataba unasema ukivunja sharti moja, mbili, tatu, mkataba unastishwa. Ndiyo tulichofuata. Sasa kama ni kushtaki ni kawaida wana uhuru wa kushtaki na nina hakika kwamba tutafuata Mahakama na wahusika wote watafuata mkataba ulikuwa unasema nini.

Na. 50

**Kuchanja Mifugo**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA** aliuliza:-

Kwa kuwa ni sera ya Serikali kuchanja mifugo kunapotokea dalili ya magonjwa ya mlipuko na katika wilaya ya Sumbawanga Vijijini hususani Kata zote za mpakani na nchi ya Zambia hasa katika Jimbo la Kalambo, ng'ombe wengi wamekufa kutokana na kufanyiwa chanjo kimakosa:-

(a) Je, Serikali ina tamko gani kuhusu jambo hilo?

(b) Je, wananchi hao watafidiwa namna gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Niliwahi kujibu swali na hoja za Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na fidia zinazopaswa kulipwa kwa mfugaji endapo atapoteza mifugo yake kutokana na huduma duni kutoka kwa wataalamu wetu. Hata hivyo tulipitisha hapa Bungeni Sheria ya Afya ya Mifugo Na. 17 ya 2003 inayosimamia jambo hili ili haki itendeke kwa wahusika wote yaani mfugaji kwa upande mmoja na Serikali kama msimamizi wa huduma kwa upande mwingine.

Utaratibu wa chanjo dhidi ya ugonjwa wa homa ya mapafu, inaonyesha kuwa ni asilimia 1-3 ya ng'ombe wanaochanjwa katika kampeni inayoendelea nchini wanaweza kupata athari ya kuvimba mwili na wachache chini asilimia 0.3 wanaweza kufa. Viwango hivi vya athari ni kidogo ikilinganishwa na vifo vinavyoweza kufikia hadi asilimia hamsini kama chanjo haitafanyika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tukio analolizungumzia Mheshimiwa Mbunge lilitokea huko Sumbawanga wataalam wetu kutoka Kituo cha Uchunguzi wa Magonjwa ya Mifugo Kanda ya Nyanda za Juu Kusini walikwenda katika Tarafa ya Mwimbi na Laila, ili kufanya uchunguzi na kutafuta kiini cha tatizo hilo. Taarifa zinayonyesha kuwa jumla ya ng'ombe 10,475 walichanjwa na kati ya hao 183 walivimba ikiwa ni sawa na asilimia 1.7 na ng'ombe 18 waliopotiwa kufa ikiwa ni sawa na asilimia 0.17. Kwa bahati mbaya mizoga ya ng'ombe hao haikupatikana ili kuhakiki chanzo cha vifo vyao.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashauri wafugaji kwamba endapo wataona uvimbe umejitokeza au magonjwa mengine ya mifugo mara zote wanashauri watoe taarifa haraka kwa wataalam wa mifugo aliye karibu nao ili wapatiwawe huduma ya kitaalam na kuelekezwa namna ya kuihudumia mifugo iliyoathirika. Pale vifo vinapotekea baada ya chanjo wafugaji washauriane na wataalam kuthibitisha kwamba ni kweli vifo hivyo vimetokana na chanjo. Ikiwa itathibitika kama kwamba mnyama amekufa kwa ugonjwa unatokana na chanjo Serikali itaweza kufidia kulingana na Sheria ya mifugo ya mwaka 2003. Kwa bahati mbaya haikuweza kuthibitishwa hivyo kule Sumbawanga Vijijini lilikotokea tatizo hilo ambalo Mheshimiwa Mbunge amelieleza.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kukubali kwamba mizoga haikuonekana kwa sababu wataalam wako walikimbia baada ya kuona mifugo mingi imekufa, na mzee mmoja amepoteza zaidi ya ng'ombe 17 ambao ng'ombe hao kama unavyojua wilaya yetu, tunafuga ng'ombe kwa adabu hatufugi ng'ombe hovyo hovyo na kwa wingi sana.

Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri anasema mizoga haikuonekana, na mimi namwambia waliokufa sio asilimia hiyo walioyokufa. Unachukua hatua gani ili uweze kupata uhakika wa ng'ombe wote waliokufa kutokana na chanjo hii, na kutoa fidia?

Swali la pili, wananchi katika Jimbo la Kalambo hivi sasa wanasema Serikali imeondoa kodi ya mifugo na imekuja kuchanja ng'ombe ili wafe kwa sababu wanaona hawana manufaa nayo. Je, hii ndio mpango wa Serikali, kuwauwa ng'ombe wa wananchi kwa sababu hawalipi tena ushuru wa mifugo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO**: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwananzila, anasema wataalam walikimbia, lakini ni wataalam hao hao waligundua kwamba mizoga haikuonekana, na kukimbia walikimbia anasema kwa kutishika ng'ombe 17 wamekufa kati ya ng'ombe 10,450 waliochanjwa sasa kidogo inaniwia vigumu, na kukimbia kwao tungepata taarifa kutoka kwenye uongozi wa maeneo yale kwamba kweli wataalam walikuja na wamekimbia. Lakini taarifa tuliyoipata ni kwamba waliuliza mizoga iko wapi kwa bahati mbaya hawakuelezwa mizoga iko wapi. Kwa hiyo, kuna uwezo mizoga ile wanajua waliko iweka au inawezekana ni kweli ng'ombe 17 wale walikufa au ikawa ng'ombe wachache zaidi.

Suala la pili anaeleza kwa kweli nashindwa kuelewa kwa nini Serikali ilaumiwe kwa kupeleka chanjo na *disinformation* yaani wapeleke taarifa za uwongo kwamba nia ya Serikali ni kuwauwa wale ng'ombe. Sidhani kama kweli hiyo ina mantiki kwa sababu wakati wote Serikali imekuwa mbele kutetea mali na wananchi wake, na ndio kazi moja ambayo imepewa kikatiba. Sasa hilo kama linatokea, tuko tayari kuja kulielezea kwa wananchi kwamba kwa kuchanja mifugo unawaponyesha kutokana na matatizo ambayo yaweza kujitokea. Lakini kwa kuwaacha nina hakika kwamba wangekufa wengi kama wataalam wanavyotueleza ukiacha kuwa chanja kama una ng'ombe 100 kuna *possibility* kubwa kwamba ng'ombe hamsini wanaweza kufa badala ya ng'ombe asilimia ambayo tumeisema ya asilimia kama tatu ambayo ni idadi dogo zaidi ikilinganishwa na kama usingechanja.

**SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha. Kuna tangazo la kikao cha Kamati moja nayo ni Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mwenyekiti, wake Mheshimiwa Dr. John Malecela anawatangazia wajumbe wake kwamba leo tarehe 13 mara baada ya kipindi cha maswali na majibu, kikao cha Kamati hiyo kitafanyika gorofa ya kwanza chumba Na. 133, Kamati ya Ulinzi na Usalama. Mwisho wa matangazo.

## HOJA ZA SERIKALI

### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2004, Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2005/2006 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2005/2006.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. WILLIAM J. KUSILLA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja zote mbili zilizo mbele ya Bunge lako Tukufu, Hoja ya Waziri wa Fedha na Hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kufanya hivyo na mimi ningeomba niungane na wenzangu waliotangulia kuchangia hoja hizi mbili ili kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bahi nitoe pole nyingi sana kwa Ndugu wa familia na wananchi wote wa Jimbo la Kilombero kwa ajili ya kifo cha aliyekuwa Mbunge wao, Mheshimiwa Abu Kiwanga, tunaungana na wenzetu wote kumwomba Mwenyezi Mungu ili aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia hoja hizi mbili, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Benjamin Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali yake yote ya awamu ya tatu kwa hii misamaha ambayo tumeipata *latest* kama ilivyotangazwa kwenye vyombo vya habari leo asubuhi ya kuiwezesha nchi yetu kupata misamaha ya madeni yote tuliyokuwa tunadaiwa na *IMF* na Benki ya Dunia. Kwa hakika hizi ni cheche za mwisho za Mheshimiwa Mkapa na Serikali yake ambazo zinaashiria kwamba Chama cha Mapinduzi kwa hakika kitapata

ushindi, ushindi wa kimbunga cha Sunami katika Uchaguzi Mkuu ujao. Nawapongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile niwapongeze sana Mawaziri wote wawili, Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji, kwa hoja mbili ambazo wameziwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu, zenye maelezo ya kina na yakuridhisha sana na ya kutia moyo kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii. Ila ninayo haya machache ya kuchangia katika hoja hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, kwanza hii ni bajeti ya kutekeleza mkakati wa kukuza uchumi na kuondoa umaskini nchini, ambao lengo lake kama mkakati wenyewe unavyosema ni kukuza uchumi na vile vile kuongeza kipato cha mifukoni cha wananchi, pamoja na kuboresha hali ya maisha ya wananchi na unazingatia suala la utawala bora. Sasa wananchi wako wilayani na wilaya ndizo zimepewa jukumu la msingi kabisa la kusimamia uchumi wa nchi katika maeneo yao pamoja na kuhakikisha maendeleo ya wananchi. Kwa hiyo, tofauti na bajeti zilizopita, katika bajeti hii ambayo ni bajeti ya MKUKUTA ningelitegemea kuwe na tofauti katika sura ya bajeti hii. Bajeti zote za nyuma, fedha nyingi sana zinabaki Wizarani na fedha kidogo zinapelekwa kwenye wilaya ambako ndiko maendeleo yanakotokea. Kwa hiyo, ningetegemea mwaka huu sura ya bajeti hii iwe tofauti kwa maana kwamba fedha nyingi zipelekwe wilayani, na kiasi kidogo kibaki katika Wizara na Mikoani kwa ajili ya kuratibu shughuli mbalimbali zinazoendelea katika Wilaya. Kwa maneno mengine badala ya bajeti hii kuendelea kuwa na sura ya kuwa *top heavy* iwe sasa na sura tofauti ya kuwa *bottom heavy*, kwa misingi hiyo kwamba fedha nyingi ziko wilayani badala ya kuwa katika Wizara na Mikoa. Lakini sasa nilipokuwa naipitia bajeti hii naona ina sura ile ile fedha kidogo sana zimepelekwa Wilayani, na fedha zilizo nyingi zimeendelea kubaki katika Wizara mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti hii ni bilioni 51 na milioni 588 na laki tisa na tano elfu na mia saba tu kati ya shilingi zilizotengwa kwa ajili ya mipango mbalimbali ya maendeleo ambayo jumla yake ni *trillion* moja bilioni mia tatu themanini na tano, milioni mia moja themanini na tatu laki moja na kumi na mbili elfu na mia nne, ndizo zimeelekezwa katika Mikoa na Wilaya zake, na kwa mahesabu yangu kiasi hiki ni chini ya asilimia nne ya fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo.

Sasa kwa mgao kama huu ninashindwa kuelewa namna ambavyo wilaya zinaweza zikasimamia mipango mbalimbali ambayo lengo lake ni kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa wananchi. Mimi ningelitegemea na ningelipendekeza, kwamba fedha zote ambazo katika bajeti zimetengwa kwa ajili ya maeneo mbalimbali ambayo lengo lake ni kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa wananchi, zote zipelekwe katika wilaya. Kwa mfano nashindwa kuelewa kwa nini fedha ambazo zimetengwa katika bajeti hii kwa ajili ya mikopo kwa wafanyabiashara ndogo ndogo katika Ofisi ya Makamu wa Rais ambayo kiasi chake ni bilioni tatu milioni mia tano na themanini zibaki katika Ofisi ya Makamu wa Rais badala ya kupelekwa wilayani. Sasa kama zinabaki katika Ofisi ya Rais, maana yake ni kwamba wananchi mbalimbali ambao watakuwa wanahitaji mikopo hii kwa ajili ya biashara ndogo ndogo, itabidi maombi yao yaanzie wilayani lakini yakaishie katika Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake kama ninavyoweza kutegemea itakuwa ni urasimu na ucheleweshaji mkubwa. Kwa hiyo, katika utekelezaji wa mkakati huu tunaweza tusifikie malengo yetu. Ninashindwa kuelewa kwa nini fedha za mradi wa *TASAF* zibaki katika Ofisi ya Makamu wa Rais wakati shughuli zenyewe zinafanyikia Wilayani. Katika bajeti hii zimetengwa bilioni 10 kwa madhumini haya lakini mradi mzima wa *TASAF* katika awamu ya pili unakusudiwa kupewa jumla ya bilioni 180. Sasa mimi ningelitegemea fedha hizi zipelekwe wilayani ili kuondoa urasimu na ucheleweshaji usio wa lazima kwa shughuli mbalimbali za *TASAF*.

Naomba niseme, kutokana na urasimu huu ambao umekuwepo tangu miradi ya *TASAF* imeaanza, kuna wananchi wengi katika Jimbo langu la Bahi, ambao walishiriki miradi mbalimbali ya *TASAF* ya awamu ya kwanza mpaka sasa hivi bado wanadai fedha hawajalipwa fedha walizotakiwa kulipwa kwa ajili tu ya urasimu huu mpaka awamu ya kwanza ikaisha, na awamu ya pili ikaanza. Wananchi wangu wa vijiji vya Chaligongo, Chalisanga, Chalimakulu, Chipanga, Chikopelo, Zejele, Mpalanga, Nkhome bado wanasubiri malipo yao mpaka sasa. Lakini najua halikuwa tatizo la fedha lakini lilikuwa ni tatizo la urasimu, sasa kama hali hii haibadilishwi, bado fedha zote zitaendelea kuwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais badala ya kupelekwa Wilayani moja kwa moja, matatizo haya yataendelea na kwa hakika yataathiri utekelezaji wa programu nzima.

Mheshimiwa Spika, mimi ningelipendekeza kwamba kwa madhumuni na manufaa ya mkakati huu, basi fedha zote ambazo zimetengwa kwa ajili ya maeneo mbalimbali ambayo madhumuni yake ni utekelezaji wa mkakati huo ambao ni mzuri ni wa manufaa sana kwa Taifa letu basi zipelekwe moja kwa moja wilayani. Kwa mfano hizi fedha, fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya mikopo midogo midogo hii hizi bilioni tatu na milioni mia tano themanini, kwa nini zisigawanye na kupelekwa moja kwa moja kwa wakurugenzi watendaji wa wilaya, Halmashauri na Manispaa ili wakashughulikie suala la mikopo midogo midogo huko huko badala ya fedha hizi kubaki katika Wizara zinazohusika.

Mheshimiwa Spika,ljingine ambalo nilitaka nilisemee katika muda huu mfupi ambao umebaki ni kusisitiza tu nina hakika na wengine wanaweza kuwa wamelizungumzia hili suala la umeme vijijini. Kwa kweli kama suala hili hatutalipa umuhimu linavyostahili na kuongeza kasi ya usambazaji wa umeme vijijini, basi maendeleo tutayokusudia kwa wananchi vijijini yataendelea kuwa ni ya kusuasua sana. kama umeme utafika katika vijiji vingi utakuwa ni kuvutio kwa wawekezaji mbalimbali, kwenda kuwekeza kwa mfano katika viwanda vya kusindika mazao mbalimbali ya kilimo, kuwekeza katika mashine mbalimbali za kukoboa na kusaga nafaka, na utaongeza hata ajira vijijini na kuboresha mazingira ya biashara katika vijiji na hiyo ndio itakuwa kuboresha hali ya wananchi wetu vijijini.

Kama suala hili likiendelea kwa kasi ambayo linakwenda sasa litatuchelewesha sana, ninayo *line* ya umeme kutoka hapa mpaka kwenye *studio* za *Radio Tanzania* Kanda ya Kati katika kijiji changu cha Mndemu, tumekuwa na *line* hii kwa miaka zaidi ya kumi na tano, lakini tumeshindwa kuendeleza umeme huo hata katika vijiji vya jirani na *Radio*

*Tanzania* Kanda ya Kati. Vijiji vya Kisima cha Ndeje, Msisi, Mchito, Zanka na kadhalika.

Sasa kama tukienda na kasi hii kwa kweli maendeleo vijijini itakuwa ni matatizo makubwa. Kwa hiyo napendekeza Serikali iangalie kama njia nyingine ya kongeza kasi ya kueneza umeme vijijini, iangalie uwezekano wa kuondoa kodi katika *Generator* za *diesel* na za *petrol* na vifaa vya umeme wa kutumia nguvu ya jua ili kuwawezesha wananchi wengi kujinunulia vifaa hivi kwa ajili ya matumizi majumbani kwao na hata kwa shughuli nyingine ndogo ndogo. (*Makofi*)

Hali ilivyo sasa hivi vifaa ni ghali sana kwa sababu ya kodi mbalimbali ambazo inatozwa, na kwa hiyo bei zake zinakuwa ni bei ambazo wananchi wengi hawawezi kuzimudu. Lakini kama kweli kwa mkakati huu tunataka kuwasaidia wananchi vijijini, basi napendekeza Serikali itazame suala hili iondoe kodi na hata ikiwezekana hata kuweka ruzuku katika baadhi ya vifaa hivi, ili tu kuwawezesha wananchi wengi kuvinunua na waweze kuvitumia kwa ajili ya maendeleo yao.

Nisingependa kengele ya pili inigongee nikiwa nimesimama. Kwa hiyo, naomba kwa hayo machache niishie hapa kwa kuunga mkono hoja zote mbili zilizo mbele ya Bunge lako Tukufu, naunga mkono.

**MHE. ATHUMAN S.M. JANGUO**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipatia nafasi ya kuchangia hotuba hizi mbili za mipango na bajeti, na kwa kuwa nilikwisha toa rambirambi zangu kwa niaba ya wananchi wa Kisarawe na Kamati, nakuwapongeza wote ambao wameteuliwa na Chama cha Mapinduzi, kwa ajili ya kuwania nafasi za urais sina haja tena ya kurudia rambirambi hizo na salam hizo.

Mheshimiwa Spika, ningeanza kwa kuwapongeza Mawaziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango, na wasaidizi wao kwa kazi nzuri wanayofanya na kwa hotuba nzuri ambazo wametuletea, ambazo zinatoa matumaini makubwa sana kwa Watanzania. Pia nawapongeza kuwa hotuba hizi zinathibitisha kwamba wanatekeleza sera za Chama cha Mapinduzi kwa nadharia na kwa vitendo. Tukiangalia mtiririko wa Bajeti ya matumizi ya kawaida kuanzia mwaka 2003 mpaka 2004 na hadi Bajeti hii ya 2005/2006 tunayoijadili sasa, tutaona mambo yafuatayo katika bajeti hizi yanajitokeza.

Mheshimiwa Spika, la kwanza katika Bajeti hii ni Bajeti katika maeneo yafuatayo imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka; eneo la ulipaji wa madeni ya nje na ndani, kama inavyoonyesha kwamba kwenye mwaka 2003/2004, Bajeti ilikuwa milioni 308 lakini sasa hivi tunazungumzia Bajeti ya bilioni 523. Hii inaonekena kwamba Serikali inaweka uzito katika majukumu yake na kama alivyowahi kusema Mheshimiwa Rais hapa wiki iliyopita, hatua hii imeiletea nchi yetu sifa na kuweza kupunguziwa madeni na mengine yametangazwa hata asubuhi hii kwamba sasa tunazidi kupunguziwa kwa sababu tumeonekana Watanzania wastarabu.

Pili Afya, imepanda kutoka shilingi bilioni 85 mwaka 2003 hadi bilioni 180 mwaka huu, maana yake ni kuwa kwa kweli matatizo ya wananchi yanazingatiwa kilimo

vile vile kimepanda kutoka milioni 40 ingawa kilishuka bilioni 34 kwenye Bajeti ya mwaka 2004/2005 lakini imepanda kufikia bilioni 55. Ukitazama kwa haraka haraka unaweza kusema kwamba, kilimo hakikupewa uzito, lakini ukiangalia kwamba sekta nyingine zote ndani yake kuna *element* ya kilimo, kwa hiyo ukikusanya Bajeti yote utaona kwamba Serikali inaweka uzito katika sekta hii ya kilimo.

Kwa hapa tunajifunza kama nilivyosema kwamba kuna msimamo dhabiti wa kupunguza madeni na pia vile vile hii imesaidia kuwapa uwezo wale wa ndani waliokuwa wakiidai Serikali hususani Makandarasi wa majengo na kadhalika kuwa na uwezo sasa wa kutekeleza na kuwekeza katika sekta mbali mbali nchini. Pamoja na mabadiliko ya sera kutoka Mkakati wa Kupunguza Umaskini (*PRS*) na kwenda kwenye MKUKUTA, lakini Bajeti hii inaonyesha kwamba yale maeneo nyeti bado yamezingatiwa. Kwamba MKUKUTA unalenga kuboresha sekata zote bila kujaLI sekta moja, lakini kwamba zile sekta nyeti ambazo ndizo zenye kero za wananchi kwa maana ya miundo mbinu, barabara vijijini, maji afya na kadharika vimepewa uzito. Kwa hiyo inaoneka wazi kabisa kwamba mgao wa Bajeti ya maendeleo. Kwa mfano; kati ya shilingi trillioni 1,333. 6 zilizopangwa kwa Wizara zote, bilioni 712.3 zimeelekezwa katika sekta nyeti. Mimi nadhani Serikali inastahili pongezo kwa kuangalia hizi sekta nyeti. (*Makofi*).

Mheshimiwa Spika tukiangalia mtiririko wa Bajeti ya Mikoa katika kipindi cha miaka 2003/2004 hadi Bajeti hii tuyoizungumzia, tutaona kuwa yapo mambo ambayo Serikali inastahili kupongezwa na yapo mengine tuwaulize. Ambayo ya kupomgezwa kwa haraka haraka ni kwamba kwenye Bajeti ya kawaida, mgao kwa Wizara zote umeongezeka kutoka trilioni 1, bilioni 477 hadi kufikia trilioni 2, bilioni 269, sawa na ongezeko la asilimia 54. Pamoja na kwamba walionitangulia wamehawi kutamka kwamba uzito haukuwekwa vijijini, lakini tuangalie na uwezo wa utekelezaji. Kabla hatujajenga uwezo kule kwenye Mikoa na Wilaya, si jambo zuri kuepeleka pesa halafu usimamizi ukawa mbaya.

Nyongeza amabayo imeonyeshwa katika Bajeti zetu katika Mikoa kutoka bilioni 263 hadi billioni 524 ambalo ni ongezeko la asilimia 200, kwa kweli linahitaji kusifiwa inaonyesha kwamba Serikali inapeleka uzito huko ambako ndiko ziliko kero. Katika Bajeti ya matumizi ya kawaida, Mikoani kulikuwa na tofauti kubwa sana baina ya Mkoa na Mkoa hizo siku za nyuma. Nikitoa mfano, kwenye Bajeti ya 2003/2004, mgao mkubwa ulikwenda Dar es Salaam ambapo walipewa shilingi bilioni 23.95 wakati Mkoa uliopewa kiwango cha chini kabisa ulikuwa Mkoa wa Pwani jirani yake ambao ulipata milioni 590. Unazungumzia bilioni 23 ukilinganisha na milino 500, Wamarekani wanasema ni "*peanut*." Hii ilikuwa tofauti kubwa sana, hali hiyo iliendelea hadi Bajeti ya mwaka 2004/2005, ambapo Mkoa wa Mbeya ndiyo ulipata kiwango cha juu, ulipata bilioni 30.158 wakati Mkoa wa mwisho ukaendelea kuwa Mkoa wa Pwani ambao umepewe milioni 590 kiwango ambacho ni karibu sawa sawa na kile cha mwaka 2003. Lakini kwenye Bajeti hii naona kidogo kuna tofauti inayoonyesha angalau kwamba, Mikoa haikupishana sana. kwa mfano, chini ya Bajeti hii, Mkoa ambao umepewa kiwango cha chini kabisa, bilioni 14 ni Mkoa wa Lindi, wakati Mwanza ambayo imepata kiwango cha juu imepata bilioni 39.9. Angalau sasa nasema kwamba hilo pengo huwezi

ukalilinganisha na zile milioni 590 ukilinganisha na bilioni 30 ambazo ilikuwa imepata Dar es Salaam.

Kwa hiyo, ningependa kuipongeza Serikali kwa kuangalia kwamba sasa hivi tofauti baina ya Mikoa wanaona kwamba kuna haja ya kuondoa zile tofauti kubwa, lakini vile vile inapungua. Naona kama Bajeti hii imelenga kuinua kidogo ile Mikoa ambayo siku za nyuma ilikuwa imebaki nyuma sana. Lakini jambo la kuuliza hapa ni moja.

Je, hivi kwa nini Mikoa fulani kila wakati inakuwa ndiyo ya nyuma tu katika kupangiwa Bajeti? Mawaziri watakapo jibu ningeomba wanijibu hili. Hebu tuangalie migao kwa miaka hii niliyo itaja ya Mkoa wa Pwani, Mara, Kagera na Lindi, utaona kwamba kila wakati Mikoa hii inapewa kidogo. Sababu ni nini? (*Makofi*)

Labda niseme kuwa katika hili Serikali pengine vile vile ingestahili hiyo pongezi ya viwango kuwa havipishani sana lakini bado katika Bajeti ya mwaka huu, Mkoa wa chini kabisa umepewa milioni 400 na wa juu kabisa umepewa milioni 700, kwa hiyo nasema kwamba angalau tofaui yake ni ndogo lakini bado iko pale pale. Kuna Mikoa ambayo inapewa migao kidogo zaidi kulikoni mingine. Kwa haraka haraka sasa niruhusu niipongeze Serikali na kwa kweli tujipongeze wote pamoja na Bunge kwa mafanikio ambayo yanaonekana katika Bajeti hizi.

(1) Kuwezesha uchumi uongezeke kwa wastani wa 6.7 mwaka huu wakati tumetoka katika miaka ya nyuma uchumi ukiongezeka kwa aslimia 1.9.

(2) Kushuka kwa mfumuko wa bei kutoka asilimia 27.4 kwenye Bajeti ya 95 hadi kufikia asilimia nne mwaka huu.

(3) Kuongeza ukusanyaji wa mapato kama tulivyoambiwa katika hizi Bajeti, ambayo miaka ya nyuma ilikuwa kwenye kiasi cha bilioni 25 kwa mwezi, sasa hivi ni zaidi ya bilioni 125.

(4) Serikali kuweza kudhibiti matumizi yake yenyewe chini ya Bajeti, ingawa nimesoma katika magazeti, kiongozi mmoja wa upinzani analaumu kwa hili, lakini mimi nafikiri tuipongeze Serikali kwa kuwa imeona umuhimu wa kupunguza matumizi.

(5) Kuongeza mauzo ya bidhaa zetu kwa nje, lakini hapa Bajeti zinasema kwamba zimeongezeka kidogo tu tukilinganisha na matarajio. Kwa hiyo, mimi ninaamini kwamba kama tutatekeleza vizuri mipango yetu tufanye kazi kwa bidii, Watanzania wote tujihusishe kikamilifu kabisa na Mkakati wa *NEPAD* na tupime shughuli zetu kwa kutumia *PRM,* ninaamini kwamba lengo letu la asilimia 10 katika miaka mitano ijayo tunaweza tukafikia bila matatizo.

Mheshimiwa Spika, tunaambiwa kuwa Benki ya Dunia imetoa dola milioni 500 kwa ajili ya shughuli za maendeleo na imetenga dola milioni 570 kwa ajili ya kuwekeza katika miradi ya maendeleo na pia vilevile Benki ya Afrika imetenga milioni 580 kwa ajili hiyo hiyo.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuwa Watanzania tuchangamke sana katika kuhakikisha kwamba fedha hizi zinaingia Tanzania kwa kutayarisha miradi ambayo inaweza ikaitumia. Mimi ninaamini kwa matatizo tuliyokuwa nayo, hasa kule vijijini ya ukosefu wa maji, barabara mbovu, umeme hakuna, ambayo kwa kweli *NEPAD* inaweza ikasaidia sana katika miradi kama hii itabidi tujaribu kuandaa miradi ili ikubalike na tuweze kuzitumia fedha hizo. Nikitoa mfano wa Jimbo langu kule Kisarawe sasa hivi, hata hizi simu za mkononi ni pale Wilayani tu, lakini ukienda kwenye vijiji hakuna kwa sababu hakuna umeme. Sasa kama tunaweza tukaandaa miradi hii, hii ya umeme vijijini halafu tukafikisha kule na tukaweza kuzitumia fedha hizi ninaamini kwamba tutafika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto zilizotajwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha ambazo muhimu ni tatu, mimi ninayo maoni yafuatayo: Lengo la ukuaji wa uchumi la asilimia 10. Kwa kuwa Watanzania wanaongezeka kwa wastani wa asilimia 3 kila mwaka, hapana budi tujitahidi kadri iwezekanavyo ili kusudi lengo hili la ukuaji wa uchumi kwa asilimia 10 tulifikie au zaidi, vinginevyo tunaweza tukawa kwenye matatizo kama alivyosema mtoa mada. Lakini nina matumaini, tulikotoka kama nilivyosema uchumi ulikuwa unakua kwa kiwango cha chini cha asilimia 1.9. Sasa hivi, kama tumefika kwenye asilimia 6.7, hizo zilizobaki asilimia 3.3 mimi ninaamini kabisa kwa yale niliyoyasema kama tutayatekeleza tutafikia lengo hili.

Pili, kuhusu Bajeti yetu kuendelea kuwa tegemezi, mimi sitishiki sana, tena nimeona kwenye vyombo vya habari kiongozi mmoja wa Upinzani analaumu hili. Lakini tuangalie tulikotoka tulikuwa tegemezi zaidi kulikoni hivi ilivyo sasa. Hata Bajeti iliyopita ile tulikuwa tegemezi kwa asilimia 45, sasa tuko tegemezi kwa asilimia 40 tunasonga mbele.

Kuhusu fedha za kigeni kutokana na misaada, ni kweli tunahitajika kuweka nguvu zaidi hasa katika kuuza biashara zetu za nje. Lakini mimi nasema tusiishie hapo, sisi pamoja na Waafrika wenzetu wengine na nchi zote zilizokuwa maskini tuzishinikize nchi tajiri ziache kutupangia bei katika mazao yetu ya kilimo na ziache ukiritimba wa kusema kwamba wao tu ndio pekee ambao wanaweza kutuamulia. Tukiweza kuzishinikiza hivi ninaamini kabisa kwamba tutavuka.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kuipongeza Serikali kwa kuzingatia mambo nyeti kwenye mgao wa fedha wa Bajeti hii. Mengi yameorodheshwa katika Ibara ya 18 ya hoja ya Mheshimiwa Basil Mramba, lakini napenda niipongeze Serikali kwa haya machache yafuatayo:-

(1) Kutenga asilimia 4.5 ya msaada kwa Serikali ya Zanzibar. Hatua hii itaimarisha Muungano wetu.

(2) Kutenga fedha za malipo ya mafao ya waliokuwa watumishi wa Afrika Mashariki, mimi nafikiri hii itaondoa kero zile za maandamano ambayo yameonekana. Lakini hapa kuna moja wameambiwa watapewa asilimia 10 je, zile nyingine lini? Na sasa hivi wengi wanaotuuliza wakachukulie wapi hizo pesa, nani atakuwa anawapa? Mashirika yao, Hazina au nani? Nafikiri wakifafanuliwa hili watakuwa wameelewa vizuri.

(3) Kutenga fedha kwa ajili ya mishahara ya watendaji vijijini vikiwemo viporo. Sisi wote tunajua kuwa hawa ndio waliomstari wa mbele katika kutekeleza jukumu la kukuza uchumi wa nchi hii. Kwa hiyo, kuwatengea mishahara hawa nafikiri itazidi kuongeza hari na mapato yetu yatazidi kwenda juu.

(4) Kutenga asilimia 18 ya mapato yetu kwa ajili ya Bajeti ya maendeleo, huu ni mfano mzuri sana. Miaka ya nyuma Bajeti ya Maendeleo ilikuwa inagharimiwa tu na misaada kutoka nje. Lakini kwa mara ya kwanza tumeweza kuwa na Bajeti ambayo angalau inalenga katika kutumia fedha zetu wenyewe katika sehemu ya maendeleo. Naipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, naziunga mkono hoja hizi. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa na mimi nafasi nichangie Bajeti iliyoletwa mbele yetu na Waziri wa Fedha. Kwanza napenda kuwapongeza sana Mawaziri wote wawili waliotoa Bajeti, na ninaipongeza Serikali kwa utekelezaji wa Bajeti ya mwaka jana kwa sababu Bajeti iliyopita mwaka jana 2004 kwa kweli imetekelezwa vizuri na hii nategemea kwamba itatekelezwa vizuri. Ninaipongeza Serikali, hasa nampongeza Rais wetu Benjamin William Mkapa kwa kuwa mstari wa mbele kwa kuiomba Mataifa tajiri ambayo tunawakopa watusamehe madeni. Hilo itakuwa msaada sana kwetu katika Bajeti hii na katika Bajeti zijazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli hakuna ubishi kabisa kwamba Bajeti yetu au Mapato yetu yameongezeka. Yameongezeka sana na ninaipongeza Serikali pamoja na *TRA* kwa makusanyo mazuri waliyofanya mpaka tukafikia hapa, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Kuna mafanikio hata katika miradi ya Wananchi Vijijini inaonekana kabisa wanasema kwamba Serikali sasa ni tofauti na kipindi kilichopita kwa ajili ya kuona fedha zinafika katika miradi huko Vijijini.

Mheshimiwa Spika, ningependa tu kusema tatizo moja, kwamba tatizo la kushuka kwa thamani ya fedha zetu. Hili ni tatizo ambalo sijui Serikali ifanye nini kwa sababu kushuka kwa fedha ukiangalia mwaka 1995/1996 dola moja ilikuwa na thamani ya shilingi 850 ya fedha zetu, kwa sasa dola moja ni 1,080 hii hata mishahara ya Watumishi wanapolipwa inaonekana hata ukiongeza bado ni ndogo, bado haitimizi mahitaji.

Ukiangalia katika nchi nyingine kwa mfano Kenya mshahara wa Katibu Tarafa ndio unalingana na mshahara wa *RC* Mkuu wa Mkoa huku kwetu. Ni kwa sababu thamani ya fedha zao hailingani kabisa na ya kwetu, ya kwetu imekuwa ni kama sijui niseme nini.

Sasa mwalimu wa kawaida huko Kenya mshahara wake ni sawa na Mkurugenzi huku kwetu. Sasa ningeomba hebu tuangalie hili suala kwa sababu hili ndio linatuumiza, bado linatuumiza kabisa na inaonekana hata juhudi zetu za kukusanya Mapato bado Benki Kuu nadhani Serikali ikae na Benki Kuu kuangalia hili tatizo, kwa sababu ni tatizo mojawapo ambalo linaturudisha nyuma hii kushuka kila siku kwa thamani ya fedha zetu ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la mikopo. Serikali imeweka utaratibu mzuri wa kupunguza umaskini, MKUKUTA na Serikali imebuni Sera ya Taifa ya Mikopo midogo midogo, *National Microfinance Policy* ni nzuri sana na inasaidia.

Mheshimiwa Spika, lakini nina tatizo hapa bado utaratibu na kanuni na sera iliyowekwa sijui kama itawafikia Wanakijiji ambao umaskini ndio umekithiri huko Vijijini. Kwa sababu haya masharti yenyewe sidhani kama wanakijiji wanaweza wakayamudu. Kwa mfano ni Wananchi wangapi maskini ambao wana hatimiliki, ambao wanaweza wakakopa hizi fedha? Sasa Serikali ina mpango gani kuwasaidia wale watu wenye hali ya chini? Nitoe mfano, Serikali imebuni njia nzuri sana ya kuwasaidia wakulima. Tulitoa pesa za pembejeo, lakini hizo fedha za pembejeo hazikufika Vijijini kule kwa wakulima wadogo wadogo, zimechukuliwa na matajiri tu.

Ni watu matajiri ndio wamechukua hizo fedha kwenda kujengea magorofa, wale ambao walitarajiwa kwamba wapate hawakupata hata huu mkukuta, nadhani inawezekana ikawasaidia tena wale matajiri waneemeke zaidi wapate fedha zaidi maskini wale wa chini wazidi tu kunyong'onye bila kuwa na fedha. *(Makofi)*

Ndio maana *gape* imetokea kubwa sana hapa Tanzania kuna matajiri wa hali ya juu na maskini wengi sana, matajiri ni kama asilimia 10 tu wengine wote ni maskini lakini wao ndio bado wanajaliwa kupata mikopo hii. Nashukuru sana mpango ni mzuri lakini hebu tuangalie mikopo Vijijini, katika Jimbo langu mimi sijawahi kumwona Mwananchi aliyekopa hakuna kabisa. Lakini Waziri wa Fedha kila siku anasimama pale anasema mapesa yamejaa kwenye Mabenki kopeni, ukienda Benki kwanza wanasema tuna eneo hawataki watu wakope ambao wako mbali. Sasa Vijiji viko mbali na Mabenki, wanataka wafanyabiashara wadogo wadogo walioko karibu ili waweze waka-*monitor* sasa Vijiji vilivyoko mbali kule hakuna Mabenki. Nashukuru hapa umetaja Mabenki Kata, haya Mabenki Kata ndio yanaweza yakawasaidia hawa watu maskini walioko Vijijini. Lakini kwa utaratibu huu wa kwamba Jimbo langu niambiwe nitegemee Benki iliyoko Monduli nikienda pale Arusha, Arusha ndio karibu zaidi kuliko Monduli, naambiwa Benki lako ni Monduli jambo ambalo haliwezekani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi bado nasema Serikali iige utaratibu wa *TASAF* kwa watu wengine wanalalamikia *TASAF,* lakini vile mimi bado sijapata lakini naona kwamba utaratabu huu wa *TASAF*, *TASAF* imefikisha miradi Vijijini pesa imefika Vijijini muige utaratibu huo wa *TASAF*. Mimi naona *TASAF* ndio kama ni kuondoa umaskini na kuwasaidi wanyonge naona *TASAF* ndio inasaidia wanyonge na ndio inafikisha fedha kwenye miradi ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la *SACCOS*. Naomba utaratibu huu wa kusaidia *SACCOS*, kukopesha *SACCOS* hizi *SACCOS* ziko Vijijini lakini hakuna utaratibu wowote wa fedha kutoka Benki kwenda kwenye hizo *SACCOS* kupata mikopo. Kwenye Jimbo langu sisi tumeanzisha nyingi, tuna *SACCOS* moja ambayo ina mifugo madume 150, mwezi wa saba watauza hao ng'ombe wote. *(Makofi)*

Tuna *SACCOS* nyingi sana, lakini hawana elimu tunaoma elimu, wapate elimu namna ya kupata msaada katika Mabenki haya, wapate mikopo. Lakini kama mkiweka semina mijini tu bila kufika Vijijini kuwaelimisha Vijijini, huu umaskini hautatoka hata siku moja. Jambo lingine nipende kuzungumzia suala la elimu, Serikali imesaidi imepunguza au imewasaidia watu wasio na uwezo kupunguza ada kutoka shilingi 40,000 kwenda 20,000. Lakini waliopunguziwa ni wale wanafunzi wa kutwa, sasa kule kwetu wafugaji huwezi kuwapata wafugaji wanaosoma kutwa. Wote wako bweni *(boarding),* sasa kuna wengine ambao hawana uwezo kabisa lakini wako *boarding.*

Ningeomba utaratibu huo ufanywe kwa hawa watoto maskini walioko *boarding* ambao hawakupata msamaha huo au msaada huo, naomba Serikali iangalie tena hawa wanafunzi walioko *boarding* kwa sababu ni watu ambao hawana uwezo kama wale wengine wasaidiwe nao waingie katika punguzo hilo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni ugawaji wa fedha katika Halmashauri zetu katika Wilaya zetu. Unakuta kila mara Arusha inatajwa kwamba inapata fedha nyingi sana, lakini mtazamo wa Arusha ni hapo Manispaa ya Arusha. Ukienda katika Vijiji Halmashauri nyingine ambazo ziko nje ya mji wa Arusha, ni Halmashauri ambazo hazina kitu kabisa kama Wilaya yangu yaani vitu vinavyosemekana kwamba tumepata nini na nini sisi hatuna. Umeme hatuna, barabara hatuna, lakini nazungumza kwamba Arusha ina barabara za lami. Kwa hiyo ningependa kusema kwamba huu mgao usiangalie, usitazame sana Mikao itazame Halmashauri. Je, kama tunavyosema kwamba tupeleke fedha kwenye Halmashauri hiyo ndio inaweza ikatusaidia, ukigawa Kimkoa kwa kweli hali bado ni mbaya zaidi katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, napenda tu kusema hayo machache na ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nitoe hayo niliyosema. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kuweza kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Bajeti hii ya Wizara ya Fedha pamoja na Mipango. Kwanza na mimi niungane na wenzangu kutoa pole kwa familia ya marehemu Mheshimiwa Abu T. Kiwanga ambaye amefariki Mbunge wa Kilombero naomba Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi Amina.

Napenda nichukue nafasi hii pia kuwapongeza walioteuliwa na Chama cha Mapinduzi ili kupeperusha bendera katika uchaguzi ujao Mheshimiwa Jakaya M. Kikwete, Mheshimiwa Rais Karume kutoka Zanzibar na Shein Makamu wa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mimi nichukue nafasi hii pia niwapongeze viongozi wote katika Wizara hii ya Fedha na Mipango ambao wameandaa Bajeti hii, na kuipongeza *TRA* jinsi ilivyoweza kufanya kazi na kuweza kuongeza Mapato ya Serikali katika kipindi hiki. *(Makofi)*

Lakini pili, pia nimpongeze Rais wetu Benjamin William Mkapa ambaye amesimamia vizuri sana Serikali hii ili kuweza kuondoa kero mbalimbali katika nchi yetu ya Tanzania, ni kero za msingi kama vile kuondoa ada ya *UPE* katika kipindi hiki cha miaka mitano, Kodi ya Maendeleo na Ushuru wa aina mbalimbali kwa Wananchi maskini wa kawaida katika nchi yetu. Lakini lipo jambo moja ambalo sisi kama Wabunge tunapokuwa huko katika Majimbo yetu tumekuwa tukilalamikiwa katika nalo ni suala la afya. Suala la afya, uchangiaji wa afya kwa kweli Wananchi katika Jimbo langu la Kalambo wamekuwa wakililalamikia sana, na wanaiomba Serikali ione ni jinsi gani itavyoweza kupanga nayo uchangiaji huu wa afya kwa sababu ya umaskini wa Wananchi. Bado inaonekana ni kero na wanaomba Serikali itumie mbinu zake zote kuhakikisha kwamba si wakinamama tu na watoto wenye chini ya umri ya miaka mitano wanaotibiwa bure, lakini wapo wazee ambao wamelitumikia Taifa hili na hawana uwezo wa kuweza kujitibu na tukielewa kabisa mtu akifikia katika umri mkubwa magonjwa yanaanza kuongezeka ya ajabu ajabu, wasaidiwe waweze kutibiwa nao pia bure pamoja na Wananchi wengine. Hii itaweza kusaidia kuboresha afya za Watanzania ili waweze kushiriki vizuri katika uzalishaji wa mali na kuongeza pato la Taifa.

Naipongeza Serikali pia kwa kuongeza Pensheni kwa wastaafu na wale waliochukua mkupuo wakarudishwa kwenye daftari la Pensheni, lakini wapo wafanyakazi walioifanyia Serikali hii kwa mkataba hasa katika Idara ya Polisi na Magereza. Hao walifanyakazi kwa mikataba na walipoondoka wamepata *gratuity* tena ndogo, basi wameondoka lakini wanapata matatizo sana kama hawakuitumikia nchi hii. Naomba Serikali nayo iweze kuangalia ni jinsi gani ya kuwarudisha, au kuweza kuwapatia kitu kile kitakachoweza kuwasaidia na wao wajione kwamba wamekuwa ni sehemu ya jamii hii na ni sehemu ya Serikali hii, wameifanyia kazi Serikali hii na wao waweze kustahili kupata malipo yatakayowasaidia katika matatizo yao mbalimbali kama hao waliorudishwa katika daftari la Pensheni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mipango ni bahati mbaya sana kwamba kwa kipindi cha miaka mimi nimekuwa nikizungumzia kwamba mipango wakati mwingine haiangalii vizuri ukuaji wa Mikoa na mahitaji ya Mikoa, na mwaka jana mimi na Mheshimiwa Lucas Selelii tulizungumzia sana juu ya mipango inayofanyika katika nchi hii kwamba Mikoa mingine huwa haiangaliwi na inapewa fedha kiasi kidogo ukilinganisha na Mikoa mingine. Mheshimiwa Waziri Mkuu akatutuma kwa Waziri wa Fedha tukae tuzungumze naye kuhusu suala hili, tumekwenda kuzungumza naye akatuahidi kwamba jambo hili tutaona jinsi ya kuweza kulikabili katika kipindi kijacho, tukashukuru tukizani kwamba mambo yatakwenda vizuri. Lakini ukiangalia katika kitabu hiki cha mpango wa maendeleo wa mwaka 2005/2006 Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji ukurasa wa 51 jambo lile lile linajitokeza, sijui ni kwa nini, Mkoa wa Arusha hauna fedha za nje, Mkoa wa Kigoma hauna fedha za nje, Mkoa wa Tabora hauna fedha za nje na Mkoa wa Rukwa

fedha za nje. Sasa ukiangalia na Mikoa mingine ukilinganisha kwa kweli unaona aibu, unaona aibu jinsi gani Mikoa mingine iwe na mabilioni ya lakini Mikoa hii inapewa tu fedha kiasi kidogo. Je, Serikali haikuona ni jinsi gani ya kuweza kupanga walau ikaongezewa hii ambayo haina fedha za nje ikiongezewa walau kiasi kidogo.

Kwa kweli ni jambo ambalo nimelizungumzia kwa miaka mitano lakini inaonekana sikuweza kufanikiwa kushawishi Ofisi ya Mipango Wizara ya Mipango hii ili iweze kuona jinsi ya kuweza kusaidi Mikoa hii ambayo kihistoria imebaki hivyo. Sasa na Waziri wa Fedha naye yupo hapa na mwaka jana tumezungumza naye katika Ofisi yake pale akatueleza kwamba ataliangalia mwaka huu ataona jinsi ya kuweza kufanya. Lakini yamerudia yale yale, sasa nasema tuendelee tu. Ni kweli tunahitaji kasi kubwa zaidi ya kukua kwa uchumi, kama mkakati mkubwa utakaotufanikisha azma yetu ya kujitegemea. Lakini azma hii kama hatutaiwekea mkakati maalum wa kuweza kusaidia maeneo yale ambayo wananchi wengi wa Tanzania wako katika shughuli za kiuchumi wakulima ambao ni asilimia kubwa, pamoja na wafugaji ambao ndio asilimia kubwa ya Watanzania walipo kule tusipowekea mkakati maalum wa kuwasaidia Wananchi katika maeneo haya uchumi huu tunaotarajia uweze kukua kwa haraka kwa kweli hauwezi ukakua kwa kasi tunavyotarajia. Hivyo tunaiomba Serikali ijaribu kuangalia ni jinsi gani ya kuangalia hawa maskini walio wengi katika nchi hii, wakulima na wafugaji waweze kupewa ruzuku au waweze kupewa mikopo ili waweze sasa kuzalisha zaidi ili tuuze zaidi ili na uchumi uweze kukua zaidi. Utegemezi wa Bajeti yetu kwa asilimia 41 bado ni kiwango kikubwa, tumejitahidi kuweze kushuka kutoka 47 kuja 41. Lakini mimi nasema Serikali bado iendelee na mipango yake ili tuweze kuona kama tunaweza kushuka zaidi tukarudi mpaka kwenye 20, asilimia 20 ndio tegemezi katika Bajeti yetu. Bila kufanya hivyo kwa kweli Bajeti zetu zitakuwa bado zina matatizo na tutaendelea kuwa tegemezi kwa nchi zilizoendelea.

Kuhusu kilimo, tunaishukuru Serikali mwaka jana imeweza kutoa ruzuku kwa Mikoa minne Rukwa, Mbeya, Iringa na Ruvuma na uzalishaji ukaongezeka kiasi kidogo. Lakini ruzuku ilichelewa sana kutolewa, tunaomba Serikali isiwe na urasimu kwa sababu Wananchi wako radhi kufanya kazi ya kuzalisha zaidi. Lakini ruzuku hii iliyoahidiwa inapochelewa kutolewa inakuja kutolewa mwezi wa 11 wakati tayari watu wameshachelewa kuweka mbolea katika mazao yao kwa kweli haisaidii sana, hatuisaidii nchi hii. Tunaomba kwanza Serikali izingatie mahitaji ya mbolea kwa kila Mkoa sisi Mkoa wa Rukwa tulikuwa tunahitaji karibu tani 23 za mbolea, lakini tuliyopata ni chini ya tani 4,000. Sasa ukiangalia mahitaji ya Mkoa na kiwango cha mbolea tuliyoipata kwa kweli hatuwezi tukazalisha kwa matarajio ya Serikali ili tuweze kuchangia na sisi katika Pato la Taifa. Tukipewa kile tunachohitaji kwa wakati nina uhakika kabisa tutazalisha zaidi kwa sababu Wananchi wetu wako tayari kufanya kazi ya kilimo, lakini misaada hii ambayo Serikali inaahidi kama ruzuku haifiki kwa wakati unaopatikana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la mifugo, katika kujibu swali langu muda si punde ulipita imeonyesha Serikali haikuwa makini na Wizara ingepaswa ikiri tu kuwa haikuwa na takwimu kuhusu mifugo waliokufa kutokana na chanjo ile. Kwa sababu ni kweli ilitokea uchanjaji mbaya wa mifugo na mifugo mingi ilikufa, walipoambiwa wataalam warudi kwenda kuangalia mifugo ili waweze kuhesabu mizoga, waliogopa kwa

sababu hasira ya Wananchi ilikuwa ni kubwa sana wakaogopa kwenda wakakaa zaidi ya mwezi mzima hawajaenda kule. Sasa Wananchi wangeweka mizoga wanasubiri tu wataalam kwa muda ambao hawategemei watakuja, wengi walizika mizoga hiyo wengine wakatupa na ng'ombe 17 niliokuwa nasema ni wa mtu mmoja tu ambaye alifiwa karibu zizi zima katika kijiji kimoja katika Kata ya Mambokenya. Kwa kweli huu ni udhaifu lazima Serikali ikubali kuwajibika katika mambo haya wataalam wake wanapokosea ni lazima Serikali ikubali kubebe lawama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la miundombinu, tuinashukuru Serikali imejitahidi sana kujenga miundombinu lakini katika Mkoa wetu wa Rukwa barabara ya Tunduma - Sumbawanga ni muhimu sana na hata chakula mnachokitafuta inapotokea njaa katika nchi hii ni lazima kipite katika barabara hii. Waziri wa Ujenzi aliahidi mbele ya Makamu wa Rais aliyekuwa anafungua madaraja yale 11 kwamba mwezi wa nne mwaka 2005 ujenzi utakuwa umeanza lakini mpaka leo hakuna chochote, mmekaa kimya lakini sehemu nyingine barabara zinajengwa! Tunaomba na sisi barabara hii ijengwe kama Serikali ilivyoahidi ili na sisi tuweze kusafirisha mazao yetu kupeleka katika masoko mbalimbali. *(Makofi)*

Naishukuru Serikali imekubali kuondoa *VAT* katika vifaa vya treni hivyo *TAZARA* na *TRC* kwa kweli watapata unafuu. Lakini naomba niulize hivi suala la deni la ujenzi wa reli ya *TAZARA* likoje, mbona Serikali imekaa kimya juu ya suala hili? Kwa kukaa kimya na kutolipa deni hilo ni aibu na wala hatumuenzi Baba wa Taifa aliyetusaidia kupata reli hii. Nadhani umefika wakati wa kukaa kufikiria kuona ni jinsi gani tutakavyoweza kulipa walau kiasi kidogo kidogo pamoja na uchumi tunaoupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo, naunga mkono Bajeti hii kwa sababu ni Bajeti ambayo kwa kweli inamwangalia mwananchi maskini wa kawaida ili aweze kuondokana na mzigo mkubwa wa maisha magumu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja ya Bajeti hii ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza mchango wangu, naomba nitumie nafasi hii kutoa salaam za rambirambi kwako wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wote, familia, ndugu na wananchi wa Jimbo la Kilombero kwa kumpoteza Mheshimiwa Abu Kiwanga, aliyeitwa mbele ya haki. Namwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Spika, vile vile kwa niaba ya wananchi wote wa Jimbo la Nanyumbu, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mbunge wa Chalinze na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuteuliwa, tena kwa kura za kishindo kuwa mgombea wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Chama cha Mapinduzi. Uteuzi ambao

umeungwa mkono na Watanzania wa rika zote kuanzia watoto, vijana hadi wazee na hata wana CCM wote, marafiki na wapenzi wa CCM na hata Wapinzani wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi ambao tunasafiri kwa kutumia barabara kupitia Mikoa, Wilaya na hata vijiji vya Tanzania, tumekuwa mashahidi wa wananchi wanaounga mkono uteuzi huo wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa niseme wazi kuwa hata sisi Wabunge tunaotokana na Chama cha Mapinduzi, hadhi yetu imepanda zaidi kutokana na uteuzi huo. Tumepokea pongezi nyingi lakini kubwa zaidi tumepokea ahadi za kuungwa mkono Mheshimiwa Jakaya Kikwete kutoka kwa wapiga kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jakaya Kikwete, wananchi wanayo matumaini makubwa kwake na mimi nimtakie kila la kheri katika uchaguzi unaokuja na Mwenyezi Mungu awe pamoja naye siku zote, kumwongoza ashinde na hatimaye aongoze nchi yetu Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza wa Mheshimiwa Jakaya Kikwete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein alionyesha busara nyingi kwa kutochukua fomu ili ateuliwe kuwa mgombea wa Kiti cha Urais. Kwa nafasi aliyonayo ya kuwa msaidizi mkuu wa Rais Benjamin Mkapa, wengi walitegemea kuwa angeweza kuchukua fomu. Lakini Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein hakutaka kutumia nafasi hiyo ya juu zaidi ukiondoa ya Urais kama kishawishi cha yeye kuchukua fomu.

**MBUNGE FULANI:** Naam!

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Hakika watu wa aina ya Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, ni ...

**MBUNGE FULANI:** Wachache.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Adimu kupatikana hapa Tanzania na hata duniani kote hivi sasa. Hivyo nampongeza sana Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na namtakia kila la kheri katika kazi zake zote. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** *Amin!*

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Spika, vile vile nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Zanzibar, kwa kuteuliwa tena kuwa mgombea wa nafasi ya Urais wa Zanzibar kupitia Chama cha Mapinduzi. Ni imani yangu kuwa Wazanzibar watampa ushindi

mkubwa Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa kuzingatia mengi aliyoyafanya kwa manufaa ya Wanzibar ndani ya kipindi hiki kifupi cha miaka mitano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nianze mchango wangu wa hoja ya Bajeti. Lakini kwanza kabisa nimpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin Mkapa, kwa mafanikio makubwa yaliyokwishapatikana katika nyanja za siasa, uchumi na ustawi wa jamii. *(Makofi)*

Hotuba za Bajeti za Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na ile ya Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, Waziri wa Fedha, zimeorodhesha mafanikio hayo. Lakini wananchi katika maeneo yao ni mashahidi tosha kwa hayo yaliyoorodheshwa. Kweli ni mafanikio makubwa na ya kujivunia, hivyo nimpe hongera sana Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa na Serikali yake ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naamini kuwa yule anayedai kuwa Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa na Serikali yake ya Chama cha Mapinduzi haijafanya lolote katika kuleta maendeleo ya nchi hii, ni mgonjwa wa akili. Tena wananchi wanapaswa kumwogopa mtu kama huyo kama wanavyoogopa magonjwa ya Ukoma, Malaria na UKIMWI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutamkumbuka na kumuenzi Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa kwa mafanikio hayo makubwa. Ni imani yangu kuwa wananchi wataendelea kukichagua Chama cha Mapinduzi kiunde Serikali ya Awamu ya Nne ili kuendeleza kazi nzuri iliyokwishafanywa na Serikali ya Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii inazungumzia maeneo kadhaa yaliyochochea ukuaji wa uchumi hadi kufikia kiwango cha pato la Taifa la kuridhisha la 6.7% mwaka 2004. Maeneo ambayo nitayazungumzia kwa kifupi ni kilimo, viwanda na utalii. Haya ndio maeneo ambayo Watanzania wanaweza wakashiriki kwa ufanisi mkubwa kama watawezeshwa.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi nimekuwa natoa mfano wa zao la korosho maarufu katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani, Ruvuma, Dar es Salaam na Tanga. Mkulima wa korosho anachohitaji ni zana za kulimia ziwe za kukodi au za kumiliki mwenyewe. Mahitaji mengine ni mashine za kupulizia dawa nazo zinawezakuwa za kukodi au za kumiliki mwenyewe. Lakini vile vile mkulima wa korosho anahitaji dawa kwa wingi na kwa wakati ili kupambana na magonjwa na viuatilifu vya mikorosho.

Serikali ikishamwezesha mkulima wa korosho kupata vitu hivyo kwa wakati muafaka basi Serikali itegemee kupata mapato makubwa kutokana na kodi inayotozwa kwenye zao la korosho. Aidha wakulima nao wataondokana na umaskini kutokana na mapato makubwa watakayopata. Mkorosho uliotunzwa vizuri unaweza ukatoa kilo 50 za korosho ghafi na kwa bei ya sasa hivi ya kilo moja kuuzwa kwa shilingi 700 nina hakika mkorosho mmoja unaweza kumwingizia mkulima sio chini ya 35,000/=.

Mheshimiwa Spika, ni kawaida ya wakulima wa korosho kuwa na mikorosho 100 na kuendelea. Sasa kwa kiwango hicho mkulima ana uhakika wa kupata shilingi 3,500,000 kwa mwaka. Wapo wakulima wengine ambao wana mashamba yenye mikorosho zaidi ya 500, nina hakika kipato chao kitakuwa kikubwa zaidi. Kinachohitajika ni Serikali kuamua na kutekeleza kwa dhati yale yote wakulima wanayohitaji ili kuongeza tija katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo linaweza kuinua uchumi wa Tanzania juu zaidi ni la viwanda. Hivi sasa bado tunavyo viwanda ambavyo vinafanya kazi kwa kutumia *shift* moja kwa siku na vingine *shift* mbili kwa siku ya saa nane, nane. Sasa viwanda hivi vingepewa motisha wakapanua angalau vizalishe kwa saa 24 kwa siku kwa kuwa na *shift* mbili za saa 12, 12 au *shift* tatu za saa 8, 8. Nina hakika kwa kuongezeka kwa *shift* uzalishaji utaongezeka hivyo kuongeza Pato la Taifa. Lakini vile vile kuongezeka kwa *shift* kutaongeza ajira kwa Watanzania wengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sehemu ya mwisho ambayo nilitaka niizungumzie ni utalii. Tanzania imejaliwa kuwa na vivutio vingi vya utalii vinavyopatikana karibu nchi nzima lakini hivi sasa ni sehemu ndogo tu ya nchi ndiyo imeendelezwa kwa ajili ya utalii. Ni muhimu sasa utalii ukaenea nchi nzima na Watanzania wakawezeshwa kwa mitaji na ujuzi ili washiriki kikamilifu katika biashara hii. Nina hakika kupanuka kwa biashara ya utalii kutachangia sana kukua kwa uchumi na kupanuka kwa ajira nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango wangu huo mdogo, nimalizie kwa kuiunga mkono Bajeti hii kwa asilimia mia moja lakini mwisho nikushukuru tena wewe kwa kunipa nafasi hii na niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hotuba ya Bajeti pamoja na ile ya Mipango.

Awali ya yote, kwa niaba ya Jimbo langu la Kibiti na wapiga kura wangu, napenda kupeleka salaam za rambirambi kwa wapiga kura wa Jimbo la Kilombero kwa kupoteza Mbunge wao, Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga. Mungu ailaze mahali pema peponi roho yake. *Amin.*

Pia napenda kuwapongeza wagombea wa Urais, upande wa CCM Mheshimiwa Jakaya Kikwete na wengine wote katika Vyama vya Upinzani, nawapongeza kwa kuchaguliwa na Vyama vyao kugombea Urais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru sana Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango kwa hotuba zao ambazo zimeeleza kinaganaga uchumi wetu unakotoka na unakoelekea. Niseme tu naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Ningependa kunukuu sehemu tu ya hotuba zote mbili halafu niweze kuchangia. Hotuba ya kwanza ni ile ya Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji, ukurasa wa 58, ibara ya 85 inayosema kwamba: "Serikali imetayarisha mkakati huu kwa kutumia uzoefu uliotumiwa na nchi za Kusini Mashariki ya Asia ili kuweza kuharakisha zaidi ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini nchini na hivyo kuyafikia mapema zaidi malengo ya Dira ya Taifa ya 2025."

Upande wa Wizara ya Fedha, napenda kunukuu kutoka ukurasa wa 52, ibara ya 60 inayosema kwamba: "Malengo na mikakati niliyoitaja hapo juu, inategemea juhudi za dhati za kila Mtanzania, kila mzalendo na kila mwenye nia njema na Taifa letu ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi na huduma za jamii. Lengo kuu letu ni kuhakikisha umaskini unapungua haraka hatua kwa hatua."

Mheshimiwa Spika, kusema kweli hatua tunazozipiga katika uchumi zinaonekana na walimwengu wote na hakuna mtu atakayepinga isipokuwa yule anayetaka kupinga tu. Ninachotaka kusema ni kwamba uchumi mzuri na endelevu ni ule watu wengi wanashiriki katika uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo waliyosema wataalam wa uchumi kama Adam Smith, Jeremiah Banthan, John Stewart Mill na wengineo. Wao wanasema hivi, uchumi mzuri na endelevu ni ule ambao watu wengi wanashiriki kwa pamoja kuzalisha tena kwa maarifa na akili nyingi. Haya ndio ambayo walikuwa wanayasema Waziri wa Mipango na Waziri wa Fedha kwamba hapa tulipo ina maana tukazane zaidi ili kuzalisha zaidi kuupunguza umaskini na kujiondoa hapa tulipo sasa hivi tuko tegemezi 41% tunataka kuipunguza hii asilimia ya utegemezi kwa wenzetu ambao na wao wanafanya juhudi kuinua uchumi katika nchi zao.

Mheshimiwa Spika, sisi kwetu hapa Tanzania tungeweza sio kuwa na Bajeti ya trilioni 4.2 bali tungeweza kuwa na trilioni 7.8 tena haya ningeweza kuyathibitisha moja baada ya moja kama nitapata nafasi katika mazao, madini, utalii na vinginevyo.

Kwanza upande wa kilimo, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tukipiga kelele hapa tangu mwaka 1995 wale tulioingia mwaka 1995 mpaka sasa hivi, suala la kilimo hapa Tanzania linasemwa kuwa ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi hii bado halijafanyiwa kazi na lau tungekifanyia kazi kilimo tu peke yake nadhani tungekuwa tumepiga hatua kubwa zaidi katika uzalishaji. Kwa mazao kwa mfano pamba, korosho, kahawa na kadhalika mazao haya peke yake yangetuondoa sisi katika umaskini lakini kwa vile hatukuweza kutilia mkazo viwanda mfano tulikuwa na viwanda vya kutengeneza nguo 12, viwanda vya korosho 11 viwanda vile vimekufa. Sasa kufa kule maana yake nini? Najua viwanda vya nguo mpaka sasa hivi tuna viwanda vitatu tu kile cha Urafiki, *Mwatex* na *Mutex* na vinafanya kazi chini ya uwezo wake lakini viwanda karibu tisa vya pamba vimekufa.

Mheshimiwa Spika, kwa nini tuuze pamba ghafi nje wakati ambapo sisi hapa wenyewe tungeweza kuchambua pamba ile tukatengeneza nyuzi kiwanda cha Tabora kile, tukatengeneza nguo tukauza huko na hiyo ndio ambayo ingetukwamua zaidi kukuza

uchumi. Kwanza tungepeleka viwanda vidogo vidogo kama walivyofanya wenzetu kule India huko vijijini *cottage industries* ingekuwa imetoa ajira kwa vijana na watu kule vijijini kwa asilimia kubwa sio hivyo tu bali tungeongezea thamani pamba yetu na badala ya kuuza nje ghafi tungeuza nguo na tungetumia vizuri soko la *AGOA.* Sasa kwa nini mpaka sasa hivi tunakazania kuuza pamba ghafi kule nje wakati ambapo tulikuwa na uwezo wa kuchambua, kutoa nyuzi na kutengeneza nguo hapa hapa na kuuza nje? Hii tumefanya wenyewe makusudi tumeua viwanda vile ili tuuze mali ghafi pengine kwa faida ya watu wachache haijulika. *(Makofi)*

Hivyo hivyo korosho tulikuwa na viwanda 11 sasa hivi hakuna hata kiwanda kimoja cha korosho kinachofanya kazi. Korosho zinabanguliwa kwa mkono tu na pengine kiwanda kimoja kile cha Masasi kilitaka kufanya kazi lakini bahati mbaya hakikuweza kubangua hata korosho moja. Sasa kwa nini hivi viwanda vimekufa badala ya kuvitengeneza au kuvihuisha ili vibangue korosho ili kuongeza thamani ya korosho ile? Kwa sababu korosho ikiwa ghafi ukiuza nje tani moja ni dola 850 lakini ukiwa umebangua kwa tani moja ni dola 4,200. Sasa utaona kuna tofauti kubwa kabisa. Sasa tunaendelea kuuza korosho ghafi huko nje maana yake nini?

Mheshimiwa Spika, kule India wafanyabiashara wake wanawapa *bonus* na Serikali kwa kununua korosho ghafi kutoka nje, kutoka Afrika Mashariki na Afrika Magharibi. Wakiingiza India korosho ghafi nyingi wafanyabiashara wanapata *bonus.* Sasa tuna wasiwasi kwamba hawa wenzetu walioua viwanda vyetu vya korosho hapa isiwe kwamba wanashirikiana kupata *bonus* ya wafanyabiashara kule India ndio maana viwanda hivyo vimeuawa. Tatizo letu ni nini?

Tumekazania kwamba tunataka kuongeza thamani kwa mazao yetu lakini tumeendelea kuviua viwanda vile ambavyo vingeweza kufanya kazi nzuri ya kubangua korosho au ya kuchambua pamba na kutengeneza nguo ili tuweze kuongeza thamani ya mazao yetu, hivyo hivyo katika mazao yote.

Mheshimiwa Spika, hali hii ndio aliyosema Adam Smith: *"If you want the economy which is sustainable it should be that of many hands should participate in the production."* Ukitaka uchumi wako uwe endelevu na wa kukua ni lazima mikono mingi ishiriki sio mikono michache iliyoko mjini ndio inashiriki, hapana kule vijijini tuna nguvu kazi ya kutosha na huko ndiko ambapo kusema kweli tungeanzisha viwanda kule vijana wote wangehamia vijijini na miundombinu yote ingetayarishwa vizuri ingefanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba suala hili la kuongeza thamani kwa mazao yetu ni lazima sasa liwe la msingi na tusiuze malighafi na kilimo chetu kiwe cha biashara, tuache kilimo cha kujikimu cha jembe dogo lile la *chikondora,* lile tuliache.

Mimi wakati fulani nilisema jembe la mkono lipigwe marufuku, watu wakaniona kwamba ni mwendawazi au kichaa. Si kichakaa kama tutaendelea kuruhusu jembe la mkono basi litatutawala lile hatutaweza kupindua kilimo chetu ni lazima sasa tupindue kilimo chetu. Jembe la mkono kama halipigwi marufuku, liondolewe kabisa. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Lipigwe marufuku.

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Hiyo ndiyo njia pekee ya kukifanya kilimo kiwe kilimo cha biashara! Jembe la mkono utalima hekta ngapi? Kwa hiyo, mimi nasema matrekta, plau na kadhalika yafanye kazi. Watu wanasema kwamba nitakosa kura, achilia mbali nikose kura na mimi pengine ...

**MBUNGE FULANI:** Hugombei.

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Sigombei eeh, sawasawa.

Mheshimiwa Spika, nasema ili kukipindua kilimo chetu kiwe kizuri cha kuzalisha uchumi ambao utatuondoa katika hali hii ya umaskini nadhani sasa wakati muafaka umefika wa kupindua kabisa kilimo chetu kiwe cha biashara, sio kile cha kujikimu na tuzalishe mazao ambayo tayari tunayaongezea thamani ili watu wetu wanufaike huko vijijini na kwa maana hiyo basi tutaupunguza umaskini taratibu, taratibu na hatimaye kufikia lengo letu la Taifa lile la 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu ulikuwa juu ya huko vijijini *cottage industries* na kuimarisha uchumi kule vijijini ili watu wetu waweze kukwamuka kutoka katika hali ya umaskini.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia mawili, matatu.

Mheshimiwa Spika, moja kwa moja, nianze kuwapongeza Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba na Mheshimiwa Alhaj Dr. Abdallah Kigoda, Manaibu wote wawili wa Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu na Mheshimiwa Alhaj Mufti Abdisalaam Issa Khatibu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze tena watendaji wote, Makatibu Wakuu wa Wizara zote mbili pamoja na akinamama ambao wako ndani ya Kitengo hiki kwa Wizara zote mbili kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa kuandaa Bajeti kikamilifu. *(Makofi)*

Pia nikupongeze wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika kwa kuongoza kiti chako ndani ya mikutano ishirini ya Bunge. Nikupongeze sana kwa kazi nzuri unayoifanya katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, nichukue nafasi ya pekee kumpongeza Jemedari, Rais wetu Mtukufu, Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa kwa kuongoza nchi yake kwa kipindi cha miaka kumi bila matatizo, kwa makini na kuiweka nchi yake mikononi mwa amani. *(Makofi)*

Pia nimpongeze kwa ku-*chair* kiti cha Mkutano Mkuu kwa kazi nzuri aliyoifanya kwa kuisimamia ambayo imetumika demokrasi ya uhakika na ya kweli isiyokuwa na mang'unguniko.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo nimpongeze moja kwa moja Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuteuliwa na wanachama wakamilifu asilimia mia moja, nampongeza sana na nina imani ni mwanzo mzuri ambao unaashiria ushindi wa kimbunga. *(Makofi)*

Pia niwapongeze viongozi waliofuatana naye kwa kuchaguliwa kwao Mgombea Mwenza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais na pia Mheshimiwa Aman Abeid Karume kwa kugombea nafasi ya Urais Zanzibar ambayo haina kipingamizi nina uhakika atashinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo kuisha naomba nichukue nafasi hii kwa masikitiko makubwa na kwa huzuni kwa kutoa rambirambi zangu za dhati kwa niaba ya wanawake wa mkoa wa Tabora ambao ninauwakilisha kwa msiba uliotufika hivi karibuni wa Mheshimiwa Mbunge mwenzetu Marehemu Abu Kiwanga, Mbunge wa Kilombero, Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo na rambirambi kwa uzito wake nianze moja kwa moja kwa kuchangia hotuba zote mbili zilizopo mbele yetu kwanza kwa kuunga mkono asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, unapounga mkono maana yake hotuba hizi hazina matatizo, ni hotuba ambazo zimepokelewa na wananchi kwa mipango sahihi, mipango endelevu na pia mapato na matumizi ya usimamizi ni mazuri kwa uhakika.

Mheshimiwa Spika, nimewajibika kuchangia hotuba hii hususan hizi mbili na hususan ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa sababu yeye ndiye kilindo, sisi Tabora tunasema kilindo kwamba ndiyo kwenye Hazina, kwenye kilindo kabisa ambako ndiko chakula kinapatikana na kinahifadhiwa.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha katika Bajeti yake amezungumzia suala zima la mafao ya watendaji, kwa kweli hilo nampongeza sana kwa sababu watendaji ndiyo wenye nchi na ndiyo wanaoishi na wananchi huko chini kwa ukaribu zaidi kujua matatizo yao. Ningeshauri Serikali iangalie pia kwa uzito wa pekee angalau wapewe vitendea kazi, ni muhimu sana kwa sisi ambao tunakwenda na ninashukuru kwamba wenzangu ambao ni Mawaziri ni Wabunge pia wanajua umbali wa kutoka Kata fulani na Kata fulani ambao ni mkubwa sana. Ningeomba angalau wapewe pikipiki hata kama iwe kwa mkopo au baiskeli kufuatana na uwezo walionao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwapongeza kwa hilo naomba pia nizungumzie habari ya *TASAF. TASAF* kwa kweli inafanya kazi nzuri sana na sasa hivi Watanzania asilimia kubwa sana ya nchi hii wameielewa na wanaikubali, sasa basi panapotokea

mipango na utekelezaji wake ndiyo kwenye tatizo, *TASAF* yenyewe kama *TASAF* haina tatizo, utekelezaji wake kwa mfano itakapoanza kufika mikoa yote na Wilaya zote ningeomba Serikali iangalie sehemu kubwa sana ya nchi hii ambayo iko nyuma kimaendeleo, zipewe kipaumbele Mikoa ambayo tuna uhakika kabisa kwa mfano Mkoa wa Tabora. Mkoa wa Tabora ni kisiwani hakuna miundombinu ya uhakika na hakuna barabara ambazo zinaweza zikaufungua Mkoa wa Tabora angalau hata kama kuna uwezekano wa *TASAF* kufanya kazi nzuri hata kama ya kuleta wawekezaji haiwezekani.

Kwa hiyo, nilikuwa namwomba Waziri wa Fedha kwanza aingalie TAMISEMI kwa undani zaidi ili TAMISEMI wakipata fungu kubwa zaidi la kwanza itabidi hizo pesa ziende upande wa barabara, Serikali ilikuwa na ahadi ya barabara ya kutoka Tabora kwenda Mwanza mpaka sasa bado Serikali inasuasua. Nilikuwa naomba ijitahidi katika miundombinu hiyo barabara kwa mwaka huu ifikiriwe ya Tabora kwenda Nzega, Tabora kupitia Sikonge kwenda Mbeya ambayo itakutana na barabara inayotoka Itigi kwa hiyo tutakuwa tayari tumeshafungua njia ya kutoka Mkoa hadi Mkoa mwingine, pia inayokwenda Kigoma.

Mheshimiwa Spika, wakulima wengi sana wapo Kigoma na kuna chakula cha uhakika lakini kwa bahati mbaya wanashindwa kabisa kuleta chakula mahali ambapo panastahili kwenda kuuza ili wapate soko.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo kwamba kutengwe fedha maalum hususan kwenye sehemu ambazo tuna uhakika kwamba ilikuwa mipango imefanywa ya maandalizi ya kina kuhusu mafanikio kutokana na ufinyu wa Bajeti kila mwaka tunasema ufinyu wa Bajeti, ufinyu wa Bajeti, vinginevyo sehemu hizi hazitafikiwa kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano uwanja wa ndege wa Tabora kwa miaka ya nyuma kabla ya vita ya Iddi Amini ilikuwa imetengewa mipango maalum kwa ajili ya kuutengeneza ule uwanja kwa sababu maalum lakini Wizara inajua na Serikali inajua hii imefikia wapi kuhusu uwanja wa ndege wa Tabora, ningeomba Serikali iangalie kwa kina sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa afya, mipango imeeleza kwamba itaboresha sana mambo ya afya, fedha imepanga itaongeza pesa kwa Wizara ya Afya, naomba liangaliwe suala zima la vituo au zahanati zilizoko huko walizojenga wananchi. Ukiuliza TAMISEMI wanasema fedha hazipo lakini wananchi wamejenga kwa mfano Wilaya ya Urambo ina vituo vimejengwa vya afya 22 tangu mwaka 2000 mpaka leo havifanyi kazi, wananchi wamejitolea tunawahamasisha wananchi wanajenga lakini matokeo yake Serikali haiangalii. Watoe kipaumbele wao wananchi waliamua kwamba wanatoa kipaumbele kwenye Zahanati na ndiyo maana wamejenga kila tunapokwenda kwenye mikutano tunaambiwa tembelea zahanati. Akina mama wanakufa, wanapokwenda kujifungua, watoto wanakufa, huduma ziko mbali, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa sababau wewe ndiye mwenye Hazina nzima na ninakuaminia naomba tafadhali uliangalie suala zima la zahanati walizojenga wananchi Tanzania hii katika

Bajeti ya safari hii wametenga vituo 40. Hivi hebu niambie unasemaje kuhusu vituo 40 kwa Tanzania hii, inagusa wapi na unafanya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nasema kwa kweli kwa kazi nzuri zinazofanyika tuna mipango ambayo ni endelevu na mingine ambayo si endelevu kwa hiyo, nilikuwa naomba Waziri wa Fedha aliangalie kwa uchungu huu, maana yake hata nikisema zahanati ya kwenda kujifungulia akina mama, je, akina baba hawaugui? Watoto hawaugui?

**WABUNGE FULANI:** Tunaugua kweli.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, naomba hili kwa kweli niweze kulipata tena akina baba ndiyo wabovu zaidi

**WABUNGE FULANI:** Aah!

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, nina imani amelisikia na amelipokea, mimi namjua, namfahamu mtiifu sana nalijua hilo *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kweli kuna mikopo ya akina mama. Mikopo ya akina mama inayotolewa na Mfuko wa Serikali Kuu ni kidogo sana.

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo!

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, milioni moja, milioni moja katika Wilaya inasaidia nini? Huu MKUKUTA tunautupia wapi? Utatupitia kushoto wengine kwa sababu *NGO* zote za kuweza kupata mikopo ziko Dar es Salaam, ukiwapeleka mikoani hakuna . Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri mshirikiane na Waziri wa Mipango muangalie ni jinsi gani mtawekavyoweza kuweka hii mipango sahihi ambayo wanawake mkishasema tu wafungue *SACCOS* wana uwezo huo? Tunawahamasisha lakini kama hela yetu hii tunayo ambayo mnatupa kukopesha wanawake shilingi hamsini hamsini mkatuambia fungueni *SACCOS* mtatuletea na wafadhili wengine wataingia humu.

Kwa hiyo nilikuwa naomba liangaliwe upya suala zima la kwamba kila mtu afungue, tutafungua *SACCOS* mia lakini uwezekano wa kupata mikopo hakuna zaidi, kwa hiyo, nilikuwa naomba Waziri wa Fedha hebu iangalie hiyo asilimia unayotupa ya milioni moja na pili uangalie asilimia kumi zilizokuwa zinatolewa za wanawake na wanaume za Halmashauri pia ni ndogo kwa sababu mapato si yameshafutwa mengine? Kwa hiyo, naomba waongezewe ile asilimia waliyokuwa wanaitoa, asilimia kumi ya mapato yao na wewe uongeze kidogo mimi nina imani *SACCOS* zitakuwa chini ya Halmashauri na zitakuwa ni nzuri mno kwa kazi nzuri wanazozifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia, kwa mtazamo wa kwamba benki bado hazijafunguliwa ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kumalizika)*

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima naunga mkono asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii na ninaomba kwa niaba ya wananchi wa Ruvuma nitoe pole kwa msiba uliotupata wa Mbunge mwenzetu tunaomba wananchi wake Mungu awape subira na aibariki familia iweze kuwa na uvumilivu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kwa niaba tena ya Mkoa wangu nimpongeze sana Mheshimiwa Jakaya Kikwete, kwa kuteuliwa na Chama cha Mapinduzi kuwa mgombea Urais, nimpongeze pia Mheshimiwa Amani Abeid Karume pia kwa kuteuliwa na Chama cha Mapinduzi kuwa mgombea urais kule Zanzibar na nimpongeze sana Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, naye kwa kuteuliwa na Chama cha Mapinduzi kuwa mgombea mwenza na Makamu wa Rais mtarajiwa. Nafikiri ushindi utakaopatikana kupitia kwa bendera hizo tatu utakuwa ni kiashirio cha mafanikio ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika miaka kumi iliyopita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa heshima na taadhima ninawafagilia sana wagombea wetu pamoja na Wabunge wote ambao tunakwenda kwenye harakati huko kwa niaba ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli mimi ninaanza kwa kusema kwamba Bajeti yetu hii iliyoletwa mbele yetu makadirio ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Mipango sina budi kusema kwamba yanamaliza kipindi hiki kwa kuonyesha kabisa ni jinsi gani Serikali yetu ya Chama Cha Mapinduzi ilivyokuwa na nguvu kubwa ya kufuatilia na kutekeleza mahitaji ya wananchi wa Tanzania kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hali nyingine tungeweza kusema kabisa tunachokifanya hapa ndani ni kuzungumza mambo mawili, matatu, kama ushauri wetu kwa Serikali yetu ili iweze kusonga mbele katika kutoa huduma hizi muhimu kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kuupongeza mpango wa kuhakikisha kwamba nchi yetu ya Tanzania inajiingiza katika biashara na nchi za jirani. Huwezi kushangaa vile vile mtu yeyote hawezi kushangaa Mkoa mmoja ama Mikoa zaidi ya mmoja ikapakana na nchi za jirani kwa mfano nchi ya Kenya imepakana na Mikoa ya Mara, Arusha, Kilimanjaro na Tanga vile vile nafikiri na kwa hali hiyo basi Mikoa hiyo yote ina uwezo wa kufanya mawasiliano na nchi hizo za jirani ama nchi hiyo ya jirani na hivyo kuweza kujiongezea kipato kwa wananchi wake kupitia mahusiano yanayojitosheleza.

Mheshimiwa Spika, mimi nina masikitiko makubwa, Mkoa wa Ruvuma unapakana na nchi ya Malawi na mkoa wa Ruvuma unapakana na nchi ya Msumbiji kupitia Wilaya ya Songea Vijijini kupitia kijiji cha Muhukulu mahali ambapo palishawekwa jiwe la msingi ili paweze kujengwa daraja na hivyo kuwasaidia wananchi

wa Wilaya hiyo kuweza kuwa na mawasiliano ya karibu sana na nchi ya Msumbiji na hivyo kuweza kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, siwezi kukataa mpango wa Serikali wa kujenga daraja katika Mkoa wa Mtwara, daraja litakaloingia kwenye mpango wa *Mtwara Corridor* litakalojulikana kama Daraja la Umoja , lakini hiyo isiwazuie wananchiwa wa Mkoa wa Ruvuma katika kijiji kile cha Muhukulu palipokwisha kuwekwa jiwe la msingi la ujenzi wa daraja katika eneo lile kupatiwa angalau ufumbuzi wa kufungua mawasiliano ya kibiashara kati ya nchi ya Tanzania kupitia mkoa wa Ruvuma kwenda katika nchi ya Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, jiwe lile la msingi lina miaka sasa hivi takriban hata nane lakini hakuna maendeleo yoyote yanayoonekana mahali pale. Inaleta uchungu, mimi nafikiri hata lile jiwe la msingi basi lingeondolewa ili ijulikane moja kwamba kwa mawasiliano na nchi za jirani na nchi ya Msumbiji itakuwa ni Daraja la Umoja tu. Lakini kama Mikoa mingine, mikoa zaidi ya mmoja umeweza kuwekewa mahusiano na nchi za jirani kwa nini basi Serikali isiangalie uwezekano wa kuleta basi hata kiboti kidogo pale kwenye Mto Ruvuma ili wananchi wa Wilaya ya Songea Vijijini wakawasiliana na nchi ya Msumbiji na kufungua maendeleo ya kibiashara na uchumi kupitia Mkoa wetu wa Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, tuko mbali Kusini mwa Tanzania, mipango ya *NGOs* za Kitaifa utakuta za Kimataifa hawataki kuja Mkoa wa Ruvuma kwa sababu bado tuko nyuma. Kwa hiyo, naomba niliseme hilo kwa uchungu na niombe sana Bwana Mipango aone sasa ni wakati muafaka pamoja na Daraja la Umoja lakini kijiji kile cha Muhukulu tuangaliwe na sisi Mkoa wa Ruvuma kupitia Wilaya ya Songea vijijini kupewa mawasiliano na nchi ya Msumbiji.

Mheshimiwa Spika, asilimia 48 ya Pato la Taifa linatokana na kilimo. Asilimia 70 ya ajira ya wananchi wa Tanzania inatokana na kilimo, katika Bajeti ya mwaka huu Wizara ya Fedha katika kitabu cha mpango wa maendeleo, umetenga jumla ya shilingi bilioni 63.5 kwa ajili ya kuboresha shughuli mbalimbali za kilimo. Lakini tumeambiwa katika mpango wa MKUKUTA suala la msingi ni kuwajengea uwezo wananchi wa Tanzania waweze kuboresha hali zao za maisha na kuongeza kipato.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo, Sekta ya Kilimo imewekwa kama ni sekta ya kipaumbele katika suala zima la kuinua hali za jamii na maisha ya Tanzania. Lakini katika sekta hiyo ya kilimo ambayo ndiyo sekta kiongozi, katika kitabu hiki cha mpango wa maendeleo Wizara hiyo imepewa shilingi bilioni 63 tu. Lakini kuna Wizara zilizopewa shilingi bilioni 109, shilingi bilioni 271, shilingi bilioni 153, mimi nafikiri bado tunatakiwa kuangalia upya suala la kuamini kwamba kama asilimia 70 ya Watanzania wanaajiriwa kupitia kwenye kilimo, bado Bajeti ya Wizara ya Kilimo haitoshelezi mahitaji yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika takwimu zilizoletwa na Wizara ya Mipango tumeonyeshwa kwamba miradi ya umwagiliaji maji, imekuwa ikiongezeka mwaka hadi

mwaka na uzalishaji tumeona kwamba mwaka 2003 ilikuwa tani 720, 000 na unaona kwamaba kumekuwa na ongezeko ambalo ukiangalia ongezeko la mwaka 2003/2004 tani zilizoongezeka ni kama 41 tu. Sasa ongezeko hilo ni dogo na nasema ni dogo, mimi nafikiri ni kwa sababu ya fedha inayotengwa kwenye Wizara hii ni kidogo sana, kwa sababu gani.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napitia tena Bajeti hii ya Wizara ya Kilimo, unakuta Sera na Mipango imetengewa shilingi bilioni 12, lakini umwagiliaji umetengewa shilingi bilioni 2. Sasa nikawa nafikiria hiyo sera na mipango unafanya nini? Kwenye Sera na Mipango kuna *Agricultural Sector Programme Support* na *Agricultural Sector Development Programme Support.* Hizo zote mbili ukiangalia hata kwa maneno zinafanana fanana,ni mambo ya *support, support* tu. Lakini ukichukua hiyo ukiilinganisha na bilioni mbili za umwagiliaji ambazo ndiyo zitakazowapa wananchi kipato na kutuingiza kwenye MKUKUTA, ni bilioni 2.

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri kwa *logic* yangu tu ya kawaida, ambayo siyo ya utalaamu huo wa ndani, bado inanipa hofu. Hizo sera na mipango ya kila mwaka, kwa sababu mimi najua tunahuisha ya mwaka uliopita kuja mwaka mpya inaweza kuchukua uzito gani kulinganisha na bilioni 2 ambazo zinatakiwa ziende moja kwa moja kwa wananchi maskini.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba kwamba ninaelewa mipango inabadilika kulingana na wakati. Lakini nadhani pia utendaji wa kuwasaidia wananchi kupambana na umaskini na wenyewe unabadilika kulingana na wakati na wakati huu ni wakati wa MKUKUTA, kwa hiyo, basi fedha nyingi ninafikiri zingepelekwa katika kuwawezesha wananchi kupata pato lao na kujiongezea katika maisha yao ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia mpango wa Ushirika na Masoko, katika kitabu cha maendeleo, hapa ndipo panapolala maendeleo ya wananchi walalahoi. Naipongeza Serikali kwa sababu katika mpango huo wa masoko wameonyesha kabisa kwamba Wizara hiyo itatumia shilingi milioni 511, kwa ajili ya kukuza masoko ya kahawa na pamba. Lakini mimi nilikuwa nafikiri kwamba Wizara hiyo ya Ushirika na Masoko ingeangalia sasa hivi inawezaje kuboresha hata mazao mengine mchanganyiko.

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia kahawa na pamba peke yake tukasahau korosho, ufuta, mahindi na tukasahau na alizeti na mazao mengine yanayofanana na hayo ambayo yangeweza kupata masoko ya maana sana katika nchi za nje na hata nchni mwetu Tanzania, basi nadhani bado katika mpango wa maendeleo wa Wizara hiyo bado hatujafanya kitu kizuri sana, ingawa nawapongeza sana kwa kusimamia vizuri Ushirika na Masoko, lakini nafikiri iko haja ya kurejea. Wakiweza kufanya utaratibu wa masoko mazuri basi tunaweza kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Wizara ya Ushirika na Masoko kuona tunaboreshaji hata zana bora za uzalishaji katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri pamoja na mambo yote aliyosema ya mipango hajazungumzia kuhusu kubadilisha nguvu za wananchi kutoka jembe la mkono kwenda jembe la kukokotwa na ng'ombe ama trekta. Mheshimiwa Mbunge aliyepita amezungumza sana na mimi kila siku huwa nazungumza hilo na leo tena naomba niendelee kusema kama katika mpango wa maendeleo hatujaweke fedha za kununua

majembe ya kukokotwa na wanyama na matrekta kuwasaidia wakulima basi bado uzalishaji huo utaendelea kuwa kidogo.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana juzi alijibu swali langu vizuri sana. Vijiwe vimekuwa vingi vijijini. Vijana wanahangaika kupata ajira, matatizo ni makubwa mno, Kilimo hakiwapi ajira, masoko hakuna, wamekuwa ni vijana wasio na mwenyewe. Lakini niupongeze mkakati wa Serikali, mimi nadhani ifikie wakati sasa tukubali kwamba ni muhimu kuanzisha mkakati maalum na mpango kabambe wa kuwashughulikia vijana katika kupambana na umaskini kupitia katika vijiwe vyao hivyo hivyo ama *clubs* zao za michezo na timu zao za michezo mbalimbali walizoziunda.

Mheshimiwa Spika, vijana bado hawana mwenyewe. Naipongeza sana Wizara kwa sababu inaangalia sana suala laUKIMWI lakini kwenye suala zima la mpango wao wa maendeleo mimi nadhani idara ya vijana inatakiwa kufanya kazi ya ziada.

Mheshimiwa Spika, mimi nakubali mpango mzuri umeanza katika Manispaa ya Temeke, lakini Temeke bado kuna Temeke nyingine ndogo ndogo ziko huko kwenye Halmashaauri zetu zinatakiwa pia nazo ziweze kuangaliwa kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kazi kubwa ya kutengeneza barabara lakini bado nasisitiza barabara za vijijini ziweze kupewa kipaumbele. Tunayo barabara moja inayotoka Wino kwenda Ifinga, ziko barabara nyingine nyingi tu katika maeneo ya vijijini ambazo zinatakiwa zifanyiwe ukarabati na Serikali kwa kweli ikizingatia hilo itasaidia sana na katika Bajeti hii nilikuwa najaribu kuangalia barabara hiyo ya Wino kwenda Ifinga haijazingatiwa kabisa wananchi wanatembea siku mbili wakilala njiani bila kufika eneo ambalo wanaweza kupata usafiri.

Kwa hiyo, kuna wanyama wakali kama simba, mimi nafikiri kwa kweli hawatendewi haki wananchi hao. Naomba sana Wizara ya Ujenzi itupe maelezo ni kwa nini barabara hiyo inasahaulika kila mwaka, kwa nini wananchi wa eneo hilo wana matatizo gani? Nadhani kwa kweli ni wakati muafaka wa kuangalia.

Nampongeza Rais kwa kuwatambua wanawake na nalipongeza sana Bunge lako na Wabunge wote kwa kupitisha asilimia 30 ya wanawake kuingia katika madaraka ya uongozi. Lakini nafikiri bado tunatakiwa kuendelea kuwaelimisha wanaume na wanawake kuhusu umuhimu wa wanawake katika kusaidia na kuiongoza jamii ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho napongeza Serikali kwa kuwalipa watendaji wa Vijiji, Kata, lakini napongeza sana Serikali kwa kuweza kuwalipa wastaafu wetu, wazee wetu. Hiyo itawasaidia kusomesha watoto wao na kuleta maendeleo mbalimbali katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba niwatakie Waheshimiwa Wabunge wote uchaguzi mwema wenye mafanikio, naomba nikutakie na wewe

mwenyewe binafsi uchaguzi mwema na wenye mafanikio lakini naomba niwatakie Watanzania uchaguzi mwema wa amani na wenye mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. PAUL E. NTWINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja hizi mbili ya Waziri Mheshimiwa Basil Mramba na Waziri mwenzake, hoja zao ni nzuri na kwa kweli wanahitimisha na kuonyesha tutakavyoanza tena kwenye awamu nyingine ya Serikali inayokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kutoa pole kwa familia ya Mbunge aliyefariki ndugu yetu Mheshimiwa Abu Kiwanga wa Kilombero namwomba Mwenyezi aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Pia nichukue nafasi hii kuwapa pongeza wanaogombea Urais, kwa kule Zanzibar Mheshimiwa Amani Karume na Tanzania Bara Mheshimiwa Jakaya Kikwete na Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, mgombea mwenza. Bila shaka kama kawaida CCM itapata ushindi wa kishindo na mimi namwomba Mwenyezi Mungu awape nguvu mpaka siku hizo za uchaguzi zitakapofika ili chama chetu kiendelee kutawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hoja za Mawaziri wote wawili zimeonyesha hali nzuri ya Uchumi katika nchi yetu. Nitaongea kwa ujumla jumla. Imeonyesha hali nzuri ya uchumi wetu hii ni kwa sababu tangu Rais alipochagua askari wa miavuli alisema watafanya kazi kwa nguvu na kwa jitihada kubwa ili kuinua uchumi wetu. Katika kazi walizozifanya nawapa pongezi kwa ujumla kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi juu ya ulipaji wa madeni na hasa kwa Jemedari mwenyewe Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kwa kushughulika sana ili tufutiwe madeni. Kama mnafuatilia Wabunge hata juzi wakubwa wamefuta madeni yetu, hii ni pongezi kubwa sana ambayo tunaitoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nafikiri tutajipanga upya juu ya mikopo ambayo tunachukua. Mikopo tunayochukua imefika wakati sasa tuitumie kwa mgao mzuri, kama ni sungura mdogo basi tukatiane hata mkia na manyoya wengine tupate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu kuna maeneo ambayo Wabunge tumesema sana katika hotuba zetu hapa, wengine tumekaa Bungeni miaka kumi sasa, lakini maeneo haya bado hatuoni kama yanasogea mbele. Hata tukishauri inaonekana tunashauri lakini kale kasungura kanaonekana bado ni kidogo. Ninachotaka kusema sasa ni kwamba, kwa wigo ule wa upanuzi wa ukusanyaji wa kodi, kwa wigo huu tunaosamehewa madeni na Wabunge wenzangu wamesema hapa hebu tujaribu sasa kufungua maeneo ambayo bado yamefungwa ambayo tunawalalamikia ambayo nayo yana uzalishaji wa kutosha kabisa ili kuongeza au kukuza Pato la Taifa. Nasema hivyo kwa sababu ukichukua hotuba nyingi ambazo zimetolewa kwa Wabunge hapa kuna barabara ambazo zingejengwa zingeongeza au zingefanya maeneo haya yaweze kuwa na uchumi ulio mzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, bado tunalalamikia barabara za kwenda Kigoma na hata kuna barabara hii ya katikati ya kutoka Mbeya kupitia Chunya kwenda Itigi. Barabara hii kwa bahati nzuri au mbaya ni kwamba Rais mwenyewe alivyokuja awamu ile ya kwanza yaani miaka mitano iliyopita aliahidi kwamba ingejengwa kabla ya yeye kumaliza wakati wake, lakini bila shaka kwa sababu naambiwa kuna uchambuzi yakinifu, sijui kuna michoro imepelekwa kupimwa wapi. Bila shaka baada ya wapimaji kumaliza na pesa pia zitapatikana. Lakini ninachotaka kusema ni kwamba na sisi Ileje na Chunya kule tunataka tupate barabara ambazo ni ngumu, ambazo zinaweza kustahmili wakati wote.

Awamu iliyopita mimi nilibahatika kupata *ki-peace* kidogo, mama hayupo, alikuwa Waziri wakati ule, nilimlilia hapa nikapata kilami kidogo. Ukichukua ile sehemu ya lami iliyotengenezwa haiguswi mara kwa mara kuliko hizi barabara ambazo nyingine natengenezewa karibu kila mwaka kwa sababu hizi barabara ni za udongo, za Uhuru, mimi huwa naziita za Uhuru, kwa sababu wanakwangua, basi.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali kwa kuzitengeneza mara kwa mara lakini kwa kweli umefikia sasa wakati ambao kama tungejenga ile barabara ya Mbeya-Chunya-Makongorosi tungeweza kujenga pia barabara ya Makongorosi-Mkwajuni-Mbalizi-Mbeya ambayo inakuwa kama inazunguka Wilaya ile kwa karibu halafu tukaendeleza kuipeleka Itigi halafu kwa upande mwingine tukaipeleka Gula mpaka Mpanda. Nimelizungumza sana hili, wataalam bado hawajaona eneo hilo kama ni muhimu, lakini naona ni muhimu sana kwa sababu upande wa Mpanda kuna mbuga za wanyama, ukitaka kufika kule lazima uzungukie Sumbawanga. Eneo lilikuwa fupi sana kama ungeweza kupita Mkwajuni-Saza ukaenda kule.

Pia kuna maeneo yale yale ya Gula, Ngwala, Kininga yanalima tumbaku na mwaka jana ilikuwa ni tumbaku nzuri sana yenye *grade* ya juu. Sasa ninachotaka kusema ni kwamba pamoja na kasungura kale nilikokasema mwanzo kuwa ni kadogo sasa tuangalie uboreshaji wa hizi barabara ili ziweze kupitika angalau kwa mwaka mzima. Imekuwa ni matatizo Mbunge unakuja kila Bunge unaulizia barabara hiyo hiyo moja kwa sababu inatengenezwa inaharibika, lakini ukienda maeneo mengine unakuta barabara zinafagiliwa usiku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nilitaka kulisemea ni juu ya uboreshaji wa maisha ya wananchi Vijijini. Naishukuru Serikali yetu kwa kazi nzuri inayofanya, lakini ningeomba pamoja na kwamba, sasa hivi ni soko huria bado maeneo yanatakiwa yasimamiwe angalau kwa mbali tu. Kwa mfano, sasa hii katika Jimbo langu kuna ufuta mwingi sana pamoja na kwamba nimekuwa nikisemea sana pamba, nashukuru uchunguzi unaendelea kule. Lakini sasa bei za mwaka huu za ufuta sijui kule Ileje ni bei gani, maana wale ni wenzangu lakini hizi bei zinakatisha tamaa sana, kwa sababu wameanza debe shilingi elfu sita, wamekuja elfu nane. Sio kwa sababu ni kwamba wana nini, ni tatizo, lakini sisi viongozi tukifuatilia pasipo ngazi ya juu zaidi, mnunuzi mmoja anaweza kwenda ku-*dominate* soko kule akalifanya kama la kwake na wale wanunuzi wadogo ambao anawatuma wakatumia hiyo *privilege* ya kushindwa hiyo bei, ikawa bei wanapanga wao wanavyotaka. Nashukuru kidogo imeanza kupanda na nimeongea na Waziri juu ya hali hii, amesema ataona jinsi atakavyoweza kunisaidia kwa sababu ni

kweli bila kutoa au kupeleka wanunuzi wengi bei itabaki kuwa hiyo hiyo ndogo na itazidi kuwakatisha wananchi tamaa.

Mheshimiwa Spika, katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ukurasa wa 22 na 23 ametoa changamoto zilizo mbele yetu. Ya kwanza, amesema ubunifu zaidi, ari mpya na kasi mpya vinahitajika ili kuongeza kasi ya kukua kwa uchumi. Bila kuwa na msukumo na ubunifu wa kuwapelekea wananchi kule chini bado uchumi tutaendelea kusema tu na tutakuwa tunafuata upande mwingine tunaacha ule upande ambao wananchi wangeweza kuusaidia na kuukuza kwa haraka zaidi.

Ningeomba kama alivyosema yeye hapa, Serikali kwa ujumla iliangalie hili. Halafu pia amesema Bajeti yetu ni tegemezi kwa asilimia arobaini na moja. Kwa kila Mtanzania anayesikia hili kweli linakera na bado tunatakiwa tutoe nguvu zaidi ili tuweze kufikia pale kwa kufanya kazi kwa bidii kwa kuwaelekeza wananchi, kuwasaidia wananchi, bila kuwaachia maeneo tunayosema holela au huria yakaendelea hivyo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kwamba, mauzo ya bidhaa za Tanzania hata kama hili ni soko huria basi tuangalie tutafanya nini. Kuna wakati fulani Wakuu wa Mikoa walikuwa wanasimamia sana *export* na nchi yetu ikawa na hela nyingi sana nje mpaka vita ilipotuharibu kidogo, lakini wakati ule Wakuu wa Mikoa hawa waliweza kufanya kazi na kila mtu Tanzania alikuwa anashughulika. Sasa hivi tunalalamika kuwa watu wengi wapo mitaani, tungejaribu kutafuta njia ya kuwafundisha jinsi ya ku-*export* mazao yetu au vitu mbalimbali kutoka Tanzania viingie kule nako wanakotuletea nyanya, matunda, haya mananasi wakati sisi tunayo mananasi. Bila shaka kwa kufanya hivyo nchi yetu itaweza kupiga hatua.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naishukuru sana Serikali kwa kusaidia sana Jimbo langu kuliweka katika hali nzuri. Jimbo langu ni zuri na Chama cha Mapinduzi ndio limelifanya liwe vile, yapo matatizo ambayo nafikiri Serikali ijayo itaweza kuyatatua matatizo ya maji ambalo ni tatizo kubwa. Unaweza kuwa na bahari lakini huwezi kunywa maji ya bahari maana yana chumvi. Sasa mwananchi wa kawaida anaweza kuchuja maji ya bahari akanywa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana, Serikali ijayo itusaidie katika maeneo yale ambayo tumeyapigia sana kelele.

Mheshimiwa Spika, pia kuhusu Wilaya. Mimi sitaki ku-*argue* au kusema kuwa wenzetu waliopata Wilaya na Mikoa walipendelewa hapana, labda walijenga hoja vinginevyo. Lakini upo ukweli ambao haufichiki kwamba bado tuna Majimbo makubwa, tuna Wilaya kubwa, wengine tumezijenga tayari, lakini bado tunaambiwa tutapewa baadaye sungura ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Bajeti hii mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu katika hoja hizi zote mbili. Hoja ya Waziri wa Fedha na hoja ya Mipango. Lakini kabla sijachangia na mimi nichukue nafasi hii ya kutoa salaam za rambirambi kwa kifo cha Mbunge

mwenzetu Mheshimiwa Abu Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mbunge mwenzetu wa Jimbo la Chalinze na ambaye ni Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuteuliwa kuwa mgombea Urais kupitia Chama Tawala yaani CCM, ndugu yetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. Namtakia ushindi na awe Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini pia nampongeza mgombea mwenza kwa kupata uteuzi huo, nafikiri watasaidiana na tutashinda. Lakini pia nampongeza Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa kuteuliwa kuwa mgombea urais wa Zanzibar kupitia Chama cha Mapinduzi. Wote kwa jumla nawatakia kila la kheri na washinde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, mimi nasema Bajeti ni nzuri, haijawaumiza wananchi na kimsingi inawanufaisha wananchi. Ukitaka kujua mpaka usome, urudie tena ndio utaelewa. Kwa hiyo, mimi moja kwa moja naiunga mkono, sina kigugumizi chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi leo mchango wangu kwa kiasi kikubwa nitajielekeza kwenye maeneo mawili zaidi. Maeneo hayo moja ni barabara hii inayotoka Iringa-Mtera-Dodoma-Kondoa-Babati. Hii ni barabara muhimu kabisa, lakini imesahauliwa sana na Serikali. Lakini eneo la pili, nitazungumzia barabara ya TAMISEMI kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa inayoanzia Mnenia-Masange-Itololo-Kisese-Kikole-Madege ambayo ina kilometa sio chini ya 60. Hayo ndio maeneo mawili ambayo nimechagua kuchangia, sikutaka kueleza maeneo mengi maana Serikali itasahau. Nayazungumzia haya mawili ili yazingatiwe zaidi.

Mheshimiwa Spika, nimetiwa moyo pia na suala la mkakati wa Kitaifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini. Tukiutumia vizuri unaweza kuwa mwarobaini wa kutibu ugonjwa huu wa umaskini Vijijini na Mijini.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo naomba nianze na suala hili la barabara ya Iringa-Mtera-Dodoma-Kondoa-Babati. Ina umuhimu wake kihistoria hata sasa na ina sifa za msingi nyingi tu, lakini mimi nimechagua chache. Ni muhimu kihistoria, ni moja ya ile barabara ambayo inaitwa *The Great North Road* au *C to C* maana yake Cairo mpaka Cape Town, maana yake inarahisisha usafiri na usafirishaji kutoka nje ya nchi hata ndani ya nchi. Kwa mfano, kutoka Zambia-Mbeya-Iringa-Manyara-Arusha-Nairobi na kuendelea. Ni moja ya barabara muhimu sana. Hiyo ni moja ya sifa hizo za msingi za barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, vile vile sifa nyingine, ni kuchochea kukua kwa maendeleo ya kiuchumi inakopita hii barabara. Ni masuala ya msingi sana katika hilo, lakini barabara hii ikiwa ya lami itachochea kuboreka na kukua kwa Makao Makuu Dodoma. Maana zipo dalili Dodoma kama inaanza kusahauliwa sahauliwa hivi. Baba wa Taifa angekuwa hai nafikiri angetukumbusha pia kwamba mmesahau kuendeleza Makao Makuu Dodoma. Kwa hiyo, naomba Mawaziri wahamie Dodoma ili waweze kuendesha Serikali wakiwa hapa Dodoma ndio katikati, bado sifa za katikati ni muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sifa nyingine ni urahisi wa mawasiliano baina ya Dodoma na Arusha yalipo Makao Makuu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Badala ya watu kutoka hapa kwenda Morogoro-Chalinze-Tanga- Moshi ndio Arusha, lakini watatoka hapa wanafika kilometa chache kabisa. Kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie hili. Hili ni la kuangalia tu na kulifanyia kazi. Nina uhakika kabisa pesa zipo nyingi kwani makusanyo ni mazuri, barabara hii naona labda makusudi tu inaachwa, sijui kwa nini.

Kwa hiyo, naomba sana, hiyo ni moja ya sifa lakini mimi nashangaa kwa nini haijajengwa hasa kwa kiwango cha lami. Barabara nyingi zimejengwa, lakini hii inarukwa, zinapewa umuhimu zingine za karibuni tu. Sasa sijui sisi watu wa Dodoma tutafanya nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, naomba nieleze mwaka 2004/2005, barabara hii ninayozungumzia ilikuwa imetengewa shilingi bilioni 2.4 kwa ajili ya upembuzi yakinifu, lakini sijaona kitu ni sifuri tu, *zero* kabisa. Lakini pia na kwa nini hasa kwa kweli tunaipuuza hii barabara, hii ni muhimu sana na napenda kupata maelezo baadaye. Fedha hizo sijui hata zilipelekwa wapi, labda baadaye tupate maelezo, maana nilikuwa nazitafuta hapa kwenye kitabu, hazipo hapa. Kwa hiyo, naomba tupate maelezo ziko wapi na hiyo kazi itaanza lini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005 kwenda mwaka 2006, Serikali kwenye kitabu hiki imesema, imetaja fedha za ndani na za nje zitakazotumika katika kipande kile cha Iringa kuja Dodoma wanasema watatumia milioni mia moja za ndani na za nje milioni mia nane na jumla ni kama milioni mia tisa. Sasa milioni mia tisa kweli tumedhamiria kujenga hii barabara kwa kiwango cha lami. Maana milioni mia tisa ni za kujenga tu barabara ya kawaida iliyoko chini ya Halmashauri. Halafu kipande cha Dodoma-Babati, fedha za ndani wametenga milioni kumi, halafu za nje ndio bilioni moja na milioni mia tisa ishirini na tano. Jumla ni bilioni moja na milioni mia tisa thelathini na tano. Hivi kweli tumedhamiria kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami? Mimi nasema ni kama wanatughiribu ghiribu hivi kutudanganya ili Bajeti hii ipite halafu baadaye washike hamsini zao. Kwa hiyo, naiomba Serikali ilitilie maanani hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema wazi kabisa kwamba ndugu yangu Mheshimiwa John Magufuli ni makini sana kwa kazi, lakini kwa hili la barabara hii sijui kwa nini linampiga chenga. Naomba aelekee na hii barabara ianze kujengwa kabla ya Uchaguzi. Ni moja ya malengo yetu katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Hii ianze kujengwa isiachwe tu hivi hivi. Naomba Serikali ifanye hima.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo naomba sasa nizungumzie barabara ile niliyosema ni ya TAMISEMI, lakini kupitia Halmashauri, fedha zinapita TAMISEMI halafu zinakuja kule Halmashauri, kwa hiyo, ni barabara ya Wilaya. Barabara hii inatoka Mnenia kwenda Masange-Itololo-Kisese-Kikore-Madege ambayo ina kilomita kama sitini na kuendelea. Nayo ni muhimu sana kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, barabara hii ni ya Wilaya iliharibiwa sana na mafuriko ya mwaka 1990 na kukarabati vizuri kunahitaji zaidi ya shilingi milioni mia tisa na

ilifanyiwa upembuzi mwaka 2001/2002, baina ya Halmashauri na TAMISEMI na Serikali Kuu lakini mpaka leo bado haijatengenezwa. Halmashauri haiwezi kwa sababu ni gharama kubwa. Kwa hiyo naomba sana Serikali Kuu iichukue.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kusema kwamba, nilipomwalika Waziri wa Ujenzi kuitembelea barabara hii, alimtuma Naibu Waziri, alikuja na akaitembelea barabara hiyo yote. Aliona uharibifu na ubovu wenyewe na aliona umuhimu wa hiyo barabara lakini pia aliona uchumi uliopo lakini barabara ndio shida. Sasa naomba Serikali sisi Kimkoa tumependekeza ichukuliwe na Serikali Kuu iwe inatengenezwa na *TANROAD* Kimkoa, ni ya muhimu sana kiuchumi. Kwa hiyo, nawasilisha tena pamoja na kwamba Serikali imepitia huko, lakini wamenituma tena nisisitize maana wananchi sasa wanaanza kushindwa kuamini kauli za Serikali kwa sababu hazitekelezwi kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, sasa faida ya barabara hiyo ni kuwa barabara hiyo ina faida nyingi lakini zipo za msingi.

Kwanza, itachochea mkakati huu wa Kitaifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini. Ikitengenezwa wananchi wetu hawa wataibuka kabisa wakifanya kazi za kujenga Taifa na kuimarisha uchumi. Sisi sote tunajua tumelenga kukuza uchumi, uchumi wetu unakua kwa asilimia hiyo 6.7, lakini tunatakiwa tufike angalau asilimia nane na lengo kuu ni asilimia kumi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Tarafa mbili za Bereko na Pahi zinategemea sana barabara hiyo na Kata za Kikore, Kisese, Masange, Mnenia, Bumbuta, Pahi, Kolo zinategemea hiyo barabara na Vijiji vifuatavyo pia vinategemea sana barabara hiyo na nitavitaja kwa sababu ya umuhimu wake: Kijiji cha Madege, Kikore, Mitati, Mkurumusi, Hurui, Atta, Kisese, Madisa, Disa, Mapinduzi, Sauna, Masange, Kandaga, Mkekena, Itololo, Kwayondu, Filimo, Itundwi, Bambare, Mnenia na Vijiji vingine kumi vya Tarafa jirani. Ndio maana ya umuhimu wa barabara hii na ndio maana nataka ichukuliwe na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara hiyo ikiwa imara na ikitengenezwa tutaimarisha kilimo cha umwagiliaji. Katika maeneo yale tuna *scheme* nne, *schemes* za Kikore, Hurui, Kisese na Mnenia. Sasa *scheme* hizi pamoja na kwamba wananchi wanajitahidi lakini kwa sababu hakuna usafiri, mazao hayasafirishwi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninene yafuatayo, mkakati huu wa Kitaifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini unaweza kuwa mwarobaini wa ugonjwa sugu wa umaskini nchini. Kwa hiyo, tunaomba usiwe wimbo tu, lazima tuufanyie kazi kikweli kweli. Lazima usimamiwe kikweli kweli, usijengewe vigugumizi vya kuchelewesha huo mkakati kutekelezwa na tulenge wananchi walio maskini Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja hizi na nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hotuba hizi mbili katika siku hii ya leo.

Nianze kwa kutoa salaam za rambirambi kwa familia ya mwenzetu Mheshimiwa Marehemu Abu Kiwanga, ambaye ametutoka na mimi ni mmoja kati ya watu tuliokuwa karibu naye. Tulikuwa katika Kamati moja ya Uwekezaji na Biashara. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, pili, naomba nitoe salaam za pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wetu wa Mambo ya Nchi za Nje, Mheshimiwa Jakaya Kikwete kwa kuchaguliwa kuwa mgombea pekee katika nafasi ya Urais kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi. Vile vile nimpongeze Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kuwa mgombea mwenza na Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kuchaguliwa kushika nafasi kama hiyo kule Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji pamoja na Waziri wa Fedha kwa hotuba nzuri ambazo wametoa pamoja na Manaibu na watendaji wao wakuu na hivyo niwakumbushe ndugu zangu wa kule Handeni kwamba kazi nzuri imefanyika na ndugu zangu wa kule Rombo kwamba watendaji wao wamefanya kazi nzuri. Ndugu zangu Wasukuma kule anakotoka Mheshimiwa Dr. Festus Limbu pia watambue hilo na ndugu zangu wa Zanzibar watambue hayo. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo naomba sasa nianze kwa kusema mambo yafuatayo, kwanza, hotuba hizi mbili na hasa hotuba hii ya kwanza ya Mipango na Ubinafsishaji inatupa jibu moja kubwa sana ambalo Watanzania tumekuwa tukijiuliza mara kwa mara. Ni kweli Watanzania wanasema na tunasikia na tunakubali kwamba uchumi wa Tanzania unakua, lakini Watanzania wengi pia tunashangaa na wanashangaa sana kwamba ni kwa nini hali ya maisha ya Mtanzania mmoja mmoja licha ya kwamba uchumi wa nchi unakua, hali ya maisha ya Mtanzania mmoja mmoja inazidi kudidimia. Sasa jibu linapatikana kutoka katika taarifa hizi na hotuba hizi mbili. Nitazungumzia mambo manne machache yanayotoa jibu hilo kwa usahihi kabisa.

Mheshimiwa Spika, la kwanza, katika ukurasa wa 20 tunapata taarifa inayoonyesha kwamba kuna nakisi katika urari wa huduma na hii iliongezeka kutoka dola 135 mwaka 2003 hadi dola 83 kuelekea 2004. Kushuka kwa huduma za wananchi kunaonyesha vile vile kwamba kuna matatizo, wananchi hawapati mahitaji yao kikamilifu.

Katika huduma za afya wenzangu wamekwishazungumza hapa na Wilaya ya Muheza ni mojawapo, zaidi ya zahanati kumi na sita zimejengwa, lakini upatikanaji wa watendaji katika zahanati hizo upo katika kiwango cha asilimia isiyozidi 35. Hii ina maana kwamba majengo yamejengwa mengi na mazuri sana lakini huduma bado ni duni.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni nakisi katika urari wa biashara na bidhaa. Hii inapotokea kwamba wewe unauza mauzo nje ya nchi kwa thamani ndogo zaidi kuliko thamani ya bidhaa unazoagiza kutoka nje, maana yake na tafsiri yake ya uhakika ni kwamba wewe unaanza kula mtaji. Hili limetokea na si jambo zuri sana, japokuwa ni lazima litekelezwe.

Mheshimiwa Spika, la tatu, ni kushuka kwa mikopo kwa sekta binafsi. Sekta binafsi ndio sekta tunayoitegemea baada ya Ubinafsishaji na kama mikopo inashuka katika sekta hii maana yake wawekezaji wa ndani hawatakuwa na nafasi ya kuweza kupata mtaji wa kutosha katika uwekezaji. Watakaonufaika ni wawekezaji wa nje ambao wanakuja na mitaji yao kutoka katika mikopo au katika benki zao za nje. Sekta hii ya binafsi kwa Wazalendo kwa hali hii inaonyesha mashaka makubwa sana hasa baada ya utekelezaji wa ubinafsishaji. Lazima hatua muhimu zichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, la nne, ni kasi ya upandaji wa bei za mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa, pamoja na upandaji wa bei za chakula. Bei ya mafuta ya petroli na dizeli inamgusa kila mwananchi. Magari yanayotumika katika usafirishaji ndio yanayokwenda kutoa huduma za usafirishaji wa wananchi (abiria) na mizigo kule Vijijini. Bei ya dizeli ikipanda maana yake gharama hizo zitapanda. Leo nauli inapanda wakati hali ya bei ya chakula cha mwananchi anachozalisha kule inashuka, maana yake nini? Maana yake mwananchi huyu hali yake ya maisha itaendelea kudidimia. Mafuta ya taa yanatumika kila sehemu katika Vijiji na Vitongoji vyetu na hivyo kupanda kwa bei ya mafuta haya basi kunazidi kumkandamiza mwananchi na kufanya hali yake kuwa mbaya zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuuganisha haya manne niliyoyasema na najua yapo mengi zaidi, nimechagua tu haya manne, jawabu ndiyo linapatikana kwamba ukiyachanganya yote hayo basi ni lazima utaona kushuka kwa hali ya maisha ya Mtanzania na hilo ndiyo jibu. Ili Mpango wetu wa MKUKUTA uweze kufanikiwa ni lazima mambo haya manne niliyoyataja pamoja na hayo mengine yafanyiwe kazi kikamilifu vinginevyo MKUKUTA huu tutakutana nao njia panda, hautafanikiwa.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 9 wa Taarifa ya Uwekezaji na Ubinafsishaji inaonyesha kwamba Sekta ya Maji na Madini ukuaji wake umeshuka. Ni vizuri basi katika Sekta ya Madini kwa mfano tukajua ni kwa sababu gani ukuaji wake umeshuka? Je, ni migodi mingapi ambayo imesimamisha shughuli zake au ni migodi mingapi ambayo uzalishaji wake umeshuka? Lakini katika migodi iliyopo, je, ni ipi ambayo uzalishaji wake umeongezeka kwa sababu katika ukurasa wa 14 ipo taarifa inaonyesha kwamba kuna ongezeko la mauzo ya madini nje ya nchi. Kwa hiyo, unaposema ukuaji wa sekta hii umeshuka na wakati huo huo unasema kuna ongezeko la mauzo katika nchi za nje, wananchi wanaweza wakachanganyikiwa kidogo, basi hebu tupate tafsiri yake vizuri na maelezo ya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni Sekta ya hii Maji ni kweli Sekta ya Maji uzalishaji umeshuka tumeona kwa mfano mzuri wa Dar es Salaam hali imekuwa mbaya zaidi kuliko *City Water* walivyopewa Mkataba wa kusaidia kuendesha shughuli za maji

katika Jiji la Dar es Salaam. Tumeona hatua zimechukuliwa *City Water* ameondolewa. Lakini katika maeneo mengi pia kuna hali inayofanana na hii ya Dar es Salaam katika Mji wa Muheza na Miji mingine midogo katika Mkoa wa Tanga, hali ya upatikanaji wa maji imeshuka sana.

Kwa Muheza hii inatokana na kwamba kile chanzo kilichokuwa kinategemewa ni kidogo kuliko kasi ya ukuaji wa Mji wa mdogo wa Muheza. Hapa ni lazima tuiombe Serikali isaidie katika kuboresha vyanzo vya maji katika Miji hii inayokua kwa kasi. Muheza kuna bwawa ambalo tunasema lingeweza likasaidia kuhifadhi maji katika vyanzo vile vya maji vya Mlima wa Magoroto katika kipindi ambacho mvua zinanyesha. Lakini gharama za kujenga bwawa hilo ni kubwa kiasi kwamba Halmashauri peke yake haiwezi kuzimudu. Tunaomba Serikali Kuu ione hilo na isaidiane na Halmashauri katika utekelezaji wake. *(Makofi)*

Lakini la pili, katika Sekta hii ya Maji ninaloliomba kwa Serikali wawasaidie Viongozi Watendaji katika Halmashauri zetu hasa katika Sekta hii ya Maji ili waweze kubuni miradi mizuri na hasa katika Wilaya ya Muheza ambayo imeingizwa katika Mpango wa Dunia wa Maji na Hifadhi ya Mazingira. Watendaji wetu wamekuwa wakilaumiwa sana na kuandikiwa barua nyingi sana za kulalamikiwa na wananchi hivyo wanahitaji msaada kutoka katika Serikali Kuu kuwasaidia.

Jambo lingine muhimu ni katika Sekta ya Umeme na hili nitalizungumzia kwa kirefu kidogo. Katika umeme pia ukuaji umeshuka kinyume kabisa cha matarajio ya wananchi kwamba baada ya kuanzishwa kwa Mradi wa Gesi wa *Songas* matarajio yetu wengi ni kwamba Sekta hii ya Umeme ingeendelea kukua. Lakini taarifa zinaonyesha kwamba Sekta hii inashuka. Uthibitisho wa hilo pia unaonekana katika Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano wa *TANESCO* ambao unaendeshwa hivi sasa, nini *TANESCO* wanachozungumzia katika mpango wao wa miaka mitano. Wanazungumzia kuongezeka kwa gharama kubwa za uzalishaji ambazo zinatokana na mambo yafuatayo:-

Moja, ni kwamba maji ya Mtera hayaaminiki. Lakini la pili, wanasema kwa uhakika kwamba utendaji wa *Songas* ni mbaya Kampuni ile ya gesi wamesema ndani ya ripoti yao na nanukuu kwa kiingereza wanasema: *"Songas bad performance."* Lakini la tatu, wanasema ni kushindwa kwa *Songas* kutekeleza majukumu ya uendeshaji kwa wakati uliopangwa. Lakini lingine ni gharama kubwa za malipo. Kwa mfano, *Songas capacity payment* ni shilingi bilioni 4.5/= kwa mwezi, *Songas energy payment* shilingi bilioni 1,000,000 kwa mwezi, *IPTL capacity payment* shilingi bilioni 3 kwa mwezi. *IPTL energy payment* shilingi bilioni 4 kwa mwezi jumla shilingi bilioni 12.5 kwa mwezi, kwa mwaka ni zaidi ya shilingi bilioni 155 hali hii ni ngumu kiutekeleza. Tunafanya nini kuhusu *Songas?* Mkataba wetu na *Songas* unasema nini? Kama gesi asilia ya Songosongo mwanzoni kabisa kulikuwa na mpango wa kujenga kiwanda cha mbolea, gesi haitumiki kwa kuzalisha umeme peke yake au kwenda viwandani peke yake vipo vitu vingi tu vinavyoweza kuzalishwa kutokana na gesi tunasema nini? Mkataba ule tunauangalia kweli ili uweze kutusaidia! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nawashangaa kwa sababu *TANESCO* wana *shares* kule *Songas, TPDC* pia wana *shares* kule *Songas,* lakini *Songas* wana *very bad performance* hatua gani tunazozichukua. Serikali lazima itusaidie hapo kuweka mambo sawa kule *Songas* ili mradi ule uweze kusaidia wananchi. *(Makofi)*

Jambo lingine la mwisho, ni kasi ya upandaji wa bei kutoka asilimia 3.5 kwa mwaka 2003 hadi asilimia 4.2 tena katika maeneo ambayo ni muhimu sana. Moja, ni chakula, lakini la pili, ni kupanda kwa bei ya petroli na mafuta ya taa. Sasa lazima tuchukue hatua ili Mpango wetu wa MKUKUTA uweze kufanikiwa. Changamoto iliyopo mbele yetu kuhusu suala hilo hasa la upandaji wa bei ya mafuta ni nini?

Kwanza, Serikali iuze *shares* ambazo kwa kweli ni *dormant* zipo, lakini hakuna uzalishaji unaofanya kazi, *share* zetu pale zinafanya nini si tusiondoe, tuziingize mahali pengine zizalishe. Kwa mfano, *TIPER* mpaka sasa hivi haifanyi kazi bado tuna *shares* pale kwa nini tusiziondoe pale tukangoja wakati mwingine muhimu.

Lakini la pili, chini ya mfumo huu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, hebu twende na mapendekezo ya ku-*harmonize* bei ya mafuta kwa nchi zetu zote tatu za Afrika Mashariki, jambo hili litatoa utapeli unaotokana na watu kufanya biashara kinyume cha sheria. *(Makofi)*

Lakini, la tatu, *flow meters* tujitahidi kufunga *flow meters* katika maeneo yote yanakopita mafuta, bado haijafungwa *flow meters* Tanga, bado kule Mwanza na Kagera hakuna *flow meters.* Vinginevyo tu-*declare* Dar es Salaam peke yake kama ndiyo eneo ambalo litakuwa la upitishaji wa mafuta.

Jambo lingine kabla muda haujatoweka niwapongeze ndugu zangu wa *TRA* kwa kazi nzuri ambayo wanafanya kwa makusanyo mazuri. Pamoja na kufutwa kwa kodi *TRA* wamefanya kazi nzuri ya kuweza kuhimili uchumi, mapato yameongezeka na wamesaidia sana katika kupunguza kiwango cha utegemezi. *(Makofi)*

La mwisho, labda niwapongeze Wizara ya Fedha kwa kupunguza kodi kwenye magari ya *Ambulance Health Clinic.* Lakini nilikuwa napendekeza vile vile katika kuhifadhi mazingira tuangalie magari ya usambazaji wa gesi, *LPG* nayo tuyaingize katika mpango huu kama tulivyoingiza hizi *Ambulance Health Clinics.* Lakini vile vile tuangalie uwezo wa kupunguza gharama za *LPG cinders* ili tupunguze kasi ya utumiaji wa kuni na mkaa kulinda mazingira. Jambo hili la mazingira sijaona kama limesemwa mahali pengine popote. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani ni vyema tukaliona hili jambo limechukuliwa hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kupongeza Mpango wa Chakula *National Irrigation Master Plan* na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Chakula pamoja na Naibu Waziri wake Profesa Pius Mbawala, kwa kazi nzuri ambayo kweli wanaifanya na mimi nasema Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala anapokwambia tuonane hapo nje maana yake anataka kuelewa matatizo ya mradi unaozungumzia na akishauelewa kwa uhakika anaufuatilia na unatekelezeka. Amenisaidia sana katika

Miradi ya Umwagiliaji Maji katika Wilaya ya Muheza na hivi ninavyozungumza kazi inaendelea.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kutoa mchango wangu. Lakini naomba pia nianze kwa kutoa pole kwe wenzetu wa Kilombero kwa msiba uliowapata wa Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga ambaye ni jirani yangu kwa hiyo namkumbuka sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa hayo masikitiko yangu kwa niaba ya wananchi wa Masasi, ningependa kuwapongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa sababu ya kuaminiwa na Vyama vyao ili waweze kugombea nafasi hizo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pongezi za dhati kwa Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji kwa kuleta Bajeti ambayo ina *human face.* Kwa kweli ni Bajeti nzuri sana inayofaa sana kwa maskini yeyote yule.

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya kusema hayo, ningeomba sasa nitoe mchango wangu. La kwanza kabisa nataka kusema kwamba Bajeti hii ni ya mwisho kwa Awamu hii ya Tatu na imekuwa ni Bajeti nzuri na mimi naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tatu kwa utekelezaji mzuri wa maamuzi ambayo Bunge hili lilipitisha. Si hivyo tu habari tulizopata leo kwamba Tanzania inasamehewa madeni ni habari nzuri sana kwa nchi yetu na mimi nasema haijawahi kutokea toka Awamu ya Kwanza. Hii inaonyesha wazi umakini na umahiri wa Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Benjamin William Mkapa, pamoja na Baraza lake la Mawaziri pamoja na sisi Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa kweli tumefanya kazi nzuri na kuonyesha Mataifa yote kwamba kazi hiyo tunaiweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati nikitoa pongezi hizi kwa Awamu ya Tatu, naomba nigusie yale ambayo hayakukamilika na ambayo naamini yataendelezwa kwenye Awamu ya Nne. Nataka kujikita kwanza upande wa ujenzi na hasa hasa upande wa ujenzi wa barabara. Wizara ya Ujenzi imefanya kazi nzuri sana ya kufungua nchi na hakuna aliye na wasiwasi kabisa kwamba ndugu yetu Askari wa Miavuli Mheshimiwa John Magufuli, ametekeleza vizuri sana wajibu wake kama Waziri wa Ujenzi. *(Makofi)*

Sasa lakini waswahili wanasema mgema tembo ukimsifia sana basi mwishoni tembo analitia maji. Sasa ndugu yangu Mheshimiwa John Magufuli, hajafikia hatua hiyo, lakini mimi nataka kumshauri tu kwamba dalili zimeanza kuonekana kwamba tembo hili zuri linaanza kidogo kidogo kuwekwa maji sijui na nani, sijui wataalam wake au namna gani. Nataka Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi aiangalie barabara yetu ya Dar es Salaam Kibiti- Lindi. Barabara hii ilianza vizuri lakini sasa kwa mtu yeyote aliyesafiri kutoka Minyogo kwenda Lindi mpaka Nangurukuru ataona ujenzi kwa kweli unakwenda pole pole mno na suala hili mimi nililizungumza katika Mkutano wetu wa 19 sijaona mabadiliko makubwa.

Kwa hiyo, nataka kuieleza Wizara ya Ujenzi kuwa tembo linaanza kutiwa maji. Hebu naomba sana wafuatilie ujenzi wa barabara hii. Namna nyingine yale mafanikio tuliyoyafanya mpaka sasa hivi yataanza kutoweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, hii barabara tuliahidiwa kwamba ingekuwa imekamilika itakapofika mwisho wa mwaka huu. Lakini kwa bahati mbaya hilo limeonekana kwamba halitawezekana, sasa tunasikia kwamba bila shaka katika mwaka 2006/2007. Hii inajionyesha kiuwazi kwamba hali ya ujenzi hasa katika utawala mambo hayaendi vizuri. Leo asubuhi kama mmeona Gazeti la Serikali la *Daily News* nalo limeandika ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hazina ndugu Amin Mcharo ambaye amesema kuna ubadhirifu wa karibu shilingi bilioni 560 katika miradi ya ujenzi wa barabara na humo humo imeorodheshwa sehemu ya Somanga-Matandu- Nangurukuru- Mbwemkulu-Mbemkulu hadi Minyogo katika barabara ya kutoka Dar es Salaam mpaka Lindi sasa hii ni hatari. Inaonyesha kiuwazi kwamba katika mambo ya utawala, mambo hayaendi sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuiomba Wizara Fedha kama imetoa ripoti hii iangalie ni jinsi gani ubadhirifu huu unavyoweza ukakomeshwa na pia itueleze taratibu gani nzuri zaidi zitakazotumika ili kuhakikisha kwamba barabara ile inatengenezwa kwa mujibu wa taratibu tulizojiwekea sisi wenyewe. Inaonyesha kwamba karibu asilimia 80 za mradi hazijatekelezwa na karibu pia asilimia 60 za matumizi ya ziada, karibu kila mradi uliotekelezwa inaonyesha kwamba zinatumika gharama zaidi ya asilimia 60 sasa hii ni hatari. Ndiyo maana nilisema toka mwanzo kwamba jamani kama ni hivyo tuhakikishe kwamba fedha zinazotolewa na kazi inayofanywa pale iwe kwa mujibu kanuni na taratibu tulizojiwekea. Kwa sababu jambo hili siyo ndogo ni kubwa hili.

Mimi ningeomba iundwe Tume ya kukagua na kudhibiti ubadhirifu huu unaojitokeza katika ujenzi wa barabara hii. Ningeomba sana Waziri wa Fedha hebu aangalie sana kwa undani juu ya jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, nataka kuzungumzia upande wa Sekta ya Nishati, mwenzangu Mheshimiwa Herbert Mntangi, aliyemaliza kuzungumza hivi sasa amezungumza vizuri sana na kuonyesha ni mambo gani yanayotokea kule. Sasa mimi nataka kuiuliza Wizara hivi inakuwaje kwa upande wa *Songas* gharama zao za uzalishaji inasemekana ni senti za Marekani 5 mpaka 6 yaani *0.5 to 0.60 U$ production per unit.*

Sasa inakuwaje gesi hiyo hiyo inakuja kuuzwa kwa dola 6 maana yake nini? Na utaratibu gani unatumika, mbona Wizara ya Fedha inaangalia tu? Suala hili kama *production cost* ni kidogo namna hiyo na gharama zinakuwa kubwa namna hii maana yake *Songas* haitokuwa na tofauti na *IPTL.* Tulikuwa tunategemea kwamba *Songas* ndiyo itakayotukomboa.

Lakini sasa hivi gharama hizi zinatudidimiza na mwenzangu aliyemaliza kuongea amesema tunatumia karibu bilioni 12.5 kwa mwezi. Malipo yote haya kwa ajili gani?

Kama tunakwenda namna hii, je, tutaweza kusambaza umeme vijijini na nani ataununua umeme wa aghali namna hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *Mnazi Bay* tumeanza kuchimba hiyo gesi na kutengeneza umeme, lakini mradi unakwenda taratibu na hata wale wenyewe wamesema *production cost* zao ni ndogo. Mradi utakapokamilika na ikiwa utaingizwa katika mkondo wa *TANESCO* kwa vyovyote vile utakuwa wa aghali nao hata sisi kule Kusini tutashindwa.

Sasa mimi naiomba Wizara ya Fedha katika haya mambo ya gesi afadhali tuunde aidha, Mamlaka au Kampuni inayojitegemea itakayoshughulikia umeme wa gesi. Kwa sababu kama *production cost* tunazifahamu ziko chini sasa kwa nini tuingie katika mtindo wa *TANESCO* ambao ni aghali. Tunaomba tuchukue gharama hizi vizuri na kuona jinsi gani mamlaka hiyo inaweza kusambaza umeme vijijini na ndiko waliko watu wengi. *(Makofi)*

Mwisho, nataka kuzungumzia kidogo juu ya kero mbalimbali zilizobaki katika Awamu hii ya Tatu. Kuna kero zilikuwepo za walimu na pensheni hizo bahati nzuri zimeisha. Lakini katika Wizara ya Afya nako kuna kero za watumishi wengi ambao hawajalipwa baada ya kumaliza masomo yao na hasa wapo watumishi wanaitwa *Assistant Medical Officers* ambao huwa wanakwenda kufanya *up grading* ya miaka miwili na wakirudi wanakuwa *Assistant Medical Officers* toka *Clinical Officers.* Maafisa hawa, pamoja na wa Masasi sita hawajarekebishiwa mishahara yao mpaka leo. Hii ni aibu, Wizara ya Fedha ijitahidi kurekebisha kero hii kama walivyofanya katika sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Spika, unaweza kukuta Daktari anafanya operesheni na anafanya kazi nzito lakini mshahara wake ni mdogo kuliko wa *nurse* anayemletea vifaa pale. Kwa hiyo, kero za namna hii katika Wizara yetu ya Afya hebu fanyeni zoezi kama lililofanyika kwa Wizara ya Elimu ili tuhakikishe hao wa Wizara ya Afya wanakuwa katika utaratibu mzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naomba kusema kwamba Bajeti hii ni nzuri na katika uzuri wake tusiache inachafuliwa na mambo madogo madogo au kero zisizo na sababu madeni tumesamehewa na kama bado yataisha na sungura aliyekuwa mdogo sasa ni tembo siyo sungura. Kwa hiyo, tutagawana kitu kikubwa. Kwa hiyo, mipango yetu ni lazima iwe mikubwa na tuhakikishe tunagawana vizuri ili tuondoe shida zote tulizonazo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mpaka hapo tumefikia mwisho wa kipindi cha asubuhi. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Spika bado yuko safarini kipindi cha jioni kitaongozwa na Mwenyekiti, Mheshimiwa Anne Makinda. Sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 Jioni.

*(Saa 06.52 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nikushukuru sana kwa nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika Bajeti ya Serikalli ya mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa mchango wangu ningependa nitoe rambirambi zangu za dhati kabisa kwa kifo cha rafiki yangu, jirani yangu alikuwa anakaa hapa hapa Mheshimiwa Marehemu Abu Towagale Kiwanga na nimwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii nitoe pongezi zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mbunge, kwa kuteuliwa kuwa mgombea wa Urais kwa tiketi ya Chama cha Mapinduzi (CCM). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti hii ambayo tunaijadili leo ukitaka ujue uzuri wake inakubidi uisome pamoja na Bajeti iliyosomwa hapa mwezi Juni, 2003 na nyingine iliyosomwa mwezi Juni, 2004. Ukizichanganya na hii ya leo utaelewa kwamba Serikali imekuwa inajenga uchumi *very systematically* na kwa kweli Bajeti hii ya sasa ni kifuatilio kizuri sana kwa Bajeti hizo ambazo zimepita. Kwa sababu hii nichukue fursa hii niishukuru Serikali na niwashukuru hasa walio na dhamana ya Mipango na Fedha katika Serikali yetu Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda. Wanastahili sifa kubwa sana, hongereni sana. *(Makofi)*

Pia napenda niwapongeze Manaibu Waziri na Makatibu Wakuu watatu, wawili wa Hazina na mmoja wa Mipango kwa kazi nzuri ambayo mmefanya kuongoza Wizara zenu na kutuletea Bajeti hizi ambazo zimetuvusha. Mtaona kweli tumevuka. Tangu siku ya Jumamosi vyombo vya habari vya Kimataifa vimekuwa vinaongea juu ya kazi nzuri inayofanywa Tanzania na tumefutiwa madeni yote. Haijawahi kutokea.

**WABUNGE FULANI:** Haijapata !!!!! *(Makofi)*

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo nitoe pongezi za pekee kwa Rais wetu mpendwa Benjamin William Mkapa. Amesimamia marekebisho ya uchumi mpaka tukafika sehemu ya kwanza tukafutiwa sehemu ya madeni yetu na sasa tumefika mahali hata wakubwa wanafuta madeni yote. Tumshukuru sana na tumuombee Mwenyezi Mungu ampe maisha marefu ndicho tunachoweza kusema sasa. *(Makofi)*

Kwa sababu Bajeti yenyewe nzuri sana mimi sitaiongelea kama Bajeti. Nataka nijihusishe na nini hasa tufanye, tumefutiwa madeni. Tufanye nini sasa na mapesa haya ambayo tumefutiwa hatutalipa, hii ndiyo nataka kusema. Kwa kweli hiki kitu kingechukua saa nzima kukielezea vizuri, lakini nitaeleza kitu kimoja tu. Nitaeleza tufanye nini kwenye sekta ya elimu, ile sekta ya kuondoa ujinga. Ningependa nipate

nafasi pia niongee juu ya sekta ya kuondoa umaskini na sekta ya maradhi. Lakini leo nitajikita kwenye sekta ya kuondoa ujinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu tulivyokuwa tunaingia Januari tulipeleka Sekondari tukaandikisha watoto asilimia 35 ya watoto wetu wote waliomaliza darasa la saba. Lakini Kitaifa watoto ambao walikuwa wamemaliza elimu ya msingi, watoto waliofaulu walikuwa 55 kwa mia. Kwa maana tumeacha nyumbani kama asilimia 20 ya watoto ambao walistahili waende Sekondari lakini hawakwenda kwa sababu hatuna madarasa wala shule na hatuna uwezo wa kuwasomesha. Sasa tulipofutiwa madeni wakati ni huu. Wananchi nchini kote wanajenga shule za kutwa katika Kata zao na kazi hii ni ngumu kweli kweli. Mpango wa kupanua na kuboresha Elimu ya Sekondari (MMES) fedha zake kidogo sana. Hazitoshelezi mahitaji halisi. Kwa hiyo, tutumie fedha hizi ambazo tumezipata tuwasaidie wananchi tukamilishe shule wanazojenga. Vile vile tujenge mahali ambapo wananchi hawajajenga kwa kiwango kinachostahili Shule za Sekondari.

Pia tuchukue hatua tusomeshe walimu, tujenge maabara, tuwape vifaa na mabwalo, tuwapelekee vitabu na zaidi ya hapo tujenge shule ambazo zitawapa watoto elimu ya kidato cha tano na cha sita katika kila Wilaya ya Tanzania. Hii itawapunguzia wazazi gharama kubwa wanazochukua sasa kupeleka watoto mbali na nyumbani kwao. Pili, tumepeleka kweli, tumeandikisha shuleni asilimia 35 za watoto. Lakini ukienda shule asilimia 35 haipo. Watoto walioko shule ni chini ya asilimia 20, kwa sababu gani? Pamoja na Serikali kutusikia kilio chetu tangu mwaka 2001, 2002, 2003 mwaka jana ilipunguza ada ya elimu ya Sekondari kutoka shilingi 40,000/= mpaka shilingi 20,000/= na ikaondoa michango ya majengo, madawati na mitihani ya shule. Lakini bado kiwango kilichobaki katika Shule za Sekondari cha asilimia 20; shilingi 20,000/= ni kikubwa sana kwa Watanzania wengi wanaokaa Vijijini. Hivyo watoto wengi waliofaulu (hawa 35 wakachaguliwa kwenda Sekondari) bado wamebaki nyumbani na kikwazo chao ni ada.

Sasa tumefutiwa madeni, tufute ada zote za Shule za Sekondari. Tufute ada. Hiki ni kikwazo kikubwa kwa watoto maskini kwenda shule. Tumbakizie mzazi jukumu la kumshonea mtoto wake nguo, kumpa chakula, eeh basi. Mambo mengine yachukuliwe na Serikali kutokana na fedha hizi ambazo tunapata kwa kufutiwa madeni. *(Makofi)*

Kuna kikwazo kingine cha watoto maskini. Hii ni ada ya mitihani wanapofika kidato cha pili, cha nne na cha sita. Wengi wanafanya mitihani lakini hawawezi kupata vyeti vyao kwa hivi hawajui wamefaulu kitu gani. Sasa vikwazo hivi vyote tuvifute. Serikali ichukue jukumu, ilipie. Watoto maskini waweze kupata vyetu vyao wakimaliza shule. Unaposikiliza nikisema namna hii, suala linalofuata ni halafu wakimaliza waende wapi? Wakimaliza waende Vyuo Vikuu. Tupanue Elimu ya Juu ili watoto wakitoka huko Sekondari waende kwenye Elimu ya Juu.

Nchi yetu imekuwa nyuma sana katika suala la elimu ya juu. Watoto wote walioko katika elimu ya juu katika nchi yetu hawafikii wale walioko *Makerere University*. *Makerere University* ina watoto wengi kuliko watoto wetu wote walioko Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo cha Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha

Sokoine, cha Tumaini cha Wakatoliki kule Nyegezi na vyuo vingine vyote hapa nchini ukichanganya bado ni wachache kuliko watoto wa Uganda walioko *Makerere University.*

Kwa hiyo, tunahitaji tuchukue hatua kali kabisa tupanue Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Chuo Kikuu cha Mzumbe na Chuo Kikuu cha Zanzibar. Tuwajengee madarasa, maabara, maktaba na tujenge mabweni watoto wakae huko na tuache mtindo wa watoto wetu wa Chuo Kikuu kula kwa mama ntilie. Kula mitaani, ustaarabu wa elimu ya juu unapotezwa na mambo ya kula chakula kwa mama ntilie. Tutengeneze zile *cafeteria* za zamani, watoto waende Chuo Kikuu na wasome kweli kweli. Kwa sababu sasa hatuna kisingizio tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuvipanua Vyuo vyenyewe haitoshi. Ni lazima tufungue na vyuo vikuu vipya. Mimi nakumbuka kabisa nilipokuwa Profesa kwenye Chuo Kikuu cha Sokoine, *draft* ya sheria ya Chuo Kikuu cha Dodoma ilikuwa tayari, tufungue Chuo Kikuu cha Dodoma. Chimwaga ni sehemu nzuri sana ya kuanzia Chuo Kiku cha Dodoma. Jumba kubwa lile linakaa bure huku watoto wanakaa nyumbani. Tufungue Chuo Kikuu Mbeya. Chuo Kikuu cha Mbeya sheria yake ilikuwa tayari lakini mpaka sasa bado. Tufungue Chuo Kikuu Mtwara. Kama wakati ule Mwalimu akianza aliweza kujenga Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinatushinda nini sisi na madeni tumefutiwa. Kwa hiyo, twende tubadilishe na vyuo vingine ambavyo *terms of reference* zake si nzuri. Kwa mfano kama *IFM why can't it be a University* ifundishe vitu vyote ambavyo vinafundishwa sasa halafu iwe Chuo Kikuu. Kwa sababu gani tunaacha chuo kile kinapotea bure? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuchukue fursa hii ya kufutiwa madeni tuvisaidie Vyuo Vikuu hivi vya watu binafsi ambavyo mchango wake ni mkubwa sana katika kutoa Elimu ya Juu hapa nchini kwetu. Tuvisaidie Vyuo Vikuu vya Tumaini, kule Nyegezi na Bugando, Chuo Kikuu cha Waislam hiki wanataka kuanzisha, Chuo Kikuu cha Bukoba na *Herbert Kairuki University.* Natumaini ni kengele ya kwanza?

**WABUNGE FULANI:** Naam !!!!!

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Kwa sababu mambo bado yapo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukue hili liwe jukumu letu. Katika nchi zote zilizoendelea Vyuo Vikuu vya Binafsi vinatoa mchango mkubwa sana katika elimu na utafiti katika nchi zao na kwa sababu hiyo, jamii inakuwa na wajibu wa kuvisaidia. Zaidi ya hapo ni vyema sasa tukaujenga na kuimarisha Mamlaka ya Elimu Tanzania *(Tanzania Education Authority).* Wakati tulipopitisha Sheria ya Mamlaka hii tulisema Mamlaka hii itakuwa chombo kikubwa na kichocheo cha kusaidia vifaa vya kufundishia na vifaa vya utafiti katika Vyuo Vikuu. Tukasema bajeti yake isiwe chini ya asilimia 2 ya Bajeti ya Taifa. Sasa kumekuwa na *interpretation* mbalimbali. Lakini *to the best of my understanding, that was the decision we made.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati umefika sasa tumefutiwa madeni basi tutumie sehemu ya afueni hii tuliyopata kuimarisha Mamlaka hii ili iweze kutekeleza wajibu

wake barabara. Pili, Bodi ya Mikopo ambayo tumepitisha hapa iwezeshwe ianze kazi yake mara moja ili iweze kuwakopesha watoto wanaokwenda kwenye Vyuo Vikuu. Kwa njia hii watoto wengi ambao wamepata sifa za kuweza kuingia kwenye Vyuo Vikuu basi wataweza kwenda. Ilivyo sasa chini ya asilimia moja ya watoto wetu ndiyo wanaweza kwenda Vyuo Vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefanya *precision* ya hali ya juu sana kuweza kueleza mambo haya. Kwa hiyo, nimepata dakika moja niseme mambo mengine. Suala moja ambalo kwa kuwa tumefutiwa madeni tungelifikiria ni kutafuta nishati ambayo ni rahisi. Tujikomboe na umeme ambao ni ghali sana. Hatua ya kwanza tungechukua tuinunue hii kitu inayoitwa *IPTL, this is a very expensive animal.* Tuinunue na tumwambie huyu bwana aondoke halafu tutumie fedha zetu tuzalishe umeme wa makaa ya mawe ya Mchuchuma. Tuchukue hatua ya dhati kabisa tufunge *Stigler's Gorge,* tuzalishe umeme wa kutosha. Hii itatuwezesha kuwa na msingi mzuri wa kuendeleza viwanda na sekta zingine hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabisa tuangalie maeneo ya kilimo yanayoweza kuondoa umaskini hapa nchini. Na maeneo haya yapo. Kuzalisha mbegu bora sasa hivi tunahitaji tani 32,000 za mbegu bora hapa nchini. Na zinazalishwa hapa nchini tani 2,000 peke yake. Kwa hiyo, tunahitaji na tunaleta kutoka huko nje tani 30,000 kwa mapesa mengi sana, vitu ambavyo tunaweza kuzalisha wenyewe hapa nchini. Tuwawezeshe wananchi wetu wazalishe mbegu *on farm,* wazalishe mbegu kwenye mashamba yao *on farm seeds production* hii ni njia rahisi sana ya kuzalisha mbegu bora lakini unazalisha nyumbani kwa mkulima. Tuwekeze katika kuzipa nguvu Taasisi zetu za Utafiti wa Kilimo na Taasisi zetu za Ugani wa Kilimo na zisimamiwe vizuri kweli zipeleke ushauri kwa mkulima tuongeze nguvu kwenye umwagiliaji na tuongeze nguvu kutafuta masoko ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiingii kwenye akili ya Mtanzania kwamba wananchi wa Uganda wanatoka Kampala wanakuja Singida wananunua vitunguu, wana-*package* na wanaita *produce of Uganda* na wanauza Ulaya. Sisi tuko hapa hapa. Haingii akilini hata kidogo. Kwa hivi tuongeze nguvu zetu katika kutafuta masoko maana mazao yetu sio ovyo, mazao yetu ni mazuri sana. Lakini wenzetu wanakuja wanabeba wanachukua. Wakenya wanatoa malori kuanzia Nairobi mpaka Iringa wanachukua viazi wanapeleka wanauza *as produce of Kenya.* Hiyo inataka hotuba tofauti. *(Makofi.Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie na nitoe mawazo yangu kuhusiana na Mipango pia na Bajeti yetu iliyo mbele yetu.

Kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Jakaya Kikwete, Waziri wetu wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa kuteuliwa kuwa mgombea Urais. Pia nimpe pongezi hizo hizo Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Rais wa Zanzibar na Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kama mgombea mwenza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa masikitiko makubwa nitoe pole kwa watu wa Jimbo la Kilombero kwa kufiwa na Mbunge wao Mheshimiwa Abu Kiwanga na Mungu aiweke mahali pema roho yake. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbele yetu kuna hizi hoja mbili, hoja ya Mipango na hoja ya Bajeti yetu ya mwaka 2005. Katika taarifa nzima ya mpango uliotolewa na Wizara kuhusiana na mwelekeo wa Uchumi tunakwenda namna gani imetoa viwango, takwimu ziko wazi kwamba tutakuwa kwa kiasi cha asilimia 6.7 tukitoa kwenye asilimia 6.4 imetoa kiwango cha mfumuko wa bei pia imetoa na mwelekeo mzima wa utaratibu wa kuendesha uchumi.

Sasa katika hili nimeona katika ukurasa 17 inazungumzia namna gani tunaendesha biashara yetu ya nje. Tunanunua zaidi, tunauza kidogo. Sasa katika takwimu hizi na mwelekeo tulionao ambao umetolewa na Wizara ningeomba wakati Waziri anatoa majibu ajaribu kutuweka sawa tu hapa kwamba kama tuna mwelekeo wa kukua uchumi maana yake tutaongeza mazao ya viwanda, kilimo, je, hali hiyo itatuwezesha kuuza nje kwa wingi, biashara yetu nje itapanda, biashara yetu ndani itakuwa namna gani. Ningependa atupatie maelezo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ningependa kuzungumzia suala la viwango na malengo ambayo Wizara ilipashwa iyatoe ili kwamba tuweze kujiweka sawa. Ijaribu kutueleza kwamba tumepanga mwaka huu wa Bajeti au wa mpango huu tungependa tuweze kulima ekari kadhaa za mazao ya chakula na ekari kadhaa za mazao ya biashara. Viwanda vitazalisha kiasi gani, mipango hiyo ningeomba itolewe ili iweze kupelekwa kwenye Wizara zote na kila Wizara iweze kujenga bajeti zao kutokana na hiyo. Hii ningependa Waziri wakati anatoa maelezo pia ajaribu kutueleza ili tuweze kupata mwanga zaidi.

Lakini cha mwisho ni suala la deni la Taifa. Ukurasa wa 17 unaeleza kwa kirefu kuhusiana na deni la Taifa. Limekuwa kutoka mwaka jana na mwaka huu limekuwa zaidi na maelekezo ambayo yanazungumzwa kuhusiana na msamaha ambao umetolewa ningemwomba Waziri wakati anatoa hoja yake na kujibu hayo atueleze vizuri atufafanulie tuweze kuelewa tuko wapi maana yake deni lina mambo mengi pamoja na riba ndani yake, je tunakwendaje na hili ili tujiweke sawa tunavyokwenda na Bajeti yetu mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana hotuba iliyosomwa na Waziri wa Fedha, nampongeza sana. Nawapongeza wote kwa pamoja na pia nashukuru kwamba wakati wote imeelekea kwamba tulikuwa tukipanda. Mwaka jana tulikuwa na asilimia 13.8 ya Pato la Taifa. Mwaka huu tunazungumzia asilimia 14.3 ya Pato la Taifa. Katika wingi wa fedha mwaka jana tulikuwa na trilioni 2.67 mwaka huu tunazungumzia trilioni 4.17. Ndiyo kusema tumepata zaidi na sasa hili pato la ziada. Nafahamu kuna sehemu ambayo itakwenda na kupotea ndani ya *exchange rate,* lakini pia kuna sehemu ambayo itakwenda na kupotea kwenye mabadiliko ya bei haya kwa sababu mfuko wa simenti mwaka jana sio sawa na mwaka huu. Sasa kwenye ile tofauti ambayo naiangalia hapa

ambayo inakuja karibu trilioni 1.5 ya pato la mwaka huu. Nilikuwa wakati unajenga bajeti hii naomba tuielekeze katika maeneo mawili ambayo mimi naona ni ya msingi upande wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili suala la elimu ambalo limezungumziwa na wenzangu wengi. Sehemu zote wamelizungumzia kwenye maeneo na matatizo ya ujenzi wa shule na pia ni kwamba sasa msisimko ni mkubwa wa elimu kwenda juu. Mimi katika Wilaya yangu ambako natoka katika Jiji la Mwanza pia tuna juhudi hizi hizi za kujenga shule. Lakini ukiangalia tulichofanya mpaka sasa kinahitaji nguvu kubwa ya Serikali. Ndiyo maana najaribu kusema kama mwelekeo huu wa mapato ya mwaka huu sehemu kubwa ingeelekezwa katika ujenzi wa Shule za Sekondari. Nyingi ambazo tumezijenga za kutwa katika kila Kata sana sana tumejenga vyumba viwili vya madarasa. Madawati, lakini papo hapo kuna nguvu kubwa ya wananchi imeingia humo na tangu tumalize mwisho wa mwaka jana ujenzi karibu maeneo yote umesimama sasa na hatujui tufanye nini kutoka pale sasa. Lakini kikubwa ni kwamba napenda tu niseme kwamba katika hali hii nilikuwa naomba sana Waziri wa fedha ajaribu kumpatia Waziri wa Elimu fedha za kuweza kutusaidia tuendeleze ujenzi huu vizuri ikiwezekana tuukamilishe.

Mimi nikiangalia katika Wilaya yangu kuna Kata nyingi kwa mfano ya Isamilo, Bugani, Mahina, Mkuyuni, Butimba kote wamejenga shule sawa lakini ndiyo hayo madarasa mawili mawili hakuna majengo ya kutosha ya utawala, maabara, mabwalo yaani *just like that.* Sasa picha inanitia wasi wasi na Januari tunafungua shule na tunaandikisha wanafunzi wapya, kwa hiyo, inatubidi katika kipindi hiki mpaka Januari tuweze kuwa tumejenga madarasa ya kuweza kuwahamisha hawa waliomaliza na wengine ambao wanaingia picha ambayo kwa kweli mimi sasa inanitia wasiwasi. Nikiangalia maandalizi katika maeneo mengine kwa mfano Kata ya Igoma wameandaa shule kwa nguvu za wananchi kwa kiwango kikubwa sana na wameezeka kwa nguvu zao wenyewe lakini hawakupata ruzuku ya Serikali kabisa. Sijui kama wangeweza kupatiwa mara mbili mwaka huu?

Pili, Kata ya Buhongo wamejitahidi sana pamoja na msisimko ambao tumewapelekea kule. Wamejitahidi wamejaribu na hali inakwenda vizuri mbele. Sasa katika mgao huu hoja ni kwamba ningemwomba Waziri wakati anaweka mipango yake sawa sawa ajaribu kuona sasa suala hili tulibadilishe namna gani ili kwamba tukamilishe shule hizi kwa sababu Shule ya Sekondari ni *institution* kubwa sana. Kwa mwendo wa 14 milioni hatuwezi kwenda. Mwaka huu naomba Serikali ishiriki kwa nguvu zaidi kwa sababu tuna uwezo zaidi hapo na hii itatusaidia sana kuweza kubadili elimu kwa sababu hali ya elimu katika maeneo yetu ni mbaya na mimi siridhiki kwa eneo la Wilaya ambayo natoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho ningependa katika mwelekeo huu huu ningemwomba Waziri kwa kweli suala la kilimo ni suala ambalo lazima tulizungumze kwa pamoja kwa kuelewana. Ni la msingi sana kwa sababu *population* kubwa ipo kule na kama tutaweza kuweka nguvu kwenye kilimo na kilimo kiweze kumwagiliwa na kiweze kupata vitendea kazi kama *machinery* nina imani kabisa *population* ile *percent* kubwa ya wananchi tutaingiza katika kushiriki mambo ya uchumi.

Kama itafanyika hivyo Pato la Taifa litabadilika. *GDP* itakuwa mara nne au tano na Waziri wa Fedha atakuwa na nafasi kubwa ya kupanga Bajeti yake nzuri zaidi sio kuzungumzia tena trilioni 4 itakuwa trilioni milioni 10 na kitu. Atakuwa anazungumzia asilimia kubwa ya pato la taifa limeingia katika uchumi.

Mimi ningeomba katika hili mwelekeo uwe huo na Wizara iangalie kwa makini tufanye nini ili kwa makusudi tuinue kilimo ili tuingize wananchi wetu katika shughuli hizi kwa wingi na kila mmoja aweze kushiriki katika shughuli za uchumi katika nchi yetu. Tunachofanya sasa ni wafanyakazi, wafanyabiashara kidogo sehemu kubwa ya wakulima inabaki bila ya kushiriki sawa sawa katika mambo ya kilimo. Jambo ambalo kwa kweli lazima tukubali kwamba inaturudisha nyuma na tukubali kwamba tunapashwa kulibadilisha ili tuweze kwenda mbele sawa sawa na wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa tu kusema kwamba pamoja na uzoefu ambao tunao, wote tunao uzoefu. Tumejenga madarasa ya MMEM tunajua tulivyoyajenga sasa tunajenga madarasa ya MMES kwa ajili ya Shule za Sekondari lakini ubora wake lazima kila mtu anaujua kwamba hatuufikii sawa sawa. Madarasa mengi sasa sakafu zinaanza kuvunjika. Tutumie njia gani ili kuweza kusimamia kazi hizi ziweze kuwa bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyofanya kazi kwenye ukusanyaji wa mapato kupitia *TRA* kwa nini tusiwe na chombo kingine maalum wakati fedha ziko mkononi ziweze kusimamiwa ziende kwenye *institution* yenyewe bila kuchelewa na ziweze kuleta matokeo mazuri na matunda mazuri kwa wananchi wetu. Hili naomba najaribu Wizara iangalie utaratibu wa matumizi na usimamizi wake wa matumizi ili tuweze kufaidika na haya na wananchi wetu waweze kufaidika na fedha ambazo wanaziletwa ndani ya Serikali kwa kulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine naomba nizungumzie suala la utaratibu wa kusafirisha mizigo kutoka Dodoma kwenda Mwanza kwa treni. Mizigo ya Mwanza haipakiliwi Dar es Salaam tena inapakiliwa Dodoma. Kutoka Dar es Salaam inaletwa kwa magari mpaka Dodoma. Hiyo hali imetuletea matatizo makubwa sisi Mwanza kule ya kupanda bei ya vitu kwa hali ya juu sana. Gharama ya kusafirisha mizigo kwenye lori kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma na treni ni tofauti ya treni iko chini kidogo. Pia kuna suala hapa la kubadilisha mizigo kuhamisha kwenye malori kupakia kwenye mabehewa. Hali hii inatufanya sisi watu wa Mwanza tunaumia. Kwa mfano, sasa kilo ya sukari Mwanza iko zaidi ya shilingi 1,200/=.

Mfuko mmoja wa *saruji* uko zaidi ya Sh.2,000/= na kitu na ukiuhamisha kwenda Ukerewe unafika Sh.13,000/= au Sh.14,000/=. Kagera ni hali mbaya zaidi, sasa tunajua kabisa kwa uwazi kwamba reli tunayo na angalau mapato yanapatikana, kwanini Waziri wa Fedha asimpe huyu Waziri wa Mawasiliano akarekebisha reli? Matumizi mabaya ya mali, treni ipo tunaiacha halafu tunaumiza wananchi kule. Wananchi wa Mwanza wanalalamika sana! Halafu kitu kingine kibovu cha wazi ni kwamba barabara ambazo zimejengwa kwa mfano ya Dar es Salaam - Morogoro kuja Dodoma, tumeijenga

kwa mategemeo kwamba tutakaa nayo miaka mitano, kumi au ishirini mbele, lakini kwa matumizi ya magari mazito haya, sasa inaweza ikabomoka mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tutakuwa tunafanya nini kwenye mipango yetu? Ningeomba Waziri wa Fedha leo atamke kwamba ile taratibu ya kupakilia hapa mizigo isimame kuanzia leo. Hii itatusaidia sana kuwasaidia watu wa Mwanza na watampongeza sana kwa sababu wana matatizo makubwa na hali ya kule ni mbaya na inaletwa na utaratibu mbaya tu ambao wanauona kwamba sio lazima twende hivyo.

Kigoma nao wanasema na hali ni mbaya zaidi. Lakini chanzo kikubwa ni hiki! Wizi, mizigo mingine inapotelea hapa, wafanyabiashara wanapoteza mizigo yao. Mwanza tulikuwa na *Super Market,* kwa kweli namshukuru sana Mfanyabiashara wa Mwanza Jumanne Kishimba, alikuwa na taratibu nzuri za kutusaidia bei ambazo ni halali na ndiko tulikokuwa tunakimbilia wakati mwingine sisi wote watu wa Mwanza.

Mheshimwa Mwenyekiti, Sasa hali ya pale na yeye hawezi kufanya lolote kwa hali ya hapa, inabidi alipe hizi gharama na yeye, hata kwake sasa utakuta pia bei ziko juu, hatuna pa kukimbilia sasa. Mimi ningeomba Serikali ichukuwe hili jambo kwa nguvu zake zote ili tuweze kuondokana na tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa heshima kubwa, naomba niseme kwamba nashukuru sana Serikali kwa kuweka kwenye Bajeti yake fungu la kwanza kuwalipa hawa Wastaafu wa *East Africa Community,* hiyo nashukuru sana. Mwanza pale ni Mjini, ukipita, wako hapo watu wengi wananiuliza maswali mengi sana na hata sasa nina barua zao hapa. Nilikuwa niongee na Mheshimiwa Mramba tuzungumze, sasa nimeziweka kwa sababu ameshatoa jibu. Lakini ninachoomba ni kwamba, baada ya Bajeti hii kupita, waanze kulipwa mara moja hao, nao watafurahi kuona kwamba Serikali sasa imeanza kulielewa hili na Serikali itajisafisha maana yake hizi pesa Serikali imekaanazo muda mrefu. Ilipaswa kuwa imewalipa miaka mingi kule nyuma jambo ambalo nasema kwamba Bunge lako Tukufu litoe msimamo juu ya jambo hili sasa na hawa wananchi nao ni binadamu, wana haki, sasa unawanyima kwa nini? Kwa nini wananyimwa mapato yao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo nashukurru sana kwa kunipa nafasi hii, lakini ningependa kuunga mkono hoja baada ya kupata majibu haya, kwa sababu nina wasiwasi sana. Hii hali ya treni hapa inanitia wasiwasi mimi na wenzangu kule watajisikia vibaya wakisikia kwamba ninaunga mkono na hali iko namna hii. Lakini majibu yatakapotoka na mimi nitaunga mkono. Nashukuru sana ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie hoja iliyoko mbele yetu, hoja za Mawaziri wawili, ya Waziri Ofisi ya Rais Mipango, Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda - Mbunge, hotuba ya Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, kwa Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshatoa rambirambi wakati nilipokuwa nachangia Muswada wa Sheria na vile vile nishapongeza wanaostahili kupongezwa kwenye hotuba niliyoitoa juzi tu. Kwa hiyo, nadhani kumbukumbu ipo kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takriban fedha zinazoombwa mwaka huu ni trilioni nne. Ni fedha nyingi sana kwa kweli kwa maendeleo ya Taifa hili na nimeona kuna mpango wa MKUKUTA, kwa hiyo, ndiyo maana Mheshimiwa Basil Mramba haya mambo yanayozungumzwa hapa na Waheshimiwa Wabunge ni masumbwi tofauti na masumbwi uliyopata mwaka jana. Haya masumbwi unayopata mwaka huu yamevaliwa *groves* wala hayaumizi sana, ni masumbwi ambayo ni mepesi tu wanaeleza majukumu ya mapungufu yaliyojitokeza na yanaeleza matarajio ya Bajeti yenyewe. Huo ni utaratibu mzuri kweli na kwa kweli nashukuru kwa sababu hotuba hii imekuja baada ya mambo matatu yafuatayo:-

Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, pamoja na kuiita Bajeti ya kisiasa, hii hatugawi kwenye Vyama vya Siasa ruzuku, watapata humu, lakini ni Bajeti ya kuwaendeleza Watanzania kwenye Mpango wa MKUKUTA ambao umeelezwa kwenye ukurasa wa tatu kutoka mwisho wa hotuba ya Waziri wa Fedha. Tumeazimia vilevile kumalizia Awamu ya Tatu kwa vishindo kwa vifua mbele kwa utekelezaji wa mambo ambayo yamefanywa kwa vipindi hivi viwili. Vilevile, Bajeti hii inakuja baada ya Mkutano Mkuu wa Taifa wa Chama cha Mapinduzi, tarehe 4 Mei, ambao ulifanyika kuchagua Viongozi wetu wa Serikali zetu mbili. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Zanzibar, ilitoa tayari tathmini ya etekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na kueleza na kuainisha maeneo mbalimbali. Hivyo basi, Bajeti hii ilikuwa kama inaingiza hayo mambo tu. Kwa hiyo, sisi tunaogelea, hatuogi, sikujiandaa kwa sabuni, wala taulo, lengo si usafi ni kuvuka. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna maswali kwanza nilitaka niyaeleze, haya lazima niyaeleze mapema kabla sijaingia kwenye hoja ya msingi kwamba, kwa nini tarehe ya mshahara haijulikani? Tarehe 24 mpaka 26 katikati ya hapo ndiyo mshahara wa Wafanyakazi. Wapo wachache, fedha zipo, *Cash Budget,* mapato ndiyo haya, kwa nini tarehe haijulikani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kero ya kulundikana katika Mabenki *NMB,* Watumishi hasa Walimu, pale Wami *Branch*, Morogoro, kwa nini walundikane vile? Nilikuta siku moja kama kuna Maulidi utadhani *Swalaat Jamiah,* unakuta kuna mkao wa namna ile.

**MBUNGE FULANI:** Hata hapa Dodoma.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini matatizo pale, wamejazana, kuna vurugu mno pale! Kwa nini watu wana-*overspend* wakati kuna *Cash Budget*? Mafuta ya petroli na diseli na mafuta ya taa kwa nini yapande bei? Tuliambiwa wakati ule kuna *flow meter*, tulidhani ni mkombozi, kumbe nayo imeongeza gharama! Mkulima tumemfutia kodi ya maendeleo, 2,000, 3,000 na 4,000 wakashangilia, kwa nini kilimo cha trekta Sh.17,000/= kwa hekari kwa mkulima huyo? Mikataba ya *IPTL, City*

*Water* bado wapo? Nashukuru nimeona kibao ndiyo hakipo, lakini wanasema kwamba bado wapo. Baaada ya kumaliza hayo, tunakwenda kwenye hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchumi wa mafanikio ya Serikali zetu mbili, utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2000, tunatoa hongera kwa Mheshimiwa Basil Mramba, pamoja na Manaibu Waziri wako Dr. Festus Limbu na Abdisalaam Issa Khatibu, Mheshimiwa Lyimo, Mgonja Msela, Kija, Bukuku na wengine walioko chini yenu. Wizara nyingine Mheshimiwa Abdallah Kigoda, Bukuku, Bendera na Watendeji wengine ambao nawafahamu na ninyi mliopo hapo mnaniangalia kushoto kwangu. Watendaji wote wa Hazina, Mipango, Wizara na Mikoa, hiki ndicho mlichokiomba? Kama mlikiomba, mmekipata? Mmefanikiwa? Kama mlipewa, hamjakiomba, kitumieni vizuri! Kama mlikuwa mmekiomba hamkukipata, nung'unikeni, mtapata mwakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ya Tanzania tabia yake, tuna amani, utulivu na mshikamano. Inaeleweka kwamba ni kimbilio la nchi nyingi kwa sababu tunaona walivyolundikana wakimbizi na kwamba ni ajabu ya kuku watatu wanaopigana, mweupe kumpiga mweusi, mwekundu kumpiga mweupe na mweusi kumpiga mwekundu, huo ni ugomvi wa ajabu lakini kuna nchi ya kimbilio, Tanzania. Kwa hiyo, tuheshimu, tunaheshimiwa na wenzetu majirani na sisi tuwaheshimu. Tumepata uhuru tukasema sisi kwanza, wengine baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu yeyote anayezungumza kwa takwimu anasifiwa kwa sababu alifanya utafiti na anapoongea kwa takwimu mara nyingi hakosolewi pale pale. Mara nyingi wanapofanya watakwimu taarifa zinakwenda kuangaliwa baadaye, inapotokea makosa watu hunung'unika huko wakati mwenyewe haupo. Kwa hiyo, muda wa kujisahihisha huna. Wanaoongea kwa maneno hukosolewa pale pale, mtu akiteleza, akichemsha huambiwa, hapana, sio balalababala ni barabara. Hujirekebisha hapo hapo, lakini hakikisha kariri hizo ni sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ziko takwimu zinatolewa sasa hivi, kwa mfano kuna tangazo wanasema, upande wa vifo kwa dakika moja, husema malaria huuwa mtu mmoja kila baada ya dakika tano. Kwa matangazo ya sigara, dakika nane kwa mtu mmoja. Sasa unakuta ukiorodhesha kwa pamoja kwa kweli wanakufa watu karibu 300 kwa saa, kwa takwimu walizozitaja. Sasa takwimu za kifo si sifa ya nchi. Takwimu za watu wanaopona toka hospitalini na kuwakinga ndiyo sifa za nchi. Kwa hiyo, ningeomba wasitaje idadi ya vifo kama ni sifa, sio sifa. *(Makofi/ Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa rushwa, mwaka huu mwezi Aprili, Kamati ya Fedha na Mipango ilitoa madaraka, kukasimu madaraka kupitia *reallocation* ya fedha katika Wizara mbalimbali ikaonekana kwamba rushwa ni sekta tambuka. Hivyo, Wizara zikapewa fedha na mwaka huu nikaona kipaumbele kimetolewa kwamba, zimetolewa fedha katika Wizara kwa ajili ya kusimamia na kupambana na rushwa. Hivi fedha ni silaha? Nimekuwa nawatania hapa kwamba mtu anapokuudhi mtupie mawe tu, fedha ni chambo, fedha ni chombo ambacho ni kibaya sana watu wanapokitumia. Kwa hiyo, hii rushwa ya vita ya fedha, ni sawasawa na kupambana na mtu anakutukana halafu

unamrushia keki. Unapigana vita kwa keki, rushwa ni tabia, msipigane vita kwa keki. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, muhimu kuangalia ni maeneo yaliyoanishwa na Jaji Joseph Sinde Warioba na Tume yake, katika maendeleo ya elimu, afya, ujenzi na usalama haki za raia. Katika vita usipambane kwa keki. Kwa hiyo, sheria ya *PCB* natoa wito kwa sababu hakuna neno rasmi la kukataa rushwa. Nawaambia Watanzania leo, kama Kigogo anakuomba rushwa, kataa mwambie "KAKURU" maana yake ni "Kigogo Acha Kuomba Rushwa." Kama raia anaomba rushwa kwa kigogo ili ampigie kura mwambie "RAKURU" yaani, Raia Acha Kuomba Rushwa. Maneno hayo yatumike kwa kigogo labda au kwa lugha gani hiari yao, rushwa hapo tutakuwa tumeidhibiti. *(Kicheko)*

Kuhusu udhibiti wa fedha, kuna trilioni nne, tunajigamba kwamba fedha zimepatikana kwa wingi, lakini katika hizo tumeona kuna *Subvote* ziko *intact* zimetajwa na eneo lake, barabara, *training* na kadhalika. Hakuna sehemu yoyote iliyoandikwa fedha za wizi, fedha zitakazopotea au fedha za kutolea rushwa, hakuna. Lakini taarifa ya Mkaguzi Mkuu, ziko potevu za wizi, ung'ang'anizi wa masurufu na Ankara vifani na manunuzi ya *nugatory expenditures*. Mtaziaona takwimu chache tu, kwa mfano *nugatory expenditure*s katika Mikoa mwaka huo ambao nilikuwa nimeutaja, Mikoa ilipoteza milioni 17, Serikali Kuu ilipoteza bilioni 2.3, upande wa ununuzi bila kutumia *proper authority*, yaani anaamua mtu kwenda kununua kitu bila utaratibu, ni bilioni 4.3. Vifaa vilivyonunuliwa lakini havikuchukuliwa bilioni 7.5, Ankara vifani *LPO* ile Lipa Pole pole Ofisa, ikazaliwa ni bilioni 4.5, masurufu na mikopo bilioni tano, malipo ya mishahara ya mashaka ni bilioni 49. Lazima tuwe waangalifu katika ulipaji, ama sivyo hizi trilioni nne, tukizitamka kwa majigambo zinaweza zikaishia mikononi mwa wajanja

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo sasa katika Wilaya ya Morogoro Vijijini, tuna Majimbo mawili, Jimbo la Morogoro Kusini na Jimbo la Kusini Mashariki. Tuna masoko ya kisasa mawili, kule Tawa na sehemu za Tandai Kinole, barabara 13 zimechongwa na vile vile tumejenga madaraja 28 kama Gizigizi na Mafumba na Mto Ruvu, madarasa 359 yamejengwa, nyumba za Walimu 150 zimejengwa, Walimu wapya walioajiriwa 317 na masoko mapya 12. Sekondari 12 na sasa hivi *MMES* tumeshaanza kuutengeneza Sekondari karibu 27 katika Kata zote. Kweye Jimbo la Mheshimiwa Mwenegoha na Jimbo la Mheshimiwa Semindu Pawa.

Katika upande wa barabara wana masikitiko wananchi wa kule, Luholole, Changa, Kibwaya, Mfumbwe, Logo, Uponda, Mfulu, Hewe, Bagilo, Nyamigadu, Mkololo, Kumba, Amin, Ludewa Burugi na maeneo ya kule Mkulazi Chanyumbu wanajisikia kwamba hawako tayari. Kwa sababu Serikali imetoa fedha Shilingi milioni 110. Fedha hizo hazijafika hadi leo. Kwa barabara ya kutoka Ubena kwenda Usungura, imebidi Meneja wa *TANROAD* Mkoa wa Morogoro anazisubiri fedha zile na mwaka unakaribia kwisha. Kwa hiyo, zile 110 zisirudishwe ili wananchi wa maeneo yale waweze kufanikiwa. Barabara yao vile vile Serikali iangalie kulinda viwanda vya mafuta ya mbegu, Abood na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, tunatoka hapa tuna kwenda kwenye uchaguzi. Uchaguzi ni hatua moja kama ni kuzirai kwa Bunge, hawajafa bado Wabunge, tumezirai, tutarudi tena. Kuna siku moja ilitokea ajali watu 12 walifariki, wakasema kuna Marehemu 12 hospitali. Nataka niseme hii ni muhimu sana, kuonyesha uhai wa Wabunge, Daktari apime mtu agundue kama kafa kweli, sasa huyu akapima wa kwanza kweli, wa pili kweli, wa tatu kweli, wanne Daktari akashitukia anapata kibao anapigwa na Marehemu. Alishituka akakunjwa Daktari chini, ilibidi Manesi na Madaktari wengine waliokuwa pembeni waingilie ugomvi kumnasua Daktari na alishikwa kweli kweli. Wakashangaa, mbona maiti hii ni ya ajabu? Baada ya hapo wakagundua kuwa yule Marehemu hakutokana na ile ajali ya magari, yule Marehemu ni kibonge alikuwa kwenye ugomvi Manzese, alipigwa sehemu mbaya tu kwenye Medula-oblongata akazirai na kupelekwa *mortuary*, baada ya kukaa siku tatu fahamu ikaja, sasa Daktari alipomuinamia alidhani huyo ndiye mgomvi wake ilibidi amkamate na kupambana naye. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mara nyingi watu waliozirai kama Wabunge, hotuba hii ni nzuri, lakini kwa Wizara zinazokuja zikituchokoza, wakianza kutuchokoza, tunakwenda kuzirai, tukirudi na ninahakika tutarudi wote hapa. Tunazirai, tunakwenda Majimboni wananchi watatturudisha hapa tukirudi sasa, ukitupima kuhakikisha kwamba tumekufa, tutazinduka tutawashika makoti. *(Kicheko)*

Baada ya kusema hayo ni kwamba, Bajeti hii ni nzuri sana. Tunaipongeza *TASAF, VTTP,* tunapongeza watu wa KKKT wamejitahidi sana. Sasa hivi tunatoa wito tu wakati Wabunge wako hapa watapitapita watu kwenye Majimbo, yale Majimbo kwa kweli ni Majimbo ya Wananchi, kwa hiyo, kama mnachangia michango naomba Wananchi waipokee. Pokeeni lakini msimamo wa Wabunge wenu mnajua mlikotoka nao. Hiyo ni sifa siku ya kuzika.

Tumeleta haya maendeleo mnayaona, ni maendeleo ya Bunge hili la Awamu ya Tatu. Kwa hiyo pokeeni wala msiwe na wasiwasi, kuna mtu katoa saruji pokeeni wala msikatae, hiyo ni sifa wakati wa kuzika. Tuliuguza mgonjwa miaka mitano sasa amekufa unakuja kutoa sanda ya milioni mbili, kwa nini msingetoa damu na dawa, wakati kama huu sio mzuri. Kwa hiyo, Bunge hili litakwenda pamoja ili tuipokee Serikali ya Awamu ya Nne tuendeleze haya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti shukrani haipo, kwa sababu siku moja kuna mtu alipofariki kwenda mbinguni akaambiwa atembezwe *section* za Mungu, akakuta sehemu moja akaambiwa hapa usiongee wako-*busy* kweli! Akauliza, pana nini? Akaambiwa kuna barua zinafungwa. Wanapokea barua za maombi kutaka duniani kwenda kwa Mungu kuomba kwa wale wanaotaka vyeo, Ubunge, Uwaziri na nini. Wakaenda sehemu nyingine wakakuta maboksi makubwa makubwa yanafungwa yanarudishwa duniani akaambiwa hawa usiwasalimu wako-*busy*. Kwa nini?

Hapa wanafunga majibu ya Mungu kwamba waliofanikiwa watafanikiwa huko duniani. Sehemu ya mwisho wakakuta *hall* kubwa, watu wamelala wanauchapa usingizi, akawauliza mbona hapa wamelala? Akaambiwa hapa hawana kazi ilitakiwa wale

waliofanikiwa duniani walete shukrani huku, sasa hakuna hata mmoja aliyeleta. Nashukuru sana naunga mkono hoja, ahsante. *(Kicheko)*

**MHE. TALALA BANA MBISE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Bajeti. Kabla ya yote nashirikiana na wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa ndugu, jamaa na wananchi wa Jimbo la Kilombelo kwa kuondokewa na Mbunge wao Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema Peponi. *Amin.*

Pia, nawapongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa na CCM kuwa Mgombea wa Kiti cha Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Dr. Mohamed Shein kwa kuchaguliwa kuwa Mgombea Mwenza. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa kuchaguliwa na CCM kuwa Mgombea wa Urais wa Zanzibar. Sote tunawatakia ushindi mkubwa katika uchaguzi ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze hoja kwa kusifia Serikali kwa ujumla kupitia Wizara ya Fedha chini ya Waziri na timu nzima ya Watendeji kwa kazi nzuri na ambayo imetolewa sifa nyingi. Wizara kama ambavyo waliotangulia wamesema imekuwa ikiendelea kuboresha utendaji wake tangu mwaka 2001 mpaka Bajeti hii. Kazi nzuri ikifanyika inasifiwa na hii inahitaji kusifiwa. Walioianya wapewe sifa inastahili wapewe *credit*. Kuna *sub-teams* tatu; Wizara, *TRA* na Benki Kuu. Huu utatu ukishirikiana na timu nyingine katika Serikali, wakishirikiana na wengine kwa kweli wamefanya kazi kubwa. Lakini Uongozi Mkuu na dira inatokana na neno, naomba nitumie neno ambalo ningependa lieleweke, niite “Utwiga wa Mheshimiwa Mkapa.” *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia utwiga kwa namna hii. Utwiga katika pesa zetu na twiga ni alama na nembo ya fedha zetu na ni nembo ya nchi yetu. Twiga ni mnyama ambaye tunamtumia kutoa kielelezo cha *vision*, anaona mbali hali chini, hula juu, anakuwa ni kielelezo cha dira na Mheshimiwa Rais wetu amekuwa na *vision* sio tu ikaishia kwenye mazungumzo au nadharia bali pia kuitenda kikweli kweli na kuonekana matokeo yake. Hii tunayozungumza sasa hivi uchumi wetu inatokana na *vision* yake. Mimi naona anastahili kabisa kama vile tunavyowaita wengine kuwa ni Simba wa Yuda huyu naye ni Twiga wa Tanzania. Mimi naona anastahili kuwa dira yetu ya Tanzania na yeye ni *visionary* ya Tanzania na *reference* yetu kuona ni mahali ambapo tunaweza tukapata uongozi wa Serikali ya nne na tutapenda kumtumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya tatu, tunapenda iendelee kuona huu uongozi ulipo katika hii Wizara iendelee kuutumia huu uongozi uliopo sasa hivi.

**MWENYEKITI:** Yaani ni Serikali ya nne.

**MHE. TALALA BANA MBISE:** Sawa Serikali ya Nne, Serikali ijayo. Mimi napendekeza kwamba iendelee kuutumia huu uongozi uliopo. Hilo ndilo pendekezo langu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala ambayo yanajitokeza ambayo yatahitaji kufikiriwa wakati Bajeti ikitekelezwa. Lakini kabla ya hapo nina ombi binafsi, ninatoka kwenye Kijiji ambacho ni kidogo, kina watu karibu 8,000, Kitongoji hicho kinaitwa Seela kwenye Kata ya Seela/Singisi Wilaya ya Arumeru, Jimbo la Arumeru Mashariki, kiko kama Kisiwa, kimebanwa na mito miwili mikubwa ambayo ni makorongo makubwa. Korongo la kwanza ni korongo la Mto Kibenu na la pili ni korongo la Mto Solomu. Makorongo hayo mawili yamewazunguka hao watu 8,000, kaskazini ni Mlima Meru na hiyo Mito imekuja kukutana, kwa hiyo *basically* wamefungiwa katikati. Watoto wao ili waweze kwenda Shuleni lazima wavuke hayo makorongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao wenyewe ili waweze kwenda hospitali au kwenye shughuli nyingine za maendeleo nje ya Kitongoji chao, lazima wavuke hayo makorongo mawili. Katika hayo makorongo lililo karibu nami, mita karibu 100 kutoka nyumbani kwangu, ndilo ambalo limenipa matatizo mimi kifamilia ambayo sitasahau. Ndiko ambako ajali ilitokea. Tulitengeneza kibarabara ambacho kwa gharama zetu wenyewe katika familia yangu mwenyewe binafsi, kujaribu kufungua njia ambayo ingeweza kufungua kuifanya angalau *i-open up* hicho Kitongoji. Nadhani nimeona uchungu wake. Tumejaribu kwa muda mrefu kuona ni jinsi gani Serikali inaweza ikafungua hicho Kitongoji kwa kutuwezesha tuweze kupata mawasiliano na jamii nyingine zinazozunguka hicho Kitongoji.

Katika korongo hilo ambalo tumefungua hicho kinjia, haijawezekana, kwa njia ya daraja imekuwa ni tatizo tukaona wenye utalaam wa Uhandisi wa barabara wakaona njia pekee ni kupata labda tingatinga. Tinga tinga lije libomoe upande moja na upande mwinge lijaze hapa katikati na pale kwenye mto unapopita yawekwe makaravati na kupata hilo tingatinga ikatugharimu sio chini ya Shilingi milioni 25 mpaka 30 na ijaze ili watu waweze kufunguliwa katika hicho kisiwa.

Ombi langu kwa Serikali hii kwa Mheshimiwa Waziri, tunaomba tuonewe huruma, katika hilo korongo limewaondoa watu wawili maisha yao, mtu mmoja yuko kitandani kwa miezi minane sasa hivi na mwingine amepinda shingo kwa ajili ya kuanguka kwenye hilo korongo. Tunaomba tusaidiwe, ni ombi letu la kilio kabisa kabisa kwa hao wananchi 8,000 walioko kwenye Kitongoji cha Kibenu. Ombi letu tunaomba kwa unyenyekevu tusaidiwe tuondokane na hiyo kero tuweze kufaidika na matunda ya maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Masuala mengine ambayo yamejitokeza katika Bajeti hii ni suala la ajira. Suala la ajira limezungumzwa na watu wengi, ni suala kubwa. Kuna takwimu zinazojitokeza kuhusu ajira, sehemu nyingine wanatoa kwamba ni aslimia 28 ya watu wenye umri kati ya miaka 15 mpaka 24 kwamba asilimia 28 katika Miji yetu hawana ajira. Wengine wanatoa asilimia 43 haina uhakika, inatoa mkanganyiko hapo. Wengine wanasema watu milioni mbili katika sekta rasmi hawana ajira, wengine katika sekta isiyo rasmi karibu milioni 15 hawana ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu mimi ni kwamba katika kulitazama hili suala la ajira, kitu cha kwanza ambacho tunahitaji kukifanyia kazi ni kuweka takwimu zetu sahihi, ziweze kutusaidia katika kupanga na kuona uzito wa hili suala ni upi. Japokuwa suala hili tunaliona uzito wake Mijini na Vjijini, pia ni tatizo kubwa, kwa wale ambao tunakaa Vijijini tunaona madhara ambayo yanapatikana kwa vijana wetu ambao wanakaa vijiweni. Masuala ya dawa za kulevya, ulevi wa aina nyingi na maovu mengine ambayo kwa kweli ni vigumu, lakini wengi tumeona adha hiyo. Kuna adha nyingine tunazopata kuhusu masuala ambayo yanahusu masuala ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali imetoa matamko kwamba wananchi, watoto, wazee na wajawazito katika hospitali zetu wapate huduma bure. naomba hili niseme wazi wazi kwamba hii japo ni kweli kwamba inarudiwa mara kwa mara lakini usimamizi wake bahati mbaya, wajawazito, watoto na wazee wanapokwenda kupata huduma za afya katika Vituo vinavyotoa hizo huduma, aidha lazima walipe kidogo kitu chochote au wasipofanya hivyo hawapati huduma.

Wengine wanaambiwa walete *gloves* zao wenyewe kama ni wajawazito, watoto wanapokwenda wanaambiwa lete hela angalau hela ya kuanzisha faili Sh. 1,500/=, wengine lazima ulipe vinginevyo utoe chochote vinginevyo hakuna mhudumu yeyote katika Kituo cha Afya ambaye atakuja kukuona akupe huduma kama hujanyoosha mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niite ni uhasama na huo uhasama ndio huo huo unaitwa ufisadi. Ufisadi huo kwa kweli upo, sijui itakuwaje. Lakini naomba hili lieleweke hivyo. Wengine wanambiwa waje na daftari zao, katika Mahakama zetu usipokwenda na daftari lako ili uandikiwe *statement*, uwe na chochote cha kuweza kukuwezesha wewe kuweza kuzungumza na Hakimu, kwa kweli mambo yako hayajakwenda. Huo ndiyo ukweli na watu wananyimwa haki yao kwa sababu ya hiyo hali.

Kuhusu masuala ya wenye trekta ambao wanasumbuliwa na hasa kwenye Jimbo langu; kwenye Jimbo langu nimekuwa nikifuatwa na watu kwamba wanafuatwa na Watendaji katika *TRA,* wanawafuata wakidai wapewe kodi ya mapato. Wanapokwenda wanadai kwamba kama hutoi wanachukua zile trekta zao wanawangojea tu wakati wanatoka shambani wanachukua wana-*impound* trekta zao na vifaa vingine vya shamba pamoja na trela zao, vinapelekwa mahali na ili waweze kukomboa ni lazima watoe chochote. Hiyo imetokea na mimi mwenyewe nikashuhudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishindwa kufanya lolote, lakini naomba nitoe hiyo kama taarifa na ifahamike kwamba kuna huo mchezo na tunaomba wanaohusika wahakikishe kwamba tunaondolewa hiyo kero kama ikiwezekana na nina imani inawezekana kwa sifa ambazo wanazo *TRA* na tunawasifu na kuwaheshimu kabisa kwa utendaji wa hali ya juu mno. Ni bahati mbaya kwamba kuna wachache ambao wanakuja kuharibu hizo sifa kwa vitu vidogo vidogo kama hivyo. Tuna imani kabisa kwamba siyo sera ya *TRA* hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. PHILIP S. MARMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kujadili hoja ya Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi Mipango.

Awali wa yote, ninaungana na wenzangu kutoa mkono wa rambirambi kwa ndugu jamaa wa Marehemu Mbunge wa Kilombero, Hayati Abu Kiwanga. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi. Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nachukua nafasi hii kuwapongeza viongozi wa Chama Cha Mapinduzi walioteuliwa ili baadaye wagombee nafasi za ngazi ya juu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti hii kwa ujumla wake ni nzuri na imesifiwa ndani na nje ya nchi. Uzuri wa Bajeti hii na ukuaji wa uchumi wa nchi yetu, unatia matumaini siyo tu kwetu sisi lakini pia kwa vizazi vinavyokuja. Dunia nzima inatupongeza kwa jinsi ambavyo tunaendesha uchumi. Lakini nashangaa sana raia wenzetu ambao wanazikebehi jitihada hizi. Hatari ambayo mimi naiona mbele yetu ni kwamba wananchi baadaye watawapuuza.

Nchi yetu ni nchi ya Vyama vingi na kama ilivyo desturi, kila mchezo una masharti na kanuni zake. Kama ni soka kunakuwa na wachezaji 11 kila upande, sasa ikitokea humu kuna wachezaji 12 kutoka Mkoa mmoja unaitwa labda Kaskazini Pemba baina ya wachezaji wengine 300, itakuwa ni hatari sana kwa Demokrasia ya nchi yetu.

Katika demokrasia ya Vyama vingi, kila Chama kinajiandaa vizuri sana ili kupambana kisiasa na Vyama vingine. Misuli ambayo tunajiandalia kama hakuna mahali pa kuipeleka ni hatari kubwa sana kwa wananchi. Kwa hiyo, mimi ningewasihi sana wenzangu, tukisema kwamba zulia lililoko ndani ya Ukumbi wa Bunge ni jekundu, wasiseme ni jeusi kwa sababu wananchi wataona watu wa ajabu, lakini ni hatari mbele yetu kwa sababu tunarudia katika hali ya Chama kimoja katika mazingira ya Vyama Vingi na hii siyo manufaa kwetu sisi na siyo manufaa kwao na siyo manufaa kwa wananchi zaidi ya milioni 40 sasa wa Tanzania. Kwa hiyo, tuwe pamoja katika kusifu haya mazuri yaliyoko na tutoe changamoto kwa yale yote ambayo siyo mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi, aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Fedha Duniani *(IMF),* Michel Camdessus alipokuwa hapa nasi, mimi nilinyoosha mkono kumwomba Spika aniruhusu nimwulize maswali kadhaa, kwa bahati mbaya sikupewa nafasi. Lakini swali nililotaka kumwuliza ni kwamba Tume ya Afrika ambayo Tanzania ilibahatika kuwakilishwa na Mheshimiwa Rais wetu na Mheshimiwa Prof. Anna Tibaijuka, hatima yake anadhani itakuwaje? Tofauti yake ni nini na Tume nzito kama hizi zilizopita.

Wakati wake Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na mwenzake *Chancellor* Wilbrant wa Ujerumani walikuwa na Tume kama hii yenye heshima kubwa

lakini baadaye taarifa yake ikawa kwenye *shelf*. Lakini leo na jana tumepata jibu, kwamba jitihada za Waziri Mkuu wa Uingereza, Tony Blair zimezaa matunda. Nchi yetu ni katika nchi 18 ambazo zimesamehewa madeni. Sasa ninashangaa wenzangu wasiposhangilia jambo hili jema kwa watu wetu. *(Makofi)*

Ninavyofahamu madeni yatakayosamehewa ambayo nafikiri ni kati ya leo na miezi 10 ijayo, ni yale ya Benki ya Dunia, Shirika la Kimataifa la Fedha Duniani *(IMF),* nchi ya Amerika, Uingereza, Ufaransa, Kanada, Italia, Japani na marafiki wengine na Benki ya Maendeleo ya Afrika na kadhalika. Kwa maana ya mahesabu, maana yake tutakuwa tumesamehewa zaidi ya nusu kwa Bajeti ya mwaka huu. Tukisema tu kwamba pengine tumesamehewa nusu ni kwamba tutakuwa tumesamehewa Shilingi bilioni 288. Hii ni nusu kwa sababu tunadaiwa, mwaka huu tulitenga katika Bajeti na bila shaka tutaangalia Bajeti upya kabla hatujaondoka hapa Dodoma kwa sababu ilikuwa tutenge na tumetenga katika *approximated fund* Shilingi bilioni 575.3. *(Makofi)*

Tuseme sasa nusu tunakuwa tumesamehewa, kwa hiyo lazima wenzetu katika Wizara ya Fedha na Mipango kati ya sasa na Julai 30 kabla hatujapitisha *Financial Bill*, tujue kwamba sasa Bajeti ni tofauti na mimi nachukulia tu kwa juu juu, pengine ni nusu lakini zaidi ya nusu, tutakuwa na ziada ya bilioni 288.6.

Tumefanya mambo mazuri sana katika nchi hii, lakini pia sisi ni binadamu, tumefanya makosa mengi pia. Nashukuru Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mramba juzi ametembelea Rukwa, kama raia mwema bila shaka dhamira yake inamdai jinsi barabara za Rukwa zilivyo na wakati huo huo tunajenga barabara kwenye Makao Makuu ya Wilaya ambayo siyo muhimu sana. Wilaya yenye uzalishaji mkubwa kama Rukwa barabara zake ndiyo zile, lakini hapo hapo utajenga barabara ya lami mahali ambapo pengine siyo muhimu sana katika miaka ishirini ijayo na hapa ni Tanzania. Moja, na hasa ukirejea kwenye hii bilioni 288, kwa sababu tunasamehewa itufikie wote. *(Makofi)*

Bajeti ya mwaka huu tukienda kwa undani inaweza kuwaumbua baadhi ya wenzetu. Fedha ambazo tuna hakika zinagawiwa kwa haki, nafikiri ni fedha za Elimu, hata ukiwa kwenye ndege unaona Shule zinavyojengwa, lakini barabara, acha *corridor* zetu hizi, hatuna ugomvi na *corridor*, lakini pita Mkoa mmoja kwenda Mkoa mwingine ni kama unakwenda nchi tofauti.

Leo tukiangalia Bajeti ya Mkoa fulani ya fedha za Maendeleo ya barabara ni mara nne au mara tano ya Mkoa mwingine. Fedha hizi ni ridhaa siyo ya Rais ya Waziri. Sasa tutasema, lakini baadaye tutakujasema, kwa sababu inajulikana wazi kwamba mgawo wa fedha za barabara siyo mzuri na hauna mpango ambao unaelekea kwamba utakuwa mzuri. Hapa nieleweke siongelei fedha za Serikali za Mitaa zile ambazo zinapitia TAMISEMI, nafuu zile tunazifahamu zinavyogawiwa. Lakini zile ambazo ni za (*Development),* fedha za maendeleo ambazo sasa hivi kwenye kitabu zimelundikwa pamoja*, limit discretion*. Bahati nzuri Rais wetu muungwana sana hajatumia *discretion* nafikiri kwa fedha hii, lakini fedha hizi zimetolewa kwa *discretion* muda wote na Wilaya zetu nyingine hazipitiki, siyo kwamba hakuna fedha, ni kwamba mgawo ni mbovu.

Eneo la pili ni umeme. Umeme, tuache pembeni Wilaya ambazo kwa sababu zisizozuilika haziwezi kupata umeme, lakini kuna Wilaya zina umeme tunaweza hata kutenga hata kilomita mbili lakini haiwezekani. Lakini kuna Kitongoji kidogo chenye nyumba tano kinapata umeme. Hapa mimi nimejadili sana juu ya *Electricity fall,* nimepewa kilomita 20, baadaye zimeondoka sijui zimekwenda wapi. *Discretion* katika uendeshaji wa nchi ni mbaya sana na ndiyo maana Kenya haipo katika nchi 18 zilizosamehewa madeni.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha na wenzako, naomba kuwarejesha, tuseme tutasamehewa nusu kwa miezi 12 ijayo na ni bilioni 288. Tafadhali nusu ya hizo ambayo ni bilioni 100 na 40 hivi, kila Wilaya ipewe bilioni moja. *(Makofi)*

Mimi nikipewa bilioni moja, barabara zangu zitakuwa nzuri. Siyo za Halmashauri, zile za *TANROADS* ambazo kwa sasa fedha zake ni *discretion*. Nitapeleka umeme kule ambapo ilikuwa imepangwa umeme upelekwe lakini baadaye kuondolewa. Tukubaliane hapa, fedha hizi kila Walaya ikipata bilioni moja, tuna Wilaya 120 na kitu, bado Waziri utakuwa amebakiwa na bilioni zaidi ya 180 za shughuli zake nyingine.

Kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amesema, kila Kijiji kitapata milioni tatu, basi kila Wilaya ipate bilioni moja na tutazitenga hapa hapa. Mimi nitasema nitaendesha *TANROADS* kwa ajili ya barabara zilizoko Wilaya ya Mbulu. Nitazipeleka *TANESCO* Kwa ajili ya kilomita 20 za umeme Wilaya ya Mbulu. Kila kiongozi ataeleza kama atakavyozitumia ili haki itendeke. Tumefikia hapa kwa sababu tunajaribu kutenda haki na kama binadamu pia tukubali pia tumekosea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ambayo mimi natoka huwa tunapata ujio wa Watalii kati ya 300 mpaka 600. Hawa Watalii hawafiki kule kuangalia wanyama au mandhari, wanakuja kuangalia Watanzania, familia zaidi ya 500 ambao wanaishi kwenye mapango, ambao wanakula matunda na mizizi.

Mara tu baada ya uhuru, Mheshimiwa Baba wa Taifa alichukua Mabwana Maendeleo na Bibi Maendeleo akiwepo Anna Abdallah kule, kuwatoa hao watu katika mazingira yale. Bahati mbaya haikuwezekana na sababu kubwa ilikuwa fedha. Leo tuna fedha, ni fedheha familia 500 za nchi yetu ziishi maisha kama haya. Viongozi wa eneo hilo siyo kwamba hatukuwa tunaliona hili, tumelitengea fedha kwenye Bajeti lakini hata siku moja Bajeti haijakubaliwa, iwe elimu, iwe afya au barabara.

Namshukuru sana Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa kwa kumruhusu Mheshimiwa Waziri Mkuu ahudhurie mazishi ya Dr. Arson kule Norway kwa sababu ilikuwa yeye tu amejaribu kufanya kila jitihada afungue viwanja vya ndege nane katika mapori yale ili angalau watoto na akina mama wale waweze kupata chanjo. Lakini bahati mbaya Mwenyezi Mungu amemchukua, hatujui hali itakuwaje, lakini sisi bado tunaongea juu ya kupeleka milioni tatu kwenye kila Kijiji.

Pengine hili linaonekana kama jambo geni, lakini pengine Waziri aangalie katika Bajeti za Wilaya mbalimbali, ikifika Wilaya ya Mbulu aone jinsi ambavyo tumejitahidi

kwa uwezo wetu wote kulileta jambo hili kama jambo la pekee ili nchi yetu iachane na fedheha hii.

Hawa ni Watanzania wenzetu wanataka maendeleo kama sisi, tunaongea juu ya Mfuko wa Elimu kwa ajili ya Chuo Kikuu ambapo sehemu kubwa fedha zitakwenda, lakini hawa waliomaliza Darasa la Saba wanahesabika. Waliofika mpaka Sekondari mpaka leo kwa kumbukumbu zangu wako tisa tu na hawa wanatoka katika familia 500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kumalizia kwa kusema kwamba mimi baadaye nitakuja kuunga mkono Bajeti hii iwapo kutakuwa na mfumko, bajeti itakuwa imefumuliwa kutokana na matukio haya mazito yaliyotangazwa juzi na Gordon Brown, Waziri wa Fedha wa Uingereza ambaye kwa kweli ni rafiki wa kweli wa nchi yetu na sisi ili kuonyesha pia tunathamini urafiki huu, tufumue Bajeti hii, ilenge na itekeleze matakwa na malengo yake. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi nichangie hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na hotuba ya Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia, naomba niungane na Wabunge wenzangu, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kibakwe, kutoa salamu za rambirambi kwa kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Kilombero, Mheshimiwa Kiwanga na Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi. Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nampongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mbunge wa Chalinze kwa kuchaguliwa kushika bendera ya CCM katika kinyang'anyiro cha Urais mwishoni mwa mwaka huu mwezi Oktoba. Tuna uhakika kwa kuchaguliwa kwake, Chama Cha Mapinduzi kitapata ushindi wa kimbunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza Mawaziri wote wawili kwa hotuba zao nzuri na zenye matumaini makubwa kwa maendeleo ya wananchi. Mwenzangu Prof. Maghembe alijikita kwenye elimu, mimi naomba nijikite kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mingi tumekuwa tukisema kuwa kilimo ni uti wa mgongo, kilimo ni sekta ya msingi, kilimo ni sekta kiongozi na Mheshimiwa Waziri wa Mipango amesema hivyo hivyo kwamba kilimo hadi sasa kinachangia asilimia 48.8 ya pato la Taifa. Kilimo kimechangia asilimia 66 ya fedha za kigeni, kilimo kinatoa ajira kwa asilimia 70 ya Watanzania. Kilimo kinakua kutoka asilimia 3.4 mwaka 2000 hadi asilimia 6.0 mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sifa hizi zote, Sekta ya Kilimo bado imebaki vile vile. Mkulima amebaki maskini, mkulima amebaki mnyonge, mkulima amebaki akitumia zana duni za kilimo ingawa anategemewa kubeba uchumi wa kisasa wa karne ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kilimo chetu ni duni na kiko nyuma sana. Ni kweli kinaajiri asilimia 70 ya Watanzania, lakini ni cha kujikimu tu na kwa sababu hiyo na kwa kweli si ajabu kikachangia asilimia 48.8tu ya pato laTaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijenge hoja kwamba kilimo kimepoteza sifa za kuwa sekta kiongozi katika mipango na mikakati iliyopo. Mimi nasema ni wazi kama kilimo kinaajiri asilimia 70 ya Watanzania lakini bado kinachangia asilimia 48 ya pato la Taifa, basi kutakuwa na tatizo la msingi. Mimi nasema kuna tatizo la mtizamo juu ya kilimo na kuna tatizo la uwekezaji katika kilimo.

Wananchi wetu hawana matatizo kabisa, ukiwaambia limeni, sasa ni wakati wa mvua za kupanda, watapanda, mvua za kwanza za kufanya nini, watafanya. Hawana tatizo la kufanya jitihada za kulima. Lakini nataka niseme, wakulima wetu wanalima kama mazoea bila msaada wa kutosha wa kitaalam. Bila msaada wa zana bora za kilimo, bila msaada wa mbegu bora, bila msaada wa masoko ya mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti hii tumeambiwa kuwa ni Bajeti ya MKUKUTA, na katika hoja ambayo naijenga hapa, ungeweza kusema ni Bajeti ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini, lakini kama tunasema kilimo ni sekta kiongozi, basi ungeweza kusema ni Bajeti ya kukuza kilimo na kupunguza umaskini wa wakulima wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukipitia kitabu hiki cha mpango wa MKUKUTA, uwekezaji uko vipi? Sekta ya kwanza ya Ujenzi bilioni 271, Sekta ya sita ni kilimo, bilioni 63.4. Kilimo inashika nafasi ya sita, lakini bado tunasema kilimo ni sekta kiongozi. Iko namba sita, tunaomba maelezo tena maelezo ya kutosha kabisa. Kwa nini kilimo kiwe sekta kiongozi halafu katika uwekezaji ni cha sita, tena siyo kwa pesa nyingi, ni kwa pesa kidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mikakati iliyomo kwenye kitabu hiki ni mizuri na mimi naiunga mkono mia kwa mia. Lakini nataka niseme kwamba mambo yaliyowekwa humu siyo mapya. Unaweza kurudi nyuma kwenye kumbukumbu ukayakuta kwa lugha nyingine lakini mambo ni yale yale. Lakini tatizo limekuwa ni utekelezaji wa yale ambayo tunayasema. Naomba nitoe mifano. Kule katika Jimbo langu la Kibakwe, wananchi mwaka huu wamelima ufuta, tena wamelima kwa wingi na wanastahili pongezi kwa kweli. Wameitikia wito wa Serikali yetu wa kuingia katika mazao mapya na MKUKUTA.

Umesema kuwa, sasa na ni wakati wa kuingia katika mazao mapya badala ya kuendelea kutegemea mazao asilia. Katika kuingia katika kilimo cha mazao mapya wananchi wa Jimbo la Kibakwe walitegemea umaskini walionao utapungua, lakini wana tatizo la soko la ufuta. *(Makofi)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Kibakwe wamelima ufuta wa kutosha, mwingi kabisa, lakini wana tatizo la soko. Sasa hivi wananchi wa Jimbo hili waliolima ufuta hawana mahali pa kuuza ufuta wao na wamejitokeza walanguzi,

wafanyabiashara wa kati ambao wanawadanganya wakulima na kuwapa bei ndogo sana. Debe la kilo 20 wananunua kwa Sh. 4000/= au chini ya hapo. Kwa hiyo, wananchi wangu wanalazimika kuuza ufuta wao kwa bei hiyo ndogo na matumaini yao ya kupambana na umaskini yamepotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikiwaahidi wakulima wa mazao mchanganyiko kwamba itawaundia chombo kitakachoendeleza na kusimamia mazao hayo. Lakini sasa imepita takriban miaka miwili au mitatu, chombo hicho hakijaundwa. Kwa hiyo, pamoja na mazuri yote ya Serikali ya Awamu ya Tatu, suala hili la kuwasaidia wakulima wa mazao mchanganyiko halikupewa uzito unaostahili.

Sasa katika MKUKUTA na Bajeti hii ya MKUKUTA, Serikali inatoa ahadi gani nyingine katika Bajeti hii? Katika mpango huu wa MKUKUTA, Serikali inatoa ahadi gani kwa wakulima wa zao la ufuta wa Jimbo la Kibakwe na mahali pengine katika kuwaondolea kero hii ya soko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa pili naomba niongee kidogo juu ya kilimo cha umwagiliaji maji katika maeneo yetu. Lengo la *MKUKUTA* ni kupanua kilimo hiki kutoka hekta 218,000 mwaka 2004 hadi hekta 254,000 mwaka 2007 ambayo ni sawa na hekta 12,000 kwa mwaka. Kwanza kiwango hiki cha upanuzi ni kidogo sana. Kusema kweli upanuzi wa kiwango hiki ni mdogo sana na kwa kweli unaweza kusema bado Serikali haionyeshi kwamba iko *serious* katika kupanua kilimo cha umwagiliaji maji kama ni kilimo cha kutegemewa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Kibakwe kuna *scheme* za umwagiliaji maji katika Vijiji vya Mwanawota, Mlunga, Wangi, Galigali, Matonya, Mbuga, Lufu, Mangaliza ambazo kama zikifufuliwa na kuboreshwa zitatoa mchango mkubwa katika kilimo cha umwagiliaji maji. Vile vile, katika Kijiji cha Malolo huko nyuma, Serikali ilijenga *scheme* ya umwagiliaji maji, lakini ikasahauliwa kabisa na sasa kuna ugomvi mkubwa wa kugawana maji kidogo yaliyopo kwa sababu utaratibu wa mifereji umekufa. Nashauri Serikali katika mkakati wake wa kuboresha kilimo cha umwagiliaji maji, basi itazame namna gani ya kufufua *scheme* hii ya umwagiliaji maji kule Malolo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, katika Jimbo langu la Kibakwe kuna Mradi wa Umwagiliaji Maji wa Bonde la Lumuma, ambalo tunachangia na Wilaya ya Kilosa. Malengo ya mradi huu ni mazuri na faida yake kwa wakulima wa Mafeni na Kitati itaonekana zaidi kama mradi huu utafanyiwa marekebisho. Huu mradi ulivyojengwa mabanio mengi na mifereji mingi ilijengwa upande wa Kilosa.

Kwa hiyo, upande wa Mpwapwa ambako ndiko liliko Jimbo langu, hasa kwa Vijiji vya Mafene na Kitati wamekuwa hawafaidiki na mradi huu. Kwa hiyo, ili *MKUKUTA* uwe wa maana kwa wananchi wangu wa Mafene na Kitati, ninashauri Serikali iutazame upya huu mradi mkubwa kabisa tena wa mabilioni mradi wa umwagiliaji maji wa Bonde la Lumuma na ufanyiwe marekebisho ili pande zote mbili zifaidike na mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nataka niseme tena kama walivyosema wenzangu kwamba ninaunga mkono hoja zote mbili kwa asilimia mia kwa mia. Tunachotaka sasa na ninachosubiri ni utekelezaji ili kutimiza azma iliyomo katika hotuba hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hizi. *(Makofi)*

**MHE. ELISA D. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia machache katika hotuba mbili za Bajeti za Waziri wa Nchi, Mipango na Ubinafsishaji na Waziri wa Fedha.

Kwanza, kabisa kabla ya mchango wangu nichukue nafasi hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili pamoja na Manaibu Mawaziri wao, Makatibu Wakuu na Manaibu wao, Wakurugenzi na Wafanyakazi wote wa Wizara hizi mbili kwa maandalizi mazuri ya Bajeti iliyoletwa mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha nichukue nafasi hii ya kipekee kabisa kuungana na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mbunge wa CCM Chalinze na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa kuchaguliwa kwake kwa kishindo na CCM kuwa Mgombea Urais kwa tiketi ya CCM ya Urais wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, naomba niseme kwamba Serikali, imetekeleza Bajeti ya mwaka 2004/2005 kwa mafanikio makubwa sana. Baadhi ya mafanikio tumeelezwa, ni kukua kwa uchumi wetu ambao umekua kutoka asilimia 5.4 na kufikia 6.7. Mfumko wa bei umedhibitiwa kutoka asilimia 21 mwaka 1996 hadi asilimia 4 mwaka 2005. Ukusanyaji wa mapato ni wa kuridhisha sana kutoka bilioni 37 kwa mwezi hadi kufikia bilioni 145 kwa mwezi katika mwaka huu wa 2005. Tumeelezwa pia kwamba riba ya kukopesha kwenye Mabenki imeshuka kutoka asilimia 26 mwaka 1996 hadi sasa ipo kwenye kiwango cha asilimia 14.4. *(Makofi)*

Aidha, Serikali imefanikiwa kuboresha huduma muhimu za jamii, ikiwemo maji, afya, barabara, kilimo, vita dhidi ya Ukimwi, Elimu ya Msingi na Elimu ya Sekondari, hususan miradi miwili ya Elimu ya *MMEM* na *MMES*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maendeleo haya na kwa vigezo hivi, Serikali ya Tanzania imepongezwa na vyombo vya fedha, Taasisi za Fedha na Uchumi za Kimataifa. Napenda nichukue nafasi hii basi kuipongeza Serikali kwa mafanikio ya kutekeleza Bajeti ya mwaka 2004/2005 na kwa mtiririko huu natumaini Serikali itatekeleza kikamilifu Bajeti ambayo imeletwa mbele yetu ya mwaka 2005/2006. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya mwaka huu wa 2005/2006 ni Bajeti nzuri. Nasema ni nzuri kwa sababu ina mwelekeo mzuri. Kima cha chini cha mshahara kimeongezwa na mzigo wa kodi katika kima cha chini umeondolewa; kero ya madai ya Walimu imeshughulikiwa na watalipwa kikamilifu; kero ya wastaafu ambao hawakuwa wamelipwa mafao yao kwa miaka mingi hususan wale wa Jumuiya ya Afrika Mashariki,

tumeelezwa kwamba watalipwa kikamilifu na kero ya Watendaji wa Vijiji ambao hawajalipwa kwa muda mrefu tumeelezwa kwamba watalipwa fedha zao kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio haya niliyoyataja na kwa mtiririko wa mafanikio yaliyoorodheshwa katika kifungu cha 34 cha hotuba ya Waziri wa Fedha, ukurasa ule wa 34 hadi 38 natamka kwamba, mimi binafsi naona kwamba Bajeti hii ni nzuri na inatekelezeka. Naipongeza Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba wenzangu wengi wamezungumzia Sekta ya Kilimo, naomba na mimi niungane nao kusema machache kama ifuatavyo:- Tumeambiwa na tumeelezwa na tunafahamu kwamba Sekta ya Kilimo inachangia asilimia 48 ya pato la Taifa, asilimia 66 fedha za kigeni na inatoa ajira kwa asilimia 70, mimi nilikuwa nafikiria zaidi ya asilimia 70, lakini tumeambiwa ni asilimia 70 ya Watanzania wanaajiriwa ama wanajiajiri katika Sekta hii ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu hizi, kila mmoja wetu anaona mchango wa kilimo katika uchumi wetu. Hivyo basi, ningeona kwamba ni vyema Serikali ishawishike kuongeza uwekezaji katika kilimo, barabara, miundombinu mbalimbali kama vile masoko ya ndani ya mazao yetu ya kilimo, masoko ya ndani na viwanda vya kusindika mazao ya kilimo ili tupate bidhaa mbalimbali ambazo zinaweza kuwa bidhaa mbadala ya mazao ya kilimo ambayo sasa hivi tunaagiza kutoka nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila wakati tumesema na sitaki nirudie, lakini tumesema kwamba hii ni sekta muhimu sana, sekta kiongozi, sekta mama, sekta muhimu, tumebakiza tu kusema ni sekta baba. Lakini naomba nitazame ule ukurasa wa 16 kwenye kitabu hiki cha Mpango wa Maendeleo wa Mwaka wa 2005/2006 ambao umetolewa Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa huo wa 16 mpango wa mwaka wa 2005/2006 *program* zifuatazo kwenye Sekta ya Kilimo zitatekelezwa. Nafikiri wote mnaona pale, Bajeti hii ni shilingi 63,490,000,000/=. Kati ya hizi, Shilingi bilioni 63.4 maendeleo ya utafiti yenyewe inachukua bilioni 38, Sera na Mipango inachukua bilioni 12. Kwa hiyo, vipengele hivi viwili katika Bajeti hii vinatumia bilioni 50 kwa sera na mipango na utafiti. Kama walivyotangulia wenzangu kusema, vipengele hivi vinajirudia mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitazama umwagiliaji maji mashambani, fedha zilizowekwa pale ni Shilingi bilioni 2.9 ni chini ya asilimia mbili ya Bajeti ya kilimo. Kipaumbele gani hiki tunachokipa kilimo hasa hiki cha umwagiliaji kama ni asilimia mbili ya Bajeti ndiyo inakwenda kwenye kilimo chenyewe? Hii nyingine ni tafiti na sera na mipango? Ebu naomba Bajeti hii itazamwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba kama tukiwekeza vizuri kwenye Sekta hii ya Kilimo, uchumi wetu utaibuka kwa haraka sana na hata kupita kiwango hiki ambacho kimewekwa ambacho tunatarajia kwa mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ajira ni wazi na limezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wengi. Mimi naamini kwamba wakati umefika sasa Serikali iwawezeshe wananchi, vijana wetu, wataalam wetu wajiajiri wenyewe na njia mojawapo ya kujiajiri wenyewe kwa Watanzania, ni kuwawezesha waingie kwenye Sekta ya Kilimo. Ninaamini kabisa kwamba Sekta ya Kilimo ikipewa viwanda ikapewa miundombinu, viwanda vya kusindika mazao. Mimi naamini kabisa kwamba tutaibua ajira kwa vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeandaa mikakati mazuri ya kupunguza umaskini na kukuza uchumi kama *MKUKUTA*, *Tanzania mini tigers* 2020 na *TASAF*. Miradi hii nina hakika kama ikitekelezwa vizuri hali ya maisha ya Watanzania itaboreka kwa kiasi kikubwa na naamini kabisa kwamba uchumi wetu utakua kwa kiwango kikubwa. Naona basi ni vyema niishauri Serikali kwamba katika utekelezaji wa hii miradi ambayo inachukua fedha zaidi ya nusu ya Bajeti ya mwaka 2005/2006 kuweko na usimamizi thabiti katika ngazi zote, ngazi za Taifa, Mkoa, Wilaya hata za Tarafa na Kata ili tuhakikishe kwamba miradi hii inasimamiwa vizuri.

Pia, ni muhimu wananchi wanaohusika kwenye ngazi zote wapewe elimu ya kutosha na kuwepo na taarifa za mara kwa mara na taarifa zozote zenye mapungufu na dosari lazima zishughulikiwe kwa wakati unaotakiwa**.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumalizia kwa kusema kwamba tumepata bahati Jemadari wetu, Mheshimiwa Rais Mkapa, amewashawishi Wahisani waliokuwa wanatukopesha na wametufutia madeni yote. Naomba jitihada hizi za Mheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Tatu ziendelezwe na Serikali zijazo. Naomba tu kusema kwamba katika hii ili tupate watu hawa wa nje, hawa Wahisani waliotufutia madeni waendelee kutuamini, lazima tuendeleze utawala bora, vita dhidi ya rushwa, vita dhidi ya ukiukaji wa haki za binadamu ili tuendelee na kuaminika na kukopesheka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwamba, katika Bajeti hii ya mwaka huu 2005 sijaona kama Serikali imechukua tahadhari yoyote kuhusu njaa ambayo inawezekana kabisa ikawepo kwa kiwango kikubwa sana. Katika Mkoa wangu wa Arusha, hasa katika Wilaya yangu ya Arumeru na Ngorongoro ya mwenzangu hapa tuna tatizo kubwa la njaa kwa sababu mvua zimekatika mapema na sasa hivi Mkoa mzima una shida ya njaa kwa sababu hatuna mavuno ya kutosha. Naomba wakati Mawaziri husika waki-*sum up* wakumbuke hili la njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme naunga mkono hoja ya Bajeti. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi hii nami nitoe mchango wangu katika hoja iliyoko Mezani sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kwa kutoa mkono wa rambirambi kwa Wapigakura na wanafamilia wa Marehemu Mbunge, mwenzetu Abu Kiwanga, aliyefariki hivi karibuni. Mungu ailaze roho yake mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wanawake wote wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, nachukua nafasi hii kutoa pongezi zetu za dhati kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa kuchaguliwa na Chama chetu kuwa Wagombea wa kuwania Kiti cha Urais wa Jamhuri ya Muungano na Makamu wa Rais na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, CCM haikufanya makosa hata kidogo kwa kuwateua wao kuwa Wagombea wetu. Nina uhakika kabisa kwamba Chama chetu cha Mapinduzi kitashinda kwa kishindo kikubwa sana katika uchaguzi ujao ambao utakuwa huru na wa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie sasa katika kutoa mchango wangu wa Bajeti hii ya Serikali pamoja na mipango kwa mwaka 2005/2006. Ninaanza kwa kutoa pongezi kwa Mawaziri wetu wawili, Mheshimiwa Basil Mramba na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kusimamia uchumi na maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ni nzuri na ni nzuri hasa kwa vile haikuongeza viwango vya kodi vile ambavyo vinawagusa wananchi moja kwa moja. Hamna nyongeza ya viwango vya kodi vya huduma wala bidhaa wanazotumia wananchi kwa wingi. Isipokuwa tu wameongeza kodi katika vileo na sigara kitu ambacho ni sahihi kabisa kwa sababu kodi hii ni katazo ya kutumia hivi vitu kwa sababu vinaathiri kiwiliwili cha binadamu. Vile vile ni vianzio vizuri tu vya mapato, kwani si rahisi mnywaji wa kinywaji ambacho kina *alcohol* kuacha kunywa hata ukimpandishia bei ukasema kama ni katazo aache kunywa atakunywa tu. Kama amezoea kunywa chupa tatu kwa siku ataendelea kunywa chupa hizo hizo hata kama itasababisha kubadilisha mwendo wa matumizi ya familia, lakini atakunywa tu. Ikishindikana kabisa, basi atatafuta kinywaji mbadala ambacho vile vile ni cha *alcohol* kinachopatikana Mitaani, lakini atakunywa. Kwa hiyo, ni kianzio kizuri cha mapato vile vile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanza kutoza kodi ya mapato kwa kiwango cha Sh.80,000/= badala ya Sh.60,000/= kimepokelewa vizuri sana na wananchi pamoja na Wafanyakazi kwa sababu kimewawezesha kubakisha kiasi zaidi ya fedha za matumizi kwa maana ya *disposable income*. Tunajua kuwa mfanyakazi mmoja anatakiwa kuhudumia familia kubwa ya kuanzia watu watano na kuendelea na kwa vile tuna-*extended families* kwani watu wengi tu wanahitaji kutumia fedha hizo. Kwa hiyo, kufanya hivi ni sahihi kabisa kwa kuwasaidia huo mzigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa uchumi wa asilimia 6.7 siyo mchezo, hapa Serikali inapaswa kupongezwa kabisa na kila Mtanzania. Kwa wale ambao hawaoni kuwa kimefanyika kitu cha maana,  hilo ni tatizo lao. Lakini ni kitu cha maana kimefanyika na kila mmoja anaona. Barabara zipo, hospitali zinajengwa, biashara zimekua, mawasiliano yanaendelea, iliyobakia hapa ni wananchi wenyewe tu kutumia hizi fursa ambazo zipo kwa manufaa na kujipatia wao wenyewe kipato. *(Makofi)*

Ukitoa mfano tu, kabla ya ujenzi wa barabara ilikuwa bidhaa zinaozea makapuni, hakuna wanunuzi, haziwezi zikasafirishwa kutoka *point A* kupelekwa *point B.* lakini sasa hivi watu wanafanya hivyo na kujipatia kipato chao. Mawasiliano yamekua tunaona viosiki vya kuuzia kadi za simu, vimezagaa mitaani watu wanajipatia riziki zao kwa maendeleo haya haya. Sasa kama watu hawaoni, kazi kwao! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii vile vile kupongeza Serikali kupitia *TRA* kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukusanya mapato. Mapato yameongezeka kufikia makusanyo ya Shilingi bilioni 145 kwa mwezi. Ni kazi nzuri sana ambayo wanastahili pongezi.

Kama alivyozungumza Mheshimiwa Waziri wa Fedha hapa kuwa haikuja tu hivi hivi, haikujileta yenyewe, lakini kuna kazi ambayo imefanyika. Mojawapo ni kuboresha mifumo ya ukusanyaji, taratibu za kodi, sheria ambazo zilikuwa zinaletwa hapa, tunazifanyia *amendments*, kuongeza *voluntary compliance* ya walipa kodi kwa kuwashirikisha katika kufanya maamuzi ya kikodi na hii imeweza kuziba mianya ya wakwepa kodi. Kwa hili vile vile, Serikali tunaipongeza kwa kazi nzuri iliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kama Serikali inaweza kwenda kifua mbele popote pale na kujitapa ikiwa inaweza kutumia mapato yake ya ndani kulipia mishahara ya wafanyakazi wake kwa asilimia 100 na kulipia matumizi mengine kama vile *OC* kwa asilimia 100. Serikali imeweza kufanya hili! Hii inakuwa ni kama baba ambaye anaweza kuihudumia nyumba yake kwa chakula na matumizi mengine muhimu. Kwa hiyo, Serikali yetu imeweza kufanya hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato yatokanayo na kodi, yanachangia asilimia 45.4 ya mapato yote na mapato yote ya ndani yanachangia asilimia 58.5. Kwa maana hiyo, kuna lile pengo la asilimia 41.3 ambalo inabidi tupate ufadhili kutoka nje. Tukipiga mahesabu hapa ya haraka haraka, sura ya Bajeti yetu ambayo imeonyeshwa katika ukurasa wa 55 wa hotuba ya Waziri wa Fedha, inazungumza kuwa mapato ya ndani ni Shilingi bilioni 2451.1 na matumizi ya kawaida ukitoa yale madeni ambayo tulikuwa tunatakiwa tulipe, wakati huo yalikuwa ni bilioni 2262.7 hapa inapatikana ziada ya bilioni 188.4.

Kabla ya madeni haya kufutwa ilikuwa hapa kuna nakisi ya bilioni 339.7 ambayo nakisi hii itafidiwa na mikopo na misaada kutoka nje ikiwemo ile ya *HIPC* ya Shilingi bilioni 709.7. Sasa kwa maana hiyo, hapa nilipata utata kidogo, nilipokwenda kutazama kasma za matumizi ya maendeleo, pale kuna kianzio kimoja cha ndani ambacho kinasema ni Shilingi bilioni 370.073 ambazo ni fedha zitakazotumika kwenye Miradi ya Maendeleo kama ni kianzio cha ndani. Lakini kwa mahesabu haya, hata hizi bilioni 370 ni fedha kutoka nje, ni mikopo na misaada inayoingia ndani kusaidia Bajeti.

Kwa hiyo, hiki ni kianzio vile vile kutoka nje, kwa maana hiyo basi, matumizi ya maendeleo yote yanafidiwa asilimia 100 na mapato kutoka nje ikiwa ni mikopo, ikiwa ni

misaada. Kwa hiyo, hapa kidogo niliona kuna kiini macho kimejificha kwenye mahesabu. Lakini Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya *winding-up* atakuja kutuwekea sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, bado ipo kazi kubwa ya kufanya kwa sababu tunahitaji hapa huruma za wenzetu kutoka nje kutusaidia. Si jambo baya, kila mmoja anakopa, tunajua hata Marekani wenyewe wanakopa. Lakini katika matumizi ya maendeleo kuwa hakuna fedha zetu za vianzio vya ndani. Ni tatizo! Kwa maana hiyo, bado ipo kazi kubwa kwa Serikali pamoja na Watanzania wote ya kuongeza mapato kutoka vianzio vyetu vya ndani angalau tuwe na sehemu ya mapato ya ndani yanayotumika kwenye Miradi ya Maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tubadilishe picha hii mimi naona hii mikakati yetu ambayo tumeiweka ya MKUKUTA ya MKURABITA ni mizuri lakini iwe mikakati tekelezeka, kama haikutekelezeka tunarudi pale pale. Tanzania tuna neema ya watu, tuna watu karibu milioni 36, lakini watu hawa wengi wao hawako *taxable,* hawawezi kulipishwa kodi, tulijaribu kodi ndogo ndogo mwisho tukaona ni kero na tukafuta. Hivyo, wanaochangia katika mapato ya Serikali ni wachache mno, ni asilimia ndogo tu ya watu.

Kwa maana hiyo, tujaribu basi kutafuta mbinu kama tulivyosema, hiyo mikakati ikitekelezeka, pengine hali ya mapato ya kichwa kwa watu wetu yataongezeka na watu wetu wanaweza kuchangia katika kulipa kodi za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi mkuu wa uchumi wa nchi yetu tunasema ni kilimo, lakini sasa kilimo chenyewe bado hakikidhi haja. Asilimia kubwa ya kilimo ni kilimo cha kujikimu na wakati mwingine tunashindwa hata kujikimu. Kwa maana hiyo, kilimo kipatiwe miundombinu yote ili kiweze kuendelea ikiwemo mbolea, umwagiliaji na mengine kama walivyozungumza wenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tuendelee kutafuta Wawekezaji katika viwanda vinavyoweza kutumia malighafi ya kilimo, angalau kuwe na *linkage* baina ya kilimo chetu na viwanda ili watu wapate soko la uhakika na vile vile ajira iongezeke.

Sekta isiyo rasmi inaajiri watu wengi karibu asilimia sita, nayo ifanyiwe utafiti tuone namna gani tunaweza kuwasaidia watu hawa ili wazalishe bidhaa zenye ubora ili ziweze kupatiwa soko na wao kuongeza kipato ili baadaye kuchangia kwenye mapato ya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vya *VETA* navipongeza sana kwa kazi nzuri, wanajitahidi na vijana wetu wamehamasika na hata wazee wanakwenda kujifunza pale. Kwa hiyo, Bajeti iliyopangwa wapatiwe kwa asilimia 100 na ile ya maendeleo vile vile wapatiwe ili wapanue shughuli zao na Walimu wapelekwe kujifunza zaidi kwa sababu sayansi na teknolojia na mambo ya kiufundi yanabadilika siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kidogo kuhusu Tume ya Pamoja ya Fedha. Tume ya Pamoja imeundwa hapa hapa na Sheria tumeipitisha hapa Bungeni, lakini sasa

wananchi wanajiuliza nini kinaendelea, wako kimya mno. Wananchi wanajiuliza kuna nini kinaendelea? Kwa hiyo, viongozi wa Tume hii wafanye utaratibu wa kutujulisha nini kinaendelea ili kila mmoja aridhike kuliko kukaa kimya tu. Jambo lingine ni uvuvi wa bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na vuta nikuvute ya muda tu kuhusiana na hasa mapato na utoaji wa leseni katika eneo hili. Sasa Mheshimiwa Waziri aje atueleze hapa wamekubaliana nini? Makubaliano yakoje baina ya Serikali hizi mbili? Kwa sababu ni suala la kukaa wao Serikali mbili wakaamua wakakubaliana nini cha kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la UKIMWI. UKIMWI ni tatizo kubwa, kila mmoja anajua na wagonjwa wa UKIMWI wako wengi na vifo vimeongezeka, *statistics* zinaliza. Katika mwaka 2002 watu karibu 576,000 wamekufa. Kweli kuna magonjwa mengine yanachangia katika hivi vifo, lakini UKIMWI unaendelea kumaliza watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye miradi ya maendeleo ya UKIMWI fedha ndiyo kama nilivyosema zote kutoka nje na kuna madawa yanahitajika. Sijui madawa hayo yatapatikana vipi? Ninachoshauri ni kuwa, hizi fedha zilizosamehewa madeni, zilizopangwa kulipiwa madeni ziende katika kununulia madawa tu ya kuongezea maisha kwa wagonjwa wa UKIMWI ili kila mmoja aweze kupata hayo madawa. Kwa sababu huwezi ukawapa wachache tu wakati madaktari wameshathibitisha wagonjwa wengi wanastahiki kupewa.

Kwa hiyo, kuwe na dawa nyingi zienee katika Zahanati zetu zote na ili watu waweze kuzipata kwa wale wanaozihitaji. Kwa sababu ni haki ya kila mtu kuishi, huwezi ukampa dawa mmoja mwingine ukamwacha ili afe, haiwezekani! Kuishi ni haki ya kila mtu na Watanzania wote tuko sawa. Kwa hiyo, madawa haya apatiwe kila mmoja anayehitaji ili aweze kuongeza maisha yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la utafiti. Suala la utafiti ni kitu muhimu sana katika maendeleo ya nchi. Lakini sisi bado hatuoni kama tumetoa kipaumbele cha kutosha. Kuna Taasisi zetu zinatafiti mambo ya mbegu za kilimo na mambo mengine, wanatoa mbegu nzuri tu zinastahimili magonjwa na mambo mengine ambayo yanafanana na mazingira yetu. Lakini utakuta hazipewi fedha za kutosha kufanya utafiti wake.

Kwa mfano, kuna hii Taasisi ya *TPR* inafanya kazi nzuri tu katika kutafiti mambo ya viasilifu sahihi kwa kuondoa visumbufu vya magonjwa. Lakini katika Bajeti ya mwaka jana ya matumizi yoyote ya Taasisi hiyo, wamepatiwa asilimia tatu tu ya jumla ya matumizi kuwa ndiyo ziende katika kasma ya utafiti. Inakuwa kwamba hata wale Watendaji ambao wana moyo wa kufanya kazi wanavunjika moyo kwa kutokupewa fedha za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la utafiti tulipe kipaumbele. Matunda yanayopatikana kutokana na huu utafiti yafikishwe kwa wananchi ambao ndiyo watumiaji wa tafiti hizi zisibakie tu katika *shelves* kule maofisini pamoja na kwenye mafaili, lakini manufaa yenyewe hayapatikani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imebidi niache mengine, mengine kwa kurukaruka niliona kengele ya kwanza nilishapigiwa. Kwa hayo machache, naunga mkono hoja asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi kwa kupatiwa nafasi ya kuchangia hoja hizi mbili muhimu ya Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji pamoja na Waziri wa Fedha. Kabla sijazungumza na mimi naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa niaba ya wananchi wa Korogwe na Mkoa wa Tanga kwa ujumla kutoa rambirambi zangu kwa Hayati Abu Kiwanga kwa kifo ambacho kimempata Mbunge mwenzetu. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba na mimi niungane na wenzangu kutoa pongezi za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa na Chama Cha Mapinduzi kubeba tiketi ya Chama mwezi wa Kumi katika Uchaguzi wa Taifa hili kwa nafasi ya Urais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba hii, naomba niigawe katika mafungu matatu. Kwanza nitapongeza, pili nitazungumzia kero na ushauri ambao ningeomba niitoe kwa Serikali. Nikianza na la kwanza, naomba niseme wazi kabisa kwamba naunga mkono. Naunga mkono asilimia mia hotuba zote mbili. *(Makofi)*

Nawapongeza Mawaziri wote, nikianza na Mheshimiwa Dr. Kigoda kwa hotuba yake nzuri na kwa kutuwekea mipango mizuri katika nchi yetu. Tukubali kabisa ya kwamba bila ya mipango mizuri hakuna maendeleo. Kwa hiyo, naomba nimpongeze kwa dhati kwa jinsi ambavyo ameweza kuweka hotuba yake vizuri iliyojikita kuelezea tulikotoka, tulipo sasa na tunapokwenda. Kwa kweli, nampongeza kwa dhati. Hongera Dr. Kigoda. *(Makofi)*

Naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Mramba kwa hotuba yake na hali halisi ambayo imejionyesha katika bajeti. Sisi ambao tuliingia katika Bunge hili mwaka 1995 tumejikuta kila bajeti kila mwaka inaongezeka, si kuongezeka tu lakini mambo yanaboreka na uchumi unakua. Mimi naomba niipongeze nchi na niipongeze Serikali kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Nawapongeza Waheshimiwa wa *TRA* kwa kazi nzuri ya ukusanyaji wa mapato na Wataalam wote wa Wizara zote hizi mbili kwa kazi ambayo wameonyesha. Pia, nisiache kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ndiyo wanaopitisha Miswada ya kufanikisha uchumi katika suala hili. Bila

Miswada hiyo nadhani pia mambo yasingejipa. Lakini kwa kweli lazima tupongezane. Nawapongeza sana. *(Makofi)*

Sasa baada ya kutoa pongezi, kuna maneno machache ambayo huwa yanazungumzwa na wenzetu wapinzani hapa. Ni vizuri tukayasema haya kwa sababu tunayazungumza na wananchi wanatuelewa na tuko kwa wananchi. Kwa kweli mambo ambayo yamefanyika katika kipindi hiki hata kipofu ambaye haoni, atakuwa ameona haya mambo yaliyofanyika. Kwa sababu ni mazuri mno! Yako mambo mazuri ya huduma za jamii yamefanyika katika nchi hii ambayo hayana utata. Kama mtu ana macho haoni, basi unashangaa na kuna maneno yalizungumzwa juzi hapa ya kusema kwamba eti sera za CCM hazitekelezeki. Sio kweli! Haya ni maneno ya kujiremba tu. Bwana Yesu alikuwa na wale wanafunzi wake walikuwa 12. Alipofariki siku ya kufufuka aliwatokea. Alipowatokea mmoja kati yao anaitwa Tomaso, anaambiwa Bwana Yesu kafufuka. Akasema, hata hajafufuka! Mpaka atie vidole kwenye makovu yake. Sasa ndiyo hawa wenzetu bado wengine ni Matomaso. Tunao Matomaso wengi sana. Lakini cha msingi ni kumshika tu umpeleke akaone mashule, akaone darala la Mkapa, akaone na mengine mengi tu ambayo yamefanyika. Ndiyo hayo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tujue kabisa nchi hii tuna Matomaso chungu mbovu ambao lazima tuwabadilishe waone kwamba nchi hii inakwenda. Kwa kweli mimi naomba niipongeze Serikali, imefanya kazi nzuri sana na wananchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo nataka nilizungumze ni kero. Mambo mazuri kama haya yaliyofanyika, kuna vikero vidogo vidogo visipoondolewa kwa wananchi kuna hali ya kunyong'onyea na kuondoa juhudi za wananchi. Mimi naomba nizungumzie kero moja nyeti ambayo nimeizungumzia na kwa bahati nzuri ninamalizia Ubunge wangu na nimekuwa nikiizungumza miaka yote hii nisiposema ninaweza nisirudi na siyo vizuri. Ninaomba niiseme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kuna kitu ambacho katika suala zima la ubinafsishaji tunabinafsisha, lakini ulipaji wa mafao kwa wafanyakazi linatuletea kero katika nchi yetu. Naomba Serikali walione hilo na liondoke. Ni kero sugu. Kwa nini ninalisema hili? Nalisema kwa mfano hai ambao Bunge hili na nyinyi wenyewe humu ndani mnafahamu na Mwenyekiti unalifahamu, nimekuwa nikiimba wimbo. Juzi hapa katika Bajeti ukitazama sijui ni ukarasa gani, lakini upo sina haja ya kuutamka, Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kulipa wafanyakazi wa *East African Community.* Mimi napongeza sana hatua ya Serikali. Naipongeza sana na wafanye hivyo. *(Makofi)*

Lakini wako ambao walikuwa wanadai madeni ya ndani, wafanyakazi waliokuwa Mamlaka ya Mkonge Tanzania. Ni wengi sana na wengine na Mashirika mengine, wala sina haja ya kuyasema. Sio nzuri kwa rekodi ya nchi yetu. Naomba walipwe. Napata taabu sana ninapotembelea katika maeneo yangu, ukienda maeneo ya Mgombezi, mashamba yote ya Mkonge, ukienda Hale, ukienda Magoma, swali la kwanza mafao yetu, zaidi ya watu 500, haipendezi.

Nilikuwa naiomba Serikali, ina fedha, haina fedha, ikope, inyang'anye iwalipe watu hao. Kwa sababu tunapata matatizo! Ni kero sugu. Naomba ilipe watu wale! Kama tumeweza kutenga fedha kulipa watu wa *East African Community for all those years* ningeomba suala hili la mafao ya Mamlaka ya Mkonge waliopewa na fedha zao zilitengwa, basi watu hao walipwe kwa juhudi zote na sizungumzii, mfano wa Mkonge natoa ni mfano kwa sababu unanipata mimi, lakini najua kuna tatizo hili Musoma kwenye maeneo ya viwanda vya Musoma na viwanda vingine na Mashirika mengine kama *TTCL* na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri atafute uwezekano wa kuzipata fedha hizi kwa juhudi zote ili ziweze kulipwa. *(Makofi)*

Lingine ambalo naona ni kero ambalo naliona ni nyeti tunazungumzia Wizara zote kwenye Bajeti zao wamezungumzia suala la MKUKUTA, kupambana na umaskini. Lakini huwezi kupambana na umaskini kama mwananchi hana ardhi. Sasa moja ya tatizo ambalo tunalo sisi ni ardhi. Ziko Kata ambazo nimezipigia kelele hapa, nimezungumzia ambazo mwaka 1997 ziligawiwa wakati huo Mamlaka ya Mkonge kwamba wapewe mashamba walime kwa sababu maeneo mengi ya Mkoa wa Tanga, wote mnajua, Vijiji vingi viko kandokando ya mkonge.

Wale watu waliambiwa walime na wasilime mazao ya kudumu mpaka leo na mpaka leo eneo lile limetengwa toka 1997 hekta 15,000 zimekubaliwa kutoka Wizara ya Ardhi, Rais aka-*endorse* tukagawiwa. Lakini mpaka leo wananchi wale wameambiwa kwa majina tu, hekta 400, hekta 700 hawajapewa. Naomba suala hilo liishe.

Namshukuru Dr. Kigoda kwamba Halmashauri yangu ilikuwa haina fedha, lakini yeye baada ya kupiga kelele akatoa fedha milioni 5,000 zipimwe. Lakini waliokuja kupima kutoka *PSRC* walikuja wakapima wenyewe na watu wa *Katani Limited* wakaacha kuwachukua Wenyeviti wa Vijiji na watu wa Serikali za Vijiji wakatembea nao kujua mipaka ni ipi. Leo tatizo lipo *for ten years* litakwisha lini? Wananchi wale wataondokana na umaskini lini. Naomba Mheshimiwa Waziri suala hilo ulifanyie kazi, kwa uzito wote. *(Makofi)*

Kero nyingine ambayo nilikuwa naomba niizungumzie ni kero ya bajeti hii. Bajeti ni nzuri, lakini kuna tatizo ambalo liko kwenye utendaji ambalo kama hatutaangalia tutapata matatizo makubwa. Wizara zote hazina mahusiano na Halmashauri kiutendaji. Kuna tatizo kubwa sana kati ya Wizara na Halmashauri katika utendaji. Hili lazima litafutiwe dawa. Hakuna muungano kule, kuna kero kubwa! Naomba Serikali ikae ione ni namna gani Afisa Kilimo anaweza kuwa na *direct connection* na *Ministry.* Au Afisa Ardhi ana *connection* na *Ministry* halipo, bado ni kero kubwa ambalo tunalipata katika maeneo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba bado kuna malalamiko kwamba mishahara iliyoongezwa ni kwa wafanyakazi wa Serikali. Je, hawa wafanyakazi wa Mashirika mengine au binafsi mishahara yao nani anayeshughulikia na wataongezwa vipi kwa sababu maisha ni hayo hayo na nauli ni hiyo hiyo?! Nina ushauri ufuatao:-

Naomba Miradi yote ya Umwagiliaji katika nchi hii ambayo imekwama Serikali iikwamue, kwa sababu hakuna njia nyingine yoyote ya kufanya jambo hili kama miradi ya umwagiliaji haitashughulikiwa. Kilimo cha umwagiliaji ndiyo mkombozi. Haya mambo ya kutegemea mvua jamani imepitwa na wakati. Miradi kwa mfano, kwa Mgumi umekwama, vinatakiwa vi-*box* 32 imekwama na watu hawaendelei na pale unaweza ukalima mpunga, ukafanya vitu chungu mbovu. Naomba suala hili Serikali ilione kwa nguvu zote. *(Makofi)*

Kuhusu mikopo, nilikuwa nashauri kwamba kama tumekubaliana kwamba rasilimali iliyobaki ya Mtanzania ni ardhi, wapate fedha. Mheshimiwa Mramba amesema itakwenda mpaka kwenye Kata, fedha zikipatikana. Mfano wa Mbozi usambaze nchi nzima. Isiwe Mbozi tu, Vijiji viko 10,000 vilivyopimwa ni 3,000. Haiwezekani! Serikali itoe fedha ipime Vijiji vyote Tanzania nzima ili tuweze kupata mikopo hii na tupate mitaji kwa wananchi waweze kukopa kwenye mabenki. Ndiyo kwenda na huo MKUKUTA vinginevyo tunaongelea tu MKUKUTA, MKUKUTA fedha hazifiki kwa wananchi walengwa. Naomba Serikali itatue hilo.

Tatizo ambalo nimelizungumzia ni suala la Wakurugenzi kusimamia maendeleo, kusaidiana tusisingizie TAMISEMI, Wizara *connection* TAMISEMI kuwe na *connection.* Afisa Kilimo awe na uhusiano na Wizara, kwa sababu hakuna uhusiano, kila kitu nendeni TAMISEMI. Zinapelekwa fedha za *adults* hapa, Wabunge tunapewa orodha, lakini kwa sababu kazi inayofanywa kule hatujui. Nilikuwa naomba suala hili tulifanyie kazi ili kuwe na msimamo, tuboreshe miundombinu ya kiuchumi hasa barabara za Vijijini na umeme katika maeneo mbalimbali ili tuweze kuibua uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo nilikuwa nayo, naomba Serikali iyazingatie ili tuweze kwenda na bajeti nzuri ambayo tumeletewa. Naipongeza Bajeti kwa kazi nzuri waliyofanya Serikali na ni bajeti ambayo kweli imelenga. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. IBRAHIM W. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hizi mbili zilizoko mbele yetu, hoja ya Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji na Waziri wa Fedha. Lakini awali ya yote kwa niaba ya wananchi wa Musoma Mjini, naomba na mimi niungane na wenzangu kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga pamoja na Wapigakura wote wa Kilombero kwa kumpoteza mwakilishi wao. Namwomba Mwenyezi Mungu aweze kuweka roho ya Marehemu mahali pema Peponi. Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili naomba pia kwa niaba ya wananchi wa Musoma Mjini, nichukue fursa hii kuwapongeza Wagombea wateule wa Chama Cha Mapinduzi, Mheshimiwa Jakaya Kikwete kwa kuteuliwa na Chama Cha Mapinduzi kuwa Mgombea urais kupitia Chama chetu cha CCM. Pia nimpongeze Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa kuteuliwa na Chama chetu cha CCM kuwa Mgombea urais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Pia, nimpongeze Mheshimiwa Dr. Shein kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza katika uchaguzi mkuu ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kuwapongeza Mawaziri kwa kazi yao nzuri, maana sisi kama Wabunge mahali pa kupongeza, tunapongeza na mahali pa kukosoa tunakosoa. Lakini niseme kitu kimoja kwamba hotuba za Mawaziri zimetupa mwelekeo zimetuonyesha dira ya wapi tulipo sasa hivi na wapi tunakokwenda na kwa hakika kabisa ukifanya uchambuzi wa kina utaona kwamba kwa kweli tumepiga hatua kubwa sana. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa hilo. *(Makofi)*

Lakini pia naomba niwapongeze sana *TRA* kwa sababu wamefanya kazi kubwa kwa kusimamia makusanyo ya kodi na hatimaye kuiwezesha Serikali kuweza kukusanya kiasi kikubwa cha fedha kufikia Shilingi bilioni 145 kwa mwezi. Ni hatua kubwa sana na kwa kweli hatuna sababu ya kutokuwapongeza. Lakini niseme kitu kimoja kwamba mimi ningependa kuipongeza sana Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Katika vikao vingi tuliishauri Serikali kwamba bado Serikali inaweza ikaongeza makusanyo ya mapato kama itachukua hatua fulani fulani na moja ya maeneo ambayo tuliishauri Serikali kuchukua hatua ni usimamizi wa kodi kwenye Sekta ya Mafuta na tukaishauri Serikali kwamba ikiwezekana wafunge *flow metre* kwenye maeneo ya kupokelea mafuta na wameanza kufanya hivyo pale Kurasini.

Moja ya eneo ambalo limeongezea pato au mapato haya ambayo yameongezeka kwenye makusanyo kwa *TRA* ni sehemu hii ya mafuta. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa kuchukua hatua ya kufunga *flow metre*, lakini ninachoweza kushauri ni kwamba kuna mita ambazo hazijaanza kutumika pale. Mimi na Wabunge wenzangu wa Kamati ya Miundombinu tulifika pale. Kulikuwa na mita ambazo zilikuwa hazijaanza kufanya kazi. Sasa sina uhakika kama mita hizo bado hazifanyi kazi mpaka sasa hivi au zimekwishaanza kufanya kazi.

Lakini tungependa tujue:-Je, baada ya kufungwa kwa *flow metre, impact* yake nini sasa kwenye makusanyo ya Serikali kwa upande wa mafuta? Ni kiasi gani cha fedha ambacho sasa kinakusanywa baada ya *flow metre* kufungwa? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wakati mmoja aliwahi kutamka kwamba baada ya mafanikio ya kufungwa kwa *flow metre* zoezi hili lingeendelea kwenye maeneo mengine ambayo tunadhani kuna ukwepaji mkubwa wa kodi kwenye Sekta hii ya Mafuta. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nashauri kwamba Waziri wakati atakapokuwa ana-*wind up* atueleze ni mipango gani anayo sasa ya kuhakikisha kwamba suala hili la ufungaji wa mita kwenye maeneo mengine kama Tanga, Musoma, Mwanza linafanyiwa kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ukwepaji wa kodi ya mafuta ni mkubwa sana kwenye maeneo tunayotoka sisi, watu wanakwepa kodi ya mafuta kiasi kwamba wana fedha ambazo sasa zinatishia usalama wa nchi. Maana watu wana fedha ambazo zinatokana na kukwepa kodi ya mafuta kiasi kwamba sasa wanafikiria hata kununua binadamu. Kwa hiyo, nilitaka kusema tu kwamba ni muhimu sasa Serikali ikatueleza inachukua hatua gani kuweza kupunguza hili tatizo la ukwepaji kodi ya mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka kuzungumzia ni kuhusu Mashirika yetu ya Reli. Hali ya Mashirika yetu ya Reli, *TRC* na *TAZARA* ni mbaya sana. Sisi tumepata fursa ya kutembelea ile njia ya Kati, tumepata fursa ya kutembelea reli ya Uhuru. Hali ya reli ni mbaya sana na tunapozungumzia kwa mfano suala zima la ukuzaji wa uchumi kwa Mikoa ya Ziwa na Mikoa ya Kati huwezi kukwepa matumizi ya reli ya Kati. *(Makofi)*

Mimi ushauri wangu, Sekta ya Reli bado inatozwa *fuel levy.* Kwa mfano *TAZARA* kwa mwaka mmoja wanalipa *fuel levy* takriban Shilingi bilioni moja. *TRC* wanalipa *fuel levy* takriban Shilingi bilioni mbili. Mimi nilikuwa nashauri kwamba Serikali ingeangalia kwa sababu hizi fedha zinatoka kwenda kuimarisha barabara ambayo ndiyo mpizani wa reli. Nashauri kwamba fedha hizi wangefutiwa *TRC* na *TAZARA* ili fedha hizi zitumike kuwawezesha kutengenezea njia hizi za reli badala ya fedha zile kuchukuliwa kwenda kutengeneza barabara kwa sababu tunahitaji reli na tunahitaji barabara. *(Makofi)*

Lakini kwa nini fedha za reli zichukuliwe ziende kuimarisha barabara wakati reli inakufa? Kwa hiyo, mimi nilikuwa nashauri kwamba fedha hizi za *fuel levy,* hawa *TRC* na *TAZARA* wangeachiwa ili waweze kuzitumia kuimarisha reli. Kwa sababu tayari Serikali imechukua hatua nzuri za kuondoa kodi kwenye ununuzi wa vipuri vya reli. Kwa hiyo, nadhani wakiwezeshwa pia kwa kuwaondolea hii *fuel levy* itawasaidia pia kuimarisha njia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambalo nataka kuchangia pia ni suala zima la maslahi ya watumishi wa Halmashauri za Miji, Majiji na Wilaya. Sasa hivi Serikali inapeleka fedha nyingi sana kwenye Halmashauri zetu, lakini maslahi ya watumishi wa Halmashauri zetu bado yangali chini sana na sifikirii kwamba unaweza ukambebesha mtumishi au mfanyakazi wa Halmashauri mzigo mkubwa wa kusimamia kazi za maendeleo na bajeti kubwa wakati yeye binafsi hujaangalia maslahi yake.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nashauri kwamba kuna umuhimu mkubwa kwamba Serikali ingeangalia namna gani inaweza kuboresha maslahi ya watumishi wa Halmashauri zetu za Wilaya, Miji na Majiji. Kwa sababu katika mpango mzima huu wa kupeleka maendeleo kwa wananchi, watu wanaosimamia kazi hizo ni watumishi wa Halmshauri. Sasa ukija kwenye upande wa maslahi yao kwa sababu ni duni nina hakika hiyo pia itakuwa na athari katika utendaji kazi wao wa kila siku. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri Serikali iangalie kwamba itasaidia vipi kuimarisha maslahi ya watumishi wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la ubinafsishaji. Sera ya ubinafsishaji imekuwa ni ya manufaa sana. Lakini nadhani hatuna sababu ya kudhani tunahitaji kubinafsisha Mashirika yetu katika muda wa miaka 10, miaka 20. Ni lazima tuchukue tahadhari hasa kwa Mashirika makubwa yaliyobaki ambayo yanagusa kabisa maslahi ya wananchi kwamba ubinafsishaji wake uende kwa kufanyiwa utafiti wa kina kwamba tunaweza kuchukua hata miaka 100 kufanya ubinafsishaji na si lazima tuwe sisi ambao leo tuko kwenye Serikali.

Lakini tunaweza kuacha mpango huo ukaja ukatekelezwa hata na Serikali zijazo huko mbele kwa sababu Mashirika yaliyobaki ambayo yako kwenye mpango wa kubinafsisha ni Mashirika ambayo ni nyeti. Ni Masharika ambayo yanagusa kabisa maslahi ya wananchi wetu wa kawaida na tukifanya haraka katika kuyabinafsisha tunaweza kupata matatizo. Kwa hiyo, nilikuwa namshauri Waziri mwenye dhamana ya Mipango na Ubinafsishaji, Mashirika kama *TRC*, *TAZARA,* Benki ya *NMB* tungechukua tahadhari kwa kadri itakavyowezekana kwamba tupate muda wa kutosha kufanya zoezi hili ili lifanyike kwa uangalifu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano *NMB* tulitegemea kwamba ndiyo ingekuwa Benki ya kumsaidia Mtanzania wa chini, lakini sina hakika kwamba baada ya ubinafsishaji Benki hii itabaki na jukumu hilo. Tumeona mfano kwa *NBC* ambao wakati ikibinafsishwa wawekezaji waliahidi kwamba wasingefunga matawi kwenye maeneo yasiyofanya kazi kwa faida. Lakini tulichokuja kushuhudia baadaye ni kwamba Benki baada ya kubinafsishwa maeneo yaliyofanya kwa faida Benki ilifunga matawi yake.

Mimi wasiwasi wangu ni kwamba kesi ya *NMB* na hasa wakati huu ambapo tumekubaliana kwamba mishahara ya watumishi wa Serikali ipitie Benki, ni Benki gani nyingine yenye mtandao unaoweza kufika kila sehemu nchi hii kama siyo *NMB*? Sasa tukipata wawekezaji ambao watakuja wanaangalia maeneo yanayozalisha faida, nina wasiwasi kwamba yatatokea yale yale ya *NMB* ya kufunga matawi yasiyotengeneza faida. Nina hakika kwamba katika baadhi ya matawi ya *NMB* zaidi ya matawi karibuni 20 yanaendeshwa kwa hasara.

Lakini nilidhani kwamba Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango watatueleza ni mpango au mkakati gani ambao wanapambana na rushwa ndani ya Wizara, ndani ya Taasisi zao. Tumekuwa tukizungumzia hayo kwa muda mrefu, lakini nina hakika sasa hata ushauri wetu ambao tumezungumza kwenye mikutano iliyopita, nadhani wanaufanyia kazi. Ni matumaini yangu kwamba lengo na nia yetu sisi ni kuona kwamba Serikali inakusanya mapato zaidi kuliko hapa tuliposimamia na nina hakika bado kuna vyanzo vingi ambavyo vinaweza kuipatia Serikali mapato kutoka hapa tulipo tukasogea mbele. Wenzangu wamekwishaizungumza kwamba Sekta ya Madini bado haichangii kiasi cha kutosha kwenye pato la Taifa.

Sekta ya Uvuvi tuna viwanda vya samaki kwenye maeneo tunayotoka, lakini maeneo yale sasa ambayo zamani kulikuwa na lishe ya kutosha hali ya lishe sasa hata kwenye maeneo ya Ziwa Victoria imekuwa ngumu. Tuna viwanda pale, lakini Watanzania wanaozungukwa na Ziwa wanakuwa maskini zaidi. Sasa tunasema nini faida ya kuwa na Wawekezaji kwenye maeneo yale? Kwa hiyo, nilikuwa nasema kwamba bado Serikali inaweza kutoka hapa mahala pa kukusanya bilioni 145 ikaenda mbele zaidi. Nina hakika kama nia ipo na dhamira ipo, basi tunaweza kukusanya zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona muda wangu umekwisha. Nakushukuru sana na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyoko mbele yetu. Napenda nitoe salaam za rambirambi kwa rafiki Abu Kiwanga, Mbunge wa Kilombero pamoja na familia yake na wananchi wa Jimbo lake, nawapa pole sana na ninaomba roho ya Marehemu iwe mahali pema Peponi. Ameni.

Pili, napenda nimpongeze sana *brother* Kikwete. Kwa kweli huyu *brother* ni tishio kweli! Najua sasa hivi yeye ni Rais moja kwa moja. Napenda vilevile, nimpongeze Mheshimiwa Karume kwa kuteuliwa na Mkutano Mkuu kuwa Mgombea kwa tiketi ya CCM kule Zanzibar pamoja na Dr. Shein kwa kuteuliwa kuwa Mgombea mwenza wa Mheshimiwa Kikwete. Kwa hiyo, ninawapongeza sana, ninaamini kabisa kwamba mambo sasa hivi ni poa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ila nina ushauri ufuatao:- Kwanza, vile vile napenda niwapongeze sana watu wa *TRA* pamoja na Wizara yetu ya Fedha, Bwana Mramba. Niliwahi kusema hapa *is a financial wizardry!* Hii imedhihirika, ame-*prove* ile *financial wizardry,* imejidhahirisha kamili kwamba bila hela *brother* hakuna maendeleo bwana. Hata nyumbani ukilala umekosa, hela mama anaweza kukupiga hata mwiko anasema tuondoke hapa.

Kwa hiyo, Serikali yetu ya Tanzania baada ya kuwa na hela za kutosha imeweza kufanya miradi mbalimbali ambayo kwa kweli zamani ilikuwa ni hadithi. Napenda niseme kabisa kwamba kwangu mimi Shinyanga, kwa kweli Serikali ya Rais Mkapa sina, *I don't have any complaints,* kwa sababu mambo yote yaliyoahidiwa na Mheshimiwa Mkapa, wakati anaomba kura mwaka 1995 na mwaka 2000 kwa kushirikiana na mimi mambo yote ni safi. (*Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, napenda niipongeze Serikali kwa kweli ya Mheshimiwa Mkapa, amefanya mambo. Kwa kweli mimi niliwahi hata kusema kwamba aendelee kuwa Rais, lakini ratiba yetu ndio hiyo, lakini ningependa nimshauri Mheshimiwa Kikwete kwamba awe beneti na huyu mzee ili aweze kutuokoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ningependa niseme kwamba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Mkapa kwa sisi kufutiwa madeni karibu yote na ningependa nimpongeze sana *Prime Minister,* Tony Blair, *This man has a white skin* lakini *he is an African*. *(Kicheko)*

Ametusaidia sana sababu madeni yalikuwa yametufanya vibaya sana. Kwa hiyo, mimi nampongeza sana Mheshimiwa Tony Blair na Rais Mkapa, juzi tulikuwa na Mr. Camdessus hapa. Walituambia kwamba ile *trust* na ninaamini kabisa kwamba Rais wetu atakayekuja sasa hivi ile *trust* aiendeleze. Kwa sababu kama unadaiwa, hata kulala huwezi na ukimwona anayekudai unafikiri anakuja kutafuta kumbe labda anataka kukusalimu, unaanza kumkimbia mtu kwa sababu anakudai.

Kwa hiyo nawapongeza sana Rais Mkapa, Tonny Blair, vilevile napenda niipongeze sana *Tanzania Revenue Authority (TRA)* pamoja na Wizara yetu. Wamefanya kazi nzuri sana! Mara nyingi mimi nikisema hapa kwamba kama huna hela *you are teethless man and your could be a teethless dog*. Lakini mimi kwa kweli nawapongeza sana wametuweza, mimi naamini kabisa *was the government at one time I think it was some how called bankrupt.* Lakini sasa hivi hali nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niende moja kwa moja kwenye hotuba. Kilimo cha umwagiliaji kwa kweli mimi sikubaliani kwamba bilioni mbili zinatosha na ningependa nishauri kwamba ziongezwe hizi hela kwa sababu hazitoshi unaposema kilimo ni uti wa mgongo halafu unawapa bilioni mbili, una maana gani? *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hasa!

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mimi nimesema lazima ziongezwe. Katika Jimbo langu, kwa wale ambao wameweza kuziba mito wameweza kupata mazao mazuri kabisa na njaa imeondoka na nilikuwa naomba kwamba katika suala hili la kilimo cha umwagiliaji, zitengwe hela nyingi zaidi kwa sababu mwaka 1995 tulikuwa na matatizo makubwa sana ya maji Shinyanga na nika-*declare* kwamba mimi ni Mbunge wa Maji.

Lakini sasa hivi na-*declare* kabisa kwamba mimi ni Mbunge wa Kilimo cha Umwagililaji. Kama nitabahatika kupata kura za kutosha na kurudi kwenye Bunge hili nitahakikisha kabisa kwamba lazima hela ziongezeke. Hata sasa hivi, kwa kweli nilisema nimeunga mkono, naona labda nilikuwa sijasema, kwa kweli siungi mkono kama hela za umwagiliaji hazikuongezwa. Kwa hiyo *take my record* kwamba mimi nitachukua Shilingi moja. *(Kicheko)*

Katika Jimbo langu, kuna matatizo. Kwa mfano wakulima wa Mwamalili kule Seseko *of course* nashukuru Serikali ilinipa senti kidogo zinaboresha pale na ninaona kwamba pale kidogo angalau hata njaa inapungua. Vile vile, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alinisaidia nikachimba mtaro pale Bungweto. Halafu naomba Kizumbi kule Mwamashele tuliahidiwa zamani halafu niliona hata na kitabu cha *FAO* na jina la Mwamashele lipo pale halafu na hela, lakini baadaye hela zile zikayeyuka sijui zilikwenda wapi! Gapacholi! *(Kicheko)*

Pale Ngokolo, Mazinge wana maeneo makubwa kabisa! Pale kwangu mimi pamoja na kwamba Jimbo langu linaitwa la Shinyanga Mjini, lakini nina ekari zaidi ya 2000 za umwagiliaji. Kwa hiyo, ninajua kabisa kwamba wangeliweza kumwagilia, kwa mfano Gonkolo pale Ndembezi Majinge pamoja na Mwagala pamoja na Magobeko pale kuna sehemu kubwa sana. Kwa hiyo, nitajitahidi kama itawezekana, sitaunga mkono. Kama ni bilioni mbili kwa kweli tunatania! Sasa hivi mvua zinazidi kutokomea, lazima tufanye *rain harvesting* kwa ajili ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo ningependa niongelee ni Shule ya Rajan Sekondari. Mheshimiwa Arajan alitujengea sisi *Shinyanga Secondary School* ina madarasa 36 lakini baada ya kukwama, akaikabidhi Shule Serikalini. Nilikuwa naomba

Wizara ya Elimu ihakikishe kabisa kwamba kwa kutumia *MMES* yale madarasa yanakamilishwa. *You are giving us too little money!*

**MWENYEKITI**: Bado moja.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Nataka yale madarasa yakamilishwe pale *Rajan Secondary School*, sababu kuna madarasa 36 na madarasa yale yangekamilishwa na ile Shule ingekamilishwa, kwa kweli tungekuwa tumejikomboa kabisa katika Manispaa ya Shinyanga. Kwa hiyo, ninaomba Serikali ijaribu kuangalia. Suala la rushwa, ningependa kulisemea kidogo sana. Waswahili wana methali inasema: "Palipo udhia penyeza rupia." Sasa ukitaka kuondoa rushwa, basi mwondoe udhia. Je, Serikali yetu tumeondoa udhia? Kuna udhia chungu mbovu, kero ni udhia, maana yake ni kero. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali kama kweli in nia ya kupambana na rushwa tuondoe, kwa sababu kama hujaondoa udhia, watu wataliwa rushwa tu. Palipo udhia, penyeza rupia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanja cha Ibadakuli, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi aliniahidi kabisa mwaka huu kwenye bajeti hii angekipa hela na sijaona kwa kweli hii *TCAA (Tanzania Civil Aviation Authority).* Ninaomba kiwanja hiki kijengwe kwa sababu wakati mvua zinanyesha *pilot* huwa anashindwa kushuka pale, anakwenda kushuka Mwanza na watu na Shinyanga ndio wakuu wa madini, kuna dhahabu, kuna almasi, kuna kila kitu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni Vyama vya Ushirika. Nilisema kabisa hapa kwamba Vyama vya Ushirika vikilala vimekufa, tumekufa kiuchumi. Kwa sababu hata sasa hivi msimu wa pamba umeanza tarehe 6, lakini watu hawajachangamka kwa sababu Vyama vya Ushirika havijatoka na vinadaiwa madeni lukuki na nilikuwa nasema kabisa kwamba Serikali ijitahidi kuongeza ruzuku.

**MHE. LEONARD N. DEREFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la pamba, nilikuwa naomba kwamba waongeze ruzuku ya *export credit guarantee* kwa sababu wametoa bilioni mbili na mimi nimesoma kwenye gazeti la *Daily News,* ile Kesi ya *Star Apparel* imefilisika na inadaiwa. Halafu kuna kesi ya kati ya *CRDB* na *Bank of Tanzania* ya Shilingi bilioni nne na laki tatu. Halafu zile hela walitoa bilioni mbili, *what is two billion for export credit guarantee* kwa Watanzania wote! Kama kweli tunaongea katika suala la kusema kwamba tunataka kupambana na umaskini, *I think we are joking!* Unawapaje Shilingi bilioni mbili kwa *export credit guarantee*? Hawa watu kwanza wa ile kesi ya *CRDB* pamoja na *BoT,* wanadaiwa 4.3 na hawa ningelipenda niulize Waziri wa Fedha, hawa watu wa Benki Kuu waliwapaje hii bilioni 4.3 na kuna hawa watu wa *Apparel* kuna *guarantee* gani? *I think* tunatwanga maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *I think* tunatwanga maji *this is incredible*! *SGR* tunaweka mahindi, kule kwenye Jimbo langu tunawaambia watu walime mtama, *SGR* gani inaweka mtama? Wananiambia wewe mzee *you're a crazy guy* unatuambia tuweke hata ninyi hamuitambui! Wanaweka mahindi! Ningependa nimwuliza Mheshimiwa

Waziri wa Kilimo, kwamba je, kama anasisitiza kwamba watu walime mtama, kwa nini hauweki kwenye *SGR? (Makofi)*

Sasa *this is too much! Actually* kama nitarudi, nafikiri tutapambana kikamilifu kabisa. *TAZARA* na *TRC* nilikuwa nasema kwamba Mashirika haya, *this infrastructure,* hivi kwa nini Wabunge hamwezi kutusikiliza? Wabunge tumesema *TANESCO* isiuzwe, *TRC* isiuzwe, *TAZARA* isiuzwe, *NMB* isiuzwe, hivi mnasema sisi tunasaidia Serikali, tunaisaidiaje *when we talk you don't even listen,* mnaona kama sisi wapuuzi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI**: Haya Mbunge wa Maji tunakushuru. Ndio msemaji wetu wa mwisho kwa jioni hii. Waheshimiwa Wabunge, naahirisha Kikao mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Kicheko)*

*(Saa 01.43 Usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumanne Tarehe 14 Juni, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*